



TRI-COUNTY MWONGOZO WA MWANACHAMA WA 2022

Machi 10, 2022

1-877-600-5472

TTY 711

TrilliumOHP.com



Community Health Plan®

KAUNTI-ZA-CLACKAMAS-MULTNOMAH-WASHINGTON

**Je, Unahitaji Usaидизи wa Kujuwa
Kuhusu Mafao Yako? Tupigie
simu. Tunataka kukusaidia upate
matibabu bora zaidi.**

Trillium Community Health Plan OHP

(Ikiwa ni pamoja na Trillium Behavioral Health)
13221 SW 68th Parkway, Ste. 500, Tigard, OR 97223

Ofisi yetu inaweza kufikiwa na wanaotumia kitu
cha magurudumu.

Saa*: Jumatatu - Ijumaa, 8 a.m. - 5 p.m.

Eneo la Ndani: **541-485-2155** Nambari Isiyotozwa Ada:
1-877-600-5472 (TTY: 711)

Faksi: **844-805-3991**

<http://www.trilliumohp.com>

Ikiwa unahitaji usafiri kwelekeea au kutoka kwa miadi zako
za huduma za afya, tafadhali piga simu kwa:

**MTM (Usimamizi wa Usafiri wa Matibabu au Medical
Transportation Management kwa Kiingereza)**

Nambari isiyotozwa ada: 877-583-1552 (TTY: 711)
Unaweza kupata usaидизи wa kulipia usafiri.

*Ikiwa unahitaji usaидизи nje ya saa hizi, tafadhali tuma
ujumbe au upige simu kwa Mtoa Huduma wako wa
Msingi wa Matibabu (Primary Care Provider au PCP kwa
ufupi). PCP wako ana mtu anayepokea simu wakati
wote, saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Kwa huduma za
mgogoro wa afya ya akili, tafadhali tazama sehemu ya
“Huduma za Dharura na Mgogoro wa Afya ya Akili”. Ikiwa
una dharura, piga simu kwa 911.

Mashirika ya Utunzaji wa Meno

Advantage Dental Services

Nambari Isiyotozwa Ada ya Huduma kwa Wateja
1-866-268-9631
TTY: 711

Capitol Dental Care

1-503-585-5205 au nambari isiyotozwa ada
1-800-525-6800
TTY: 1-800-735-2900

Oregon Dental Service

1-503-243-2987 au nambari isiyotozwa ada
1-800-342-0526
TTY: 1-503-243-3958 au 1-800-466-6313

RATIBA YA LIKIZO YA 2022: OFISI ZA TRILLIUM ZIMEFUNGWA

Siku ya Mwaka Mpya	Jumatatu, 3 Januari, 2022
Siku ya Kuzaliwa ya Martin Luther King Jr.	Jumatatu, 17 Januari 2022
Siku ya Kumbukumbu	Jumatatu, 30 Mei 2022
Siku ya Uhuru (inaadhimishwa)	Jumatatu, 4 Julai 2022
Siku ya Leba	Jumatatu, 5 Septemba 2022
Siku ya Kutoa Shukrani	Alhamisi, 24 Novemba 2022
Siku ya Baada ya Siku ya Kutoa Shukrani	Ijumaa, 25 Novemba 2022
Mkesha wa Krismasi	Ijumaa, 23 Desemba 2022
Siku ya Krismasi (inaadhimishwa)	Jumatatu, 26 Desemba 2022
Mkesha wa Mwaka Mpya	Ijumaa, 30 Desemba 2022

Usaidizi wa Lugha na Ukalimani

Wanachama wote wana haki ya kujua kuhusu na kutumia mipango na huduma zetu. Tunatoa aina hizi za usaidizi bila malipo:

- Lugha ya ishara;
- Wakalimani wa lugha inayozungumzwa;
- Nyenzo katika lugha zingine; na
- Breli, machapisho yenyewe herufi za saizi kubwa, na kwa njia yoyote ambayo inakufaa zaidi.

Ikiwa unahitaji usaidizi au una maswali, tafadhali pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kupitia 1-877-600-5472 (TTY 711).

Unaweza kupata mkalimani wa lugha inayozungumzwa au ya ishara katika miadi yako ikiwa unamhitaji. Unapopiga simu kwa miadi, iambie ofisi ya mto huduma wako kwamba unahitaji mkalimani na kwa lugha ipi.

Ikiwa unahitaji mkalimani wa lugha fulani au wa ishara kwa ziara za huduma za afya, unaweza:

1. Kupigia Trillium simu.
2. Kupiga simu kwa ofisi ya daktari wako na kuwaomba kuratibu mkalimani kwa ziara yako.

Maelezo kuhusu Wakalimani wa Huduma za Afya yanapatikana katika www.Oregon.gov/oha/oei.

Si usted necesita esta información en otro idioma, en letra grande, Braille o audio, llame a Trillium en uno de los números mencionados anteriormente.

Wanachama wapya wote watapokea kifurushi cha makaribisho ambacho kinajumuisha Mwongozo wa Mwanachama. Unaweza kupata nakala iliyochapishwa ya Mwongozo wa Mwanachama, au nakala katika lugha mbadala, bila malipo. Pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kupitia 1-877-600-5472; TTY: 711. Tutakutumia mwongozo kupitia kwa barua ya posta ndani ya siku 5 za kazi. Unaweza kutazama toleo la kidijitali kwenye tovuti yetu katika: www.trilliumohp.com/memberhandbook

Ikiwa utaomba tukutumie mwongozo kupitia kwa barua ya posta, tutaandika hilo katika faili yako. Ni sharti utoe idhini ili tuutume kwako kupitia kwa barua ya posta.

Kiswahili: JAMBO LA KUZINGATIA: Ikiwa huzungumzi Kiingereza, huduma za usaidizi wa lugha, bila malipo, zinapatikana kwako, ikiwa ni pamoja na tafsiri zilizoandikwa, ufasiri unaotamkwa, wakalimani wa lugha inayotamkwa na ya ishara walioidhinishwa na waliohitimu, miundo mbadala, na usaidizi na huduma za ziada, ikiwa ni pamoja na zilizoandikwa.

Piga simu kwa 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

Español (Kihispania): ATENCIÓN: si no habla inglés, tiene a su disposición servicios de asistencia lingüística sin cargo, que incluye traducciones, interpretaciones, intérpretes certificados y calificados de lenguaje hablado y de señas, formatos alternativos y servicios y asistencia auxiliares, incluidos formatos escritos. Llame al 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

Tiếng Việt (Kivietnamu): CHÚ Ý: Nếu quý vị không nói tiếng Anh, chúng tôi có thể cung cấp dịch vụ hỗ trợ miễn phí cho quý vị, bao gồm dịch vụ biên dịch tài liệu, thông dịch trực tiếp, thông dịch viên ngôn ngữ ký hiệu và ngôn ngữ nói có trình độ, định dạng khác, dịch vụ và công cụ hỗ trợ, bao gồm cả tài liệu dạng văn bản. Vui lòng gọi số 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

简体中文 (Kichina): 注意：如果您不會說英語，您可以免費獲得語言協助服務，包括書面翻譯、口譯、經過認證和合格的口語和手語翻譯、其他格式的文件以及包括書面交流在內的輔助工具和服務。請致電 1-877-600-5472；TTY：1-877-600-5473。

Русский язык (Kirusi): ВНИМАНИЕ: Если вы не говорите на английском языке, то вам доступны бесплатные услуги перевода, в том числе письменный и устный перевод, услуги присяжных и квалифицированных устных переводчиков и переводчиков жестового языка, альтернативные форматы и вспомогательные средства и услуги, в том числе письменные. Звоните по номеру 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

한국어 (Kikorea): 주의: 영어를 구사하지 않으시면, 번역, 통역, 인증되고 자격을 갖춘 통역사 및 수화 통역사, 대체 형식, 보조 지원 및 서비스, 서면 형식 등으로 언어 지원 서비스를 무료로 제공해드립니다.
1-877-600-5472번, TTY: 1-877-600-5473번으로 전화해 주십시오.

Українська (Kiyukreni): УВАГА! Якщо ви не розмовляєте англійською, вам доступні безкоштовно послуги письмового та усного перекладу, зокрема професійний усний переклад та сурдопереклад, альтернативні формати та інша допомога, зокрема письмова. Звертайся за телефоном: 1-877-600-5472; Телетайп: 1-877-600-5473.

日本語 (Kijapani): 注意事項: 英語以外での対応をご希望の方は、無料の言語支援サービスをご利用ください。文書での翻訳、口頭での通訳、認定や資格を取得している手話通訳士による口語と手話の通訳、その他の方法、筆談等の補助的支援やサービスをご利用いただけます。電話 1-877-600-5472、TTYサービス: 1-877-600-5473。

العربية: (Arabic) تنبية: إذا كنت لا تتحدث اللغة الإنجليزية، فستتوفر لك خدمات المساعدة اللغوية مجاناً، بما في ذلك الترجمات الكتابية والترجمات الشفوية ومتجمعي لغة الإشارة والمترجمين المرخصين والمؤهلين، والتنسيقات البديلة والمساعدات والخدمات المساعدة بما في ذلك الكتابية. اتصل بالرقم ٦٠٠-٥٤٧٢-١٨٧: الهاتف النصي.

Română (Kiromania) ATENȚIE: Dacă nu vorbiți limba engleză, vă sunt disponibile servicii de asistență lingvistică gratuite, inclusiv traduceri scrise, interpretări orale, interpreți autorizați și calificați pentru limbajul semnelor și limbajul vorbit, formate alternative, precum și dispozitive și servicii auxiliare, inclusiv servicii în scris. Apelați numărul de telefon 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

កម្ពុជា (Kikambodia) ប្រយ័ត្នេះ ប្រសិទ្ធភីអ្នកនិយាយភាសាអង់គេ្មៈ
មិនចាប់ទេនេះ: សេវាដំឡូលយដាក់ភាសា ដោយមិនគិតថ្លែង មានស្រាប់
អ្នក រួចបញ្ជូនទាំងភារបកប្រែសំណើ ភារបកប្រែឆ្លាប់មាត់ អ្នកបកប្រែ
ភាសាសញ្ញាណិងភាសានិយាយ ដែលមានលក្ខណៈសម្បែត្តិត្រប់ត្រាន់ និង

បានវិញ្ញា នបត្របញ្ជាក់ ទម្រង់ដៃអង់គ្លេស និងជំនួយនីងសេវានា រួម
ទាំងសំណែរោះ ទូរសព្ទមកលេខ 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473

XIYYEFFANNAA (Kikushi): HUBADHAA: Afaan Ingilizii kan hin dubbanne yoo taatan, tajaajiloonti gargaarsa afaanii, kaffaltii irraa bilisa ta'an, isiniif qophaa'aniiru: hiikkaa barreeffamaa, hiikkaa faanii/sagalee, hiiktota afaan dubbatamuu fi afaan mallattoo waraqaa ragaa qabanii fi ga'umsa qaban, filannoo foormaatii biroo, fi deggersa meeshaalee fi tajaajiloota, kan barreeffamaa dabalatee of-keessatti kan hammatu.1-877-600-5472;
TTY: 1-877-600-5473 irratti bilbilaa.

Deutsch (Kijerumani) ACHTUNG: Wenn Sie kein Englisch sprechen, stehen Ihnen kostenlos sprachliche Hilfsdienstleistungen zur Verfügung, darunter schriftliche Übersetzungen, mündliche Dolmetscher, zertifizierte und qualifizierte Dolmetscher für Laut- und Gebärdensprache, alternative Formate sowie Hilfsmittel und Dienstleistungen, auch schriftlich. Rufnummer: 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473.

فارسی کتبی (Kifarsi): توجه: چنانچه انگلیسی نمی‌دانید، خدمات کمک‌زیان رایگان، از جمله ترجمه‌های جایگزین، و ترجمه شفاهی، مترجمان زیان گفتاری و اشاره دارای گواهی و اخذ شرایط، فرمت وسایل و خدمات کمکی، از جمله موارد کتبی، درسترس شماست. با شماره ۱-۸۷۷-۶۰۰-۵۴۷۲؛ TTY: ۱-۸۷۷-۶۰۰-۵۴۷۳ تماس بگیرید.

Français (Kifaransa) ATTENTION : Si vous ne vous exprimez pas en anglais, des services d'assistance linguistique gratuits sont à votre disposition. Il s'agit notamment de la traduction des documents écrits, de l'interprétation des discours, de l'interprétation certifiée et adéquate en langue parlée et en langue des signes, d'autres formats, ainsi que des aides et services auxiliaires, y compris écrits. Composez le numéro 1-877-600-5472 ; ATS : 1-877-600-5473.

ภาษาไทย (Kithai) โปรดทราบ: หากคุณไม่ได้พูดภาษาอังกฤษ เรา มีบริการผู้ช่วยแปลภาษาให้บริการฟรี ซึ่งรวมถึงการแปลเป็นลายลักษณ์อักษร การแปลปากเปล่า ล่ามแปลภาษาและล่ามภาษา มือที่ได้รับการรับรองและมีคุณสมบัติ รูปแบบการแปลอื่นๆ รวมถึงความช่วยเหลือและบริการเสริมอื่นๆ ซึ่งรวมการเขียนเป็นลายลักษณ์อักษรด้วย โทร 1-877-600-5472 หรือส่งข้อความทางโทรศัพท์: 1-877-600-5473

Trillium Community Health Plan (Trillium) inataka kutoa matibabu na huduma bora zaidi kwa wanachama wetu.

Unafikiri Trillium Community Health Plan (Trillium) haijakutendea haki?

Trillium ni sharti ifuate sheria za jumbo na taifa za haki za raia. Haiwezi kuwashughulikia watu bila haki katika mipango au shughuli zake zozote kwa msingi wa:

- | | | | |
|--------------------|---------------------------|---------|-----------------------|
| • Umri | • Utambulisho wa kijinsia | • Mbari | • Mwelekeo wa kingono |
| • Rangi | • Hali ya ndoa | • Dini | • Ulemavu |
| • Asili ya Kitaifa | • Jinsia | | |

Una haki ya kuingia, kuondoka na kutumia majengo na huduma. Una haki ya kupokea taarifa kwa njia unayolewa. Trillium itafanya mabadiliko yanayokubalika kwa sera, mbinu na taratibu kwa kuzungumza na wewe kuhusu mahitaji yako.

Ili kuripoti matatizo au kupata maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Trillium Community Health Plan

555 International Way, Building B, Springfield, OR 97477

Nambari isiyotozwa ada 877-600-5472 (TTY 711)

<https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/member-satisfaction.html>

Tafadhali wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama kwa 541-485-2155; Nambari Isiyotozwa Ada: 1-877-600-5472; TTY: 1-877-600-5473, Jumatatu hadi Ijumaa, saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Unaweza kutumia ujumbe katika wakati mwingine, ikiwa ni pamoja na wikendi na likizo za kitaifa. Tutajibu simu yako katika siku ya kazi inayofuata. Una haki ya kutumia haki zako za mwanachama bila hatua yoyote inayoweza kukuathiri vibaya au ubaguzi. Ikiwa unahisi kwamba haki zako zimehujumiwa, unaweza kuwasilisha nung'uniko.

Pia unaweza kuwasiliana na Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson) kuitia kwa Mamlaka ya Afya ya Oregon (Oregon Health Authority) kuitia 1-877-642-0450 au TTY: 711. Simu hiyo hailipwi.

Pia unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Kutobaguliwa wa Trillium:

Geno Allen, Mratibu wa Kutokuwa na Ubaguzi

Tuma barua pepe kwa: gilbert.e.allen@trilliumchp.com

Tuma barua ya posta kwa: 555 International Way, Building B, Springfield, OR 97477

Simu: 541-650-3618, Nambari isiyotozwa ada 877-600-5472 au TTY 711

Una haki ya kuwasilisha lalamiko la haki za raia kwa mashirika haya:

Ofisi ya Haki za Raia ya Idara ya Marekani ya Huduma za Afya na Binadamu (U.S. Department of Health and Human Services Office for Civil Rights/OCR)

Tovuti: <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/smartscreen/main.jsf>

Tuma barua pepe kwa: OCRComplaint@hhs.gov

Simu: 800-368-1019, 800-537-7697 (Simu ya wenye matatizo ya kuzungumza au kusikia yaani TDD)

Tuma barua ya posta kwa: **Office for Civil Rights**

200 Independence Ave. SW, Room 509F, HHH Bldg., Washington, D.C. 20201

Haki za Raia za Mamlaka ya Afya ya Oregon (Oregon Health Authority (OHA) Civil Rights)

Tovuti: www.oregon.gov/OHA/OEI

Tuma barua pepe kwa: OHA.PublicCivilRights@state.or.us

Simu: 844-882-7889 (TTY 711)

Tuma barua ya posta kwa: **Office of Equity and Inclusion Division**

421 SW Oak St., Suite 750, Portland, OR 97204

Kitengo cha Haki za Raia cha Ofisi ya Kazi na Viwanda (Bureau of Labor and Industries Civil Rights Division)

Tuma barua pepe kwa: crdemail@boli.state.or.us

Simu: 971-673-0764

Tuma barua ya posta kwa: **Bureau of Labor and Industries Civil Rights Division**

800 NE Oregon St., Suite 1045, Portland, OR 97232

Usaidizi wa Lugha na Ukalimani	2
KARIBU KATIKA TRILLIUM COMMUNITY HEALTH PLAN	11
JE, OREGON HEALTH PLAN (OHP) NI NINI?	11
Orodha ya huduma za afya zilizopewa kipaumbele	12
Shirika la Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organization au CCO kwa ufupi) ni Nini?.....	12
Je, matibabu yanayodhibitiwa na mfumo wa malipo kwa kila huduma ni nini?.....	12
Je, itakuwaje ikiwa sitaki Trillium iwe shirika langu la matibabu yanayoratibiwa (CCO)?.....	13
Je, nitabadilishaje hadi kwa CCO tofauti?.....	13
MAELEZO YA MPANGO	14
Nitampigia nani simu ikiwa nina maswali?	14
Je, Huduma za Kuratibu Uangalizi Makini wa Wagonjwa (Intensive Care Coordination Services au ICC kwa ufupi) ni Zippi?.....	17
Baraza ya Ushauri wa Jamii.....	20
Barua ya bima ya OHP	21
Je, nitapata mkalimani vipi?	21
JE, HAKI NA MAJUKUMU YANGU YA MWANACHAMA NI YAPI?	22
Haki za Mwanachama.....	22
Majukumu ya Mwanachama	23
Haki za Abiria	24
Majukumu ya Abiria	25
JINSI YA KUPATA MATIBABU UNAPOYAHITAJI.....	26
Je, nitapata daktari au mtoa huduma vipi?	26
Je, Matibabu ya Msingi ni Yapi?	27
Je, Nitachagua Mtoa Huduma wa Msingi wa Matibabu Vipi?	27
Je, nitapanga miadi na PCP wangu vipi?	27
Je, nitabadilisha PCP wangu vipi?	28
Hapa ni baadhi ya vidokezo vya kukusaidia kuwa na uhusiano mwema na PCP wako:	28
Tunalipia maoni ya daktari wa pili	28
Nitafanya nini ikiwa siwezi kuhudhuria miadi yangu?	29

Itakuwaje ikiwa ninahitaji matibabu mara moja?	29
Itakuwaje ikiwa ninahitaji kuona mtaalamu au mtoya huduma mwingine?	29
Itakuwaje ikiwa ninapokea Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu?	29
Je, nitapata idhini ya huduma vipi?.....	30
Mafao Mengenye Yanayoliwa na Bima ya OHP	30
Je, teknolojia mpya hulipiwa na bima?.....	32
Bahashishi za daktari.....	32
Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?	33
MAFAO NA HUDUMA ZINAZOLIPIWA NA BIMA	33
OHP hulipia nini?	33
Je, nitapataje usaidizi ili kuacha kutumia tumbaku?.....	35
Muhtasari wa Orodha ya Kukagua Mafao	37
Huduma za kupanga uzazi	42
Itakuwaje ikiwa mimi ni mjamzito?.....	42
Je, nitapataje dawa zangu zinazoagizwa na daktari?	43
Je, ni dawa zipi hazilipwi na bima?.....	44
HUDUMA ZA MATIBABU YA DHARURA NA MATIBABU YA HARAKA	46
Je, dharura ya matibabu ni nini?.....	46
Huduma za gari la wagonjwa	46
Je, nitapataje matibabu baada ya dharura?	46
Je, nitapataje matibabu ya haraka?	46
Maeneo ya Matibabu ya Haraka.....	47
MAFAO NA HUDUMA ZAKO ZA MENO	48
Je, huduma za meno ni zipi?.....	48
Je, nitachaguaje mpango wa meno?.....	48
Je, nitatumiaje mafao yangu ya meno?	49
Je, Nitachagua Daktari wa Msingi wa Meno Vipi?	49
Je, nitapangaje miadi na Dakatari wangu wa Msingi wa Meno (PCD)?	49
Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?	49
Je, nitabadilishaje Daktari wangu wa Msingi wa Meno?	49
Itakuwaje ikiwa ninafikiri ninahitaji kuona mtaalamu au mtoya huduma mwingine?	49
JE, NINA MAFAO YAPI YA MENO?	50
Muhtasari wa Mafao na Huduma	50

HUDUMA ZA MATIBABU YA DHARURA NA MATIBABU YA HARAKA YA MENO	51
Je, dharura ya meno ni nini?.....	51
Je, huduma ya matibabu ya haraka ya meno ni gani?	51
Itakuwaje ikiwa siko katika makazi yangu ya kawaida na nipate dharura au kuhitaji matibabu ya haraka ya meno?	51
Je, nitapataje matibabu baada ya dharura?.....	51
MAFAO YA AFYA YA AKILI NA URAIBU WA KEMIKALI	52
Je, huduma za afya ya akili ni zipi?.....	52
Huduma za afya ya akili za watu wazima.....	52
Huduma za afya ya akili za watoto	52
JE, NITATUMIAJE MAFAO YANGU YA AFYA YA AKILI NA URAIBU WA KEMIKALI?	53
Je, nitapataje matibabu ya uraibu wa kemikali (pombe na dawa za kulevyा)?.....	53
Je, nitapataje mtoe huduma wa afya ya akili?	53
Itakuwaje ikiwa ninahitaji usaidizi wa kuchagua mtoe huduma wa afya ya akili?	53
Je, nitapangaje miadi na mtoe huduma wangu wa afya ya akili?	54
Je, nitapataje dawa zangu zinazoagizwa na daktari?	54
HUDUMA ZA DHARURA NA MGOGORO WA AFYA YA AKILI	55
Je, dharura ya afya ya akili ni nini?	55
Itakuwaje ikiwa siko katika makazi yangu ya kawaida na nipate dharura?	55
Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?	55
MALALAMIKO (MANUNG'UNIKO) NA RUFAA	56
Je, nitawasilishaje lalamiko au nung'uniko?	56
Ikiwa huduma itakaliwa – nitaombaje rufaa?	56
Jinsi ya Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi	56
Ikiwa rufaa yangu itakataliwa, nitapataje kikao cha watawala cha usikilizaji wa kesi?.....	57
Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji usikilizaji wa haraka (ulioharakishwa) wa kesi?.....	57
Je, huduma zangu zitasitishwa?.....	58
Je, nitafanya nini ikiwa nitapokea bili?	58
Wajibu wa malipo	58
Je, ni wakati upi ambapo nitalazimika kulipia huduma za afya zilizo katika OHP?	59

JE, NITATOA MAAMUZI YANGU YA MWISHO WA MAISHA VIPI?.....	60
Maamuzi ya mwisho wa maisha na Maagizo ya Mapema (Hati za Kisheria za Maelekezo Kuhusu Matibabu)	60
Tamko la matibabu ya afya ya akili.....	61
JE, MAELEZO YANGU YA KIBINAFSI NI YA FARAGHA?.....	61
Rekodi zako ni za faragha.....	61
Je, nitawasilishaje lalamiko kuhusu faragha au kuripoti tatizo la faragha?	62
TAARIFA YA UTENDAJI WA FARAGHA.....	62
JE, NITARIPOTI ULAGHAI, MATUMIZI MABAYA AU UFUJAJI UNAOSHUKIWA VIPI?	64
KUUNGANISHA HUDUMA ZAKO ZA AFYA	65
MANENO YA KUJUA	67
MADOKEZO	69

KARIBU KATIKA TRILLIUM COMMUNITY HEALTHPLAN

Tumekuwa tukiwasaidia watu wanaotumia Oregon Health Plan (OHP) tangu 1977. Tuna furaha kukuhudumia.

Tumekutumia mwongozo huu kwa sababu unapata mafao ya huduma za afya kutoka kwa OHP. Tafadhali chukua muda kusoma mwongozo huu mzima. Utapata majibu ya mengi ya maswali yako kuhusu huduma, mafao na jinsi ya kupata usaidizi ikiwa unauhitaji. Unaweza kuomba nakala ya mwongozo huu wakati wowote.

Trillium ni Shirika la Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organization au CCO kwa ufupi). Sisi ni kampuni ambayo hushirikiana na watoa huduma wa afya na washirika wa jamii wa watu wanaotumia OHP.

Watoa huduma walio katika shirika letu la matibabu yanayoratibiwa (CCO) ni pamoja na watoa huduma

wa: Afya ya Kimwili, Afya ya Akili, Afya ya Meno na MTM (Usimamizi wa Usafiri wa Matibabu au Medical Transportation Management kwa Kiingereza).

Trillium CCO hutoa usafiri wa bila malipo hadi kwa miadi ikiwa ni pamoja na huduma za afya ya kimwili, kiakili na meno.

Trillium huratibu matibabu kwa kushirikiana na kila mwanachama na watoa huduma wake wa afya ili kupata njia bora zaidi ya kutimiza mahitaji ya matibabu na yasiyo ya matibabu. Vituo vya Utunzaji wa Msingi wa Wagonjwa (Patient Centered Primary Care Homes au PCPCHs kwa ufupi) pia vinaweza kusaidia kuratibu mahitaji ya matibabu na yasiyo ya matibabu ya wanachama.

JE, OREGON HEALTH PLAN (OHP) NI NINI?

Oregon Health Plan (OHP) ni mpango unaolipia huduma za afya za Wanaoregon wenye mapato ya chini. Jimbo la Oregon na mpango wa Medicaid wa Serikali ya Marekani hulipia huduma hizo.

OHP HULIPIA:

- Ziara za daktari
- Dawa zinazoagizwa na daktari
- Kulazwa hospitalini
- Matibabu ya meno
- Huduma za afya ya akili
- Usaидizi wa kuacha kuvuta sigara, kunywa pombe na kutumia dawa za kulevyo
- Usafiri wa bila malipo hadi kwa huduma za afya zinazolipiwa na bima.

OHP inaweza kutoa vifaa vya kusikia, vifaa vya matibabu na huduma za afya za nyumbani ikiwa unastahiki.

OHP hailipii kila huduma. Orodha ya magonjwa na matatizo ya afya yanayolipiwa na bima, inayoitwa Orodha ya Huduma za Afya Zilizopewa Kipaumbele inapatikana mtandaoni katika:

<http://www.oregon.gov/oha/hsd/ohp/pages/prioritized-list.aspx>

Magonjwa mengine na matatizo ya afya kwa kawaida hayalipiwi na OHP. Matatizo hayo ya afya yanaweza kulipiwa ikiwa kuyatibu kutasaidia tatizo la afya la mgonjwa linalolipiwa na bima. Kwa mfano, mgonjwa anaweza kuwa na tatizo moja la afya linalolipiwa na bima na tatizo lingine la afya ambalo halilipiwi na bima. Tatizo la afya lisilolipiwa na bima linaweza kulipiwa ikiwa linaweza kusaidia kupata afueni kwa tatizo la kwanza. Kwa maelezo zaidi kuhusu Orodha ya Huduma za Afya Zilizopewa Kipaumbele, unaweza kupigia Trillium simu kuititia kwa 1-877-600-5472.

Orodha ya huduma za afya zilizopewa kipaumbele

Mafao ya wanachama wa Oregon Health Plan hutegemea ikiwa matatizo yao ya afya na matibabu yanapatikana katika Orodha ya Huduma za Afya Zilizopewa Kipaumbele. Tume ya Kukagua Ushahidi wa Afya ya Oregon (The Oregon Health Evidence Review Commission au HERC kwa ufupi) ilibuni orodha hii na hukutana mara kwa mara ili kuisasisha. HERC inaundwa na madaktari, wauzui, na watu wengine wanaohusika katika masuala ya afya.

Oregon Health Plan haulipii kila huduma. Huduma za uchunguzi wa kutambua magonjwa na matibabu ambazo hazipo katika Orodha ya Huduma Zilizopewa Kipaumbele hazifadhiliwi na Oregon Health Plan. Mipango yote ya matibabu yanayodhibitiwa na watoa huduma wa afya ni lazima watumie Orodha ya Huduma Zilizopewa Kipaumbele ili kuona kama wanaweza kutoa huduma chini ya OHP. Sio matatizo yote ya afya na matibabu yaliyo katika Orodha ya Huduma Zilizopewa Kipaumbele yanalipiwa na bima kwani kuna vigezo vingine ambavyo ni sharti vitimizwe.

OHP hulipia huduma zinazofaa za uchunguzi wa kutambua ugonjwa wakati ambapo mwanachama anaugua. Hii ni pamoja na uchunguzi wa kutambua ugonjwa ambao haulipiwi na bima. Ikiwa mtoa huduma wa afya ataamua kufanya uchunguzi wa kutambua ugonjwa au kutoa matibabu ambayo hayalipiwi na bima, OHP haitalipia huduma zozote za ziada kwa tatizo hilo la afya.

Trillium hulipia huduma zote zinazolipiwa na bima kwa mujibu wa Orodha ya Huduma za Afya Zilizopewa Kipaumbele na zinapotolewa kama inavyobainishwa katika Taarifa husika ya Kusudi na Maelezo ya Mwongozo ya Orodha ya Huduma Zilizopewa Kipaumbele, mradi huduma hizo zinatafahimka kimatibabu au kwa kumezwa.

Kuna tofauti ipi kati ya mpango wangu na OHP?

OHP ni Mpango wa Afya wa Jimbo la Oregon. Jimbo hufanya mikataba na Mashirika mengi ya Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organizations au CCOs kwa ufupi) ili kudhibiti huduma za afya za watu walio na OHP. Trillium ni mojawapo ya mashirika haya ya matibabu yanayoratibiwa (CCOs).

Jimbo la Oregon hubainisha mafao unayopokea. OHP hutumia mashirika tofauti ya matibabu yanayoratibiwa (CCOs) ili kuwashudumia wanachama wake. Trillium ni mojawapo ya mashirika hayo ya matibabu tanayoratibiwa (CCOs).

Shirika la Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organization au CCO kwa ufupi) ni Nini?

Trillium Community Health Plan ni Shirika la Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organization au CCO kwa ufupi). Sisi ni kikundi cha aina zote za watoa huduma wa afya wanaoshirikiana kuwashudumia watu wanaotumia OHP katika jamii yetu. Watoa huduma walio katika shirika letu la matibabu yanayoratibiwa (CCO) ni pamoja na Trillium, Trillium Behavioral Health, Advantage Dental Services, Capitol Dental Care, Oregon Dental Service na MTM. Trillium CCO hutoa usafiri wa bila malipo, unaojulikana pia kama usafiri usio wa dharura (non-emergent transportation au NEMT kwa ufupi) na huduma za afya ya kimwili, kiakili na meno katika Kaunti zote za Washington, Clackamas na Multnomah.

Je, matibabu yanayodhibitiwa na mfumo wa malipo kwa kila huduma ni nini?

CCOs (Mashirika ya Matibabu Yanayoratibiwa) ni aina ya matibabu yanayodhibitiwa. Mamlaka ya Afya ya Oregon (Oregon Health Authority au OHA kwa ufupi) inataka huduma za afya za watu wanaotumia OHP kudhibitiwa na kampuni za kibinafsi zilizowekwa kufanya hilo tu. OHA hulipa kampuni za matibabu yanayodhibitiwa kiasi kilichowekwa cha pesa kila mwezi ili ziwapatie wanachama wake huduma za afya wanazohitaji.

ITAKUWAJE IKIWA NINATAKA KADI HURU YA OHP BADALA YA TRILLIUM?

Huduma za afya za wanachama wa OHP ambazo hazipo katika matibabu yanayodhibitiwa hulipiwa moja kwa moja na OHA. Hii huitwa malipo kwa kila huduma (fee-for-service au FFS kwa ufupi) kwa sababu OHA huwalipa watoa huduma ada kwa huduma wanazotoa. Hii pia huitwa kadi huru. Wazaliwa wa Marekani/wazaliwa wa Alaska wanaweza kuwa katika CCO, lakini wanaweza

kuomba kubadilisha ili watumie Kadi Huru ya OHP wakati wowote. Pia unaweza kuomba kutumia Kadi Huru ya OHP ikiwa pia unatumia Medicare kando

na OHP. Watu wanaotumia Medicare na OHP wanaweza kuwa katika CCO, lakini wanaweza kuomba kubadilisha mafao yao ya afya ya kimwili hadi kwa Kadi Huru ya OHP wakati wowote. Mwanachama yeote wa CCO aliye na sababu ya kimatibabu ya kutumia FFS anaweza kuomba kuondoka kwa matibabu yanayodhibitiwa. Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha OHP kuititia 1-800-273-0557 kinaweza kukusaidia kuelewa na kuchagua njia bora zaidi ya kupokea huduma zako za afya.

Je, itakuwaje ikiwa sitaki Trillium iwe shirika langu la matibabu yanayoratibiwa (CCO)?

Wakati ambapo una tatizo la kupata matibabu yanayofaa, tafadhali turuhusu tujaribu kukusaidia kabla ya kubadilisha CCOs. Piga simu tu kwa kitengo chetu cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472, TTY 711 na uombe Mratibu wa Matibabu. Ikiwa bado unataka kuondoka au kubadilisha shirika lako la matibabu yanayoratibiwa (CCO), piga simu kwa kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja. Nambari zao za simu ni 503-378-2666 na 1-800-699-9075.

SHIRIKA LA MATIBABU YANAYORATIBIWA (CCO) LINAWEZA KUOMBA MAMLAKA YA AFYA YA OREGON KUKUONDOA KWA WANACHAMA WAKE IKIWA:

- Unawadhulumu wafanyakazi wa CCO au watoa huduma;
- Utafanya ulaghai, kama vile kumruhusu mtu mwingine kutumia mafao yako ya huduma za afya.
- Ikiwa utafanya kitendo cha vurugu, au kutishia maisha ya watu, kwa vurugu ya kimwili kwa mtoe huduma wa afya, wafanyakazi wa mtoe huduma, wagonjwa wengine, au wafanyakazi wa Trillium, kwa njia ambayo inaathiri vibaya mno uwezo wa Trillium wa kukuhudumia wewe au wanachama wengine.

Ikiwa tabia ya dhuluma inatokana na tatizo lako la afya, basi sio sababu inayostahiki ya kuondolewa.

SHIRIKA LA MATIBABU YANAYODHIBITIWA (CCO) HALIWEZI KUOMBA MAMLAKA YA AFYA YA OREGON KUKUONDOA KWA WANACHAMA WAKE IKIWA:

- Una mabadiliko hasi kwenye hali yako ya afya;
- Unatumia huduma nyingi za afya;
- Unafanya mambo bila ushirikiano au kwa usumbufu kwa sababu ya mahitaji yako maalum;
- Wewe ni mwanachama wa daraja linalolindwa ambalo linaonyesha kwamba unaweza kuhitaji huduma nyingi za matibabu;
- Una tatizo la afya au historia inayoonyesha kwamba anaweza kuhitaji huduma nyingi za afya; au
- Una ulemavu wa kimwili, uwezo wa kufikiri, ukuaji au wa akili.

Ili kupata maelezo zaidi, piga simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472. Pia unaweza kupiga simu kwa kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja kuititia 1-800-273-0557 au 800-699-9075. Unaweza kuuliza kuhusu wakati ambapo shirika la matibabu yanayoratibiwa (CCO) linaweza kuomba kusitishwa kwa uanachama wako (kukatizwa kwa usajili), maondoleo ya masharti ya kawaida ya usajili wa muda au maondoleo ya masharti ya kawaida ya usajili.

Wanachama watapokea taarifa iliyoandikwa ya haki za kukatizwa kwa usajili angalau siku 60 kabla ya kuanza kwa kila kipindi cha usajili.

Je, nitabadilishaje hadi kwa CCO tofauti?

Iwapo unataka kubadilisha ili utumie CCO tofauti, wewe au mwakilishi wako anaweza kufanya hivyo kwa kutamka au kwa maandishi. Pia unaweza kupiga simu kwa kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja kuititia 503-378-2666 au 1-800-699-9075. Mabadiliko hayo yataanza kutumika katika mwezi wa kwanza baada ya uidhinishaji wa OHA. Kuna nafasi nyingi za kufanya mabadiliko mradi shirika lingine la matibabu yanayoratibiwa (CCO) linakubali usajili.

- Ikiwa hutaki shirika ulilopewa la matibabu yanayoratibiwa (CCO), unaweza kulibadilisha katika siku 90 za kwanza baada ya kujisajili.
- Ikiwa ulikuwa unatumia OHP hapo awali, katika siku 30 za kwanza baada ya kujisajili katika CCO.
- Ikiwa umesajiliwa kwa miezi 6 katika shirika lako la matibabu yanayoratibiwa (CCO), unaweza kuomba kubadilisha CCO.

- Unapojiandikisha upya kwa bima yako ya Oregon Health Plan (kwa kawaida mara moja kwa mwaka) Unaweza kubadilisha CCOs mara moja kwa kila mwaka kwa sababu nyingine yoyote.

UNAWEZA KUOMBA KUBADILISHACCO WAKATI WOWOTE IKIWA:

- Ikiwa mwanachama atahama kutoka kwa eneo la huduma la CCO, anapaswa kuwasiliana na ama Kituo Pepe cha Ustahiki cha OHP kuititia 800-699-9075 au Kitengo cha Huduma kwa Wateja kuititia 800-273-0557 haraka iwezekanavyo.
- Kwa sababu ya pingamizi za kimaadili au za kidini, Trillium haitoi huduma unayotafuta.
- Wakati unahitaji huduma zinazohusiana zifanywe kwa wakati mmoja, lakini sio huduma zote zinazohusiana zinapatikana ndani ya mtandao, na mtoe huduma wako wa msingi wa matibabu au mtoe huduma mwingine abainishe kwamba kupokea huduma hizo kwa wakati tofauti kutakuweka katika hatari isiyohitajika (Kwa mfano, upasuaji wa kujifungua na kufungwa kwa neli za falopia).

Ikiwa OHA itaidhinisha kukatizwa kwa usajili, utapokea taarifa kuhusu hilo. Unaweza kuwasilisha nung'uniko ikiwa hujaridhishwa na mchakato au uombe kusikizwa kwa kesi ikiwa hukubaliani na uamuzi wa kukatizwa kwa usajili.

Je, Trillium hufanya kazi vipi?

Trillium huratibu matibabu unayopokea kwa kushirikiana na kila mwanachama na watoe huduma wake wa afya ili kupata njia bora zaidi ya kutimiza mahitaji ya matibabu

na yasiyo ya matibabu. Kwa mahitaji yasiyo ya matibabu, Vituo vya Utunzaji wa Msingi wa Wagonjwa (PCPCHs) vitawasaidia wanachama walio na wasiwasi, mfadhaiko, na uraibu wa tumbaku, dawa za kuleyya na pombe. Trillium hufuatilia mtandao wake katika aina zote za watoe huduma ili kuhakikisha mtandao toshelevu.

Wakati mwingine huwa tunatoa huduma ambazo Huduma ya OHP ya Malipo kwa Kila Huduma hailipii. Una haki ya kuomba na kupokea maelezo ya ziada kuhusu muundo na uendeshaji shughuli wa Trillium. Kwa maelezo ya ziada kuhusu muundo na uendeshaji shughuli wa Trillium, wasiliana na Trillium kuititia 1-877-600-5472, au TTY 711.

Kituo cha Utunzaji wa Msingi wa Wagonjwa (PCPCH) ni nini?

Tunataka upate matibabu bora zaidi. Njia moja tunayojaribu kufanya hivyo ni kuwaomba watoe huduma wetu wachukuliwe na Mamlaka ya Afya ya Oregon (OHA) kama Kituo cha Utunzaji wa Msingi wa Wagonjwa (PCPCH). Hilo linamaanisha kwamba wanaweza kupokea fedha zaidi ili kuwafuatilia wagonjwa wao kwa karibu ili kuhakikisha kwamba mahitaji yao yote ya matibabu, afya ya meno na afya ya akili yametimizwa.

Unaweza kuuliza kliniki au ofisi ya mtoe huduma wako ikiwa wao ni PCPCH. Huduma za afya unazopokea ni muhimu kwetu! Tunashughulikia mafao na maswali yako katika eneo lako. Ikiwa unahitaji matibabu mara moja, tupigie simu na tutakusaidia kupata matibabu unayohitaji. Asante kwa kuturuhusu tukuhudumie.

MAELEZO YA MPANGO

Nitampigia nani simu ikiwa nina maswali?

PIGIA TRILLIUM SIMU IKIWA:

- Wewe ni mgeni kwenye Trillium na unahitaji matibabu mara moja.
- Unataka kubadilisha au unataka usaizidi wa kupata Mtoe Huduma wa Msingi wa Matibabu (Primary Care Provider au PCP kwa ufupi).
- Unataka kubadilisha au unahitaji usaizidi wa kupata Daktari wa Meno.

- Unahitaji usaizidi ili kupata huduma za afya.
- Una maswali kuhusu dai au mafao yako.
- Unahitaji kadi mpya ya Kitambulisho cha Trillium OHP.
- Una lalamiko kuhusu bima yako ya afya.
- Umehusika katika ajali au una jeraha na gharama zinaweza kulipwa na mtu mwingine.

PIGA SIMU KWA KITENGO CHA OHP CHA HUDUMA KWA WANACHAMA IKIWA:

- Utahamia katika eneo lililo nje ya eneo la huduma la Trillium.

- Utapata ujauzito au mimba ikiharibika.
- Umejifungua.
- Una maswali kuhusu kustahiki kwako.
- Utapata au kupoteza bima nyingine ya afya.
- Unataka kubadilisha mpango wako wa afya.
- Unahitaji kadi mpya ya Kitambulisho cha Afya cha Oregon.
- Ikiwa maelezo yaliyo katika Kitambulisho chako cha Afya cha Oregon au barua ya bima ya OHP sio sahihi.
- Ikiwa una maswali kuhusu barua ya bima ya OHP uliyopokea kutoka kwa Mamlaka ya Afya ya Oregon.

Itakuwaje ikiwa ninahitaji matibabu mara moja?

Ikiwa wewe ni mgeni kwenye Trillium na unahitaji matibabu au dawa zilizoagizwa na daktari mara moja, tafadhali tupigie simu. Pia, panga miadi na PCP wako haraka uwezayyo ili kuwa na uhakika kwamba utapokea matibabu yoyote muhimu yanayoendelea. Ikiwa unahitaji huduma za afya ya akili mara moja, unaweza kupiga simu kwa mto huduma yeyote aliyeorodheshwa kwenye Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium, au upige simu kwa kitengo Trillium cha Huduma kwa Wanachama kuititia

1-877-600-5472, TTY 711.

KUFIKIA MATIBABU

Trillium hutoa ufikiaji wa matibabu, ikiwa ni pamoja na lakini bila kikomo kwa:

- Huduma, usaidizi, na hati zetu zozote katika lugha na/au utamaduni unaopendelea.
- Huduma ambazo ziko karibu iwezekanavyo na mahali ambapo wanachama wanaishi au hutafuta huduma;
 - Ndani ya maili 30 au dakika 30 kutoka unakoishi ikiwa unaishi katika eneo la mjini
 - Ndani ya maili 60 au dakika 60 kutoka unakoishi ikiwa unaishi katika eneo la kijiji
- Chaguo la watoa huduma;
- Ufikiaji wa wakati unaofaa kwa matibabu na huduma zinazolipiwa na bima kwa saa 24 kwa siku/siku 7 kwa wiki inapofaa kimatibabu. Huwa tunapanga ufikiaji wa wakati unaofaa wa matibabu kwa watu walipewa kipaumbele.
- Huduma za dharura za afya ya kimwili au akili: Mara moja, au kutumwa kwa idara ya dharura.

- Matibabu ya dharura ya mdomo: Huonwa na kutibiwa ndani ya saa 24.
- Matibabu ya haraka ya kimwili: Ndani ya saa 72 au yanavyohitajika, kulingana na uchunguzi wa awali.
- Matibabu ya haraka ya mdomo: Ndani ya wiki mbili au yanavyohitajika, kulingana na uchunguzi wa awali.
- Huduma za haraka za afya ya akili kwa watu wote: Ndani ya saa 24.
- Matibabu ya afya njema ya kimwili: Ndani ya wiki nne.
- Matibabu ya mara kwa mara ya mdomo: Ndani ya wiki nane, isipokuwa ikiwa kuna sababu ya kipekee ya afya ambayo hufanya kusubiri kwa zaidi ya wiki nane kuwa sawa.
- Matibabu ya mara kwa mara ya afya ya akili: tathmini ndani ya siku saba baada ya ombi, na ziara ya pili haraka inavyohitajika.
- Matibabu bobesi ya afya ya akili na huduma za matibabu ya matumizi ya dawa za kulevy: mara moja.
- Ikiwa kipindi cha wakati kilichowekwa hakiwezi kutimizwa kwa sababu ya ukosefu wa uwezo wa kutoa huduma, ni sharti uwekwe katika orodha ya wanaosubiri. Utapata huduma za muda mfupi ndani ya saa 72 baada ya kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri. Huduma za muda mfupi ni lazima zilingane na huduma ulizoomba mara ya kwanza.
- Matibabu bobesi ya afya ya akili na huduma za matibabu ya matumizi ya dawa za kulevy: mara moja. Ikiwa kipindi cha wakati kilichowekwa hakiwezi kutimizwa kwa sababu ya ukosefu wa uwezo wa kutoa huduma, ni sharti uwekwe katika orodha ya wanaosubiri. Utapata huduma za muda mfupi ndani ya saa 72 baada ya kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri. Huduma za muda mfupi ni lazima zilingane na huduma ulizoomba mara ya kwanza. Watu walipewa kipaumbele kwa huduma Bobesi za Afya ya Akili ni pamoja na:
 - Wanawake wajawazito,
 - Askari wa zamani na familia zao,
 - Wanawake walio na watoto,
 - Waangalizi wasiolipwa,
 - Familia,
 - Watoto walio na umri wa baada ya kuzaliwa hadi miaka mitano,

- Watu walio na virusi vya ukimwi/ukimwi
- Watu walio na kifua kikuu,
- Watu ambao wako katika hatari ya ugonjwa wa kichaa wa hatua ya kwanza, au
- Watu ambao wana ulemavu wa kiakili/ukuaji
- Huduma za matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya
 - Wanachama ambao ni watumiaji wa dawa za kijidunga, ikiwa ni pamoja na heroini, watafanyiwa tathmini ya mara moja na wanaweza kupokea matibabu ndani ya siku 14 au siku 120 baada ya kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri.
 - Wanachama ambao wanakabiliwa na ugonjwa wa matumizi ya dawa za afuni (opioid) watafanyiwa tathmini na kupata matibabu ndani ya saa 72.
 - Wanachama wanaohitaji huduma za Matibabu ya Kusaidiwa na Dawa (Medication Assisted Treatment au MAT kwa ufupi) watatathminiwa ndani ya saa 72. Trillium itashirikiana na watoa huduma ilioafikiana nao ili kuhakikisha kwamba huduma za muda mfupi zinatolewa. Hutahitajika kutekeleza utaratibu wa kutotumia vitu vya kusumisha kabla ya kupokea matibabu. Unaweza kupata miadi isiyopungua 2 ya ufuatilaji, pamoja na miadi moja kwa wiki baada ya tathmini. Tathmini hii itakuwa ni pamoja na:
 - o Tathmini kamili ya kimwili na nyingine ambazo hukagua mahitaji yako ya kibayolojia, kisaikolojia na kijamii, na kiroho.
 - o Mtoa huduma atakagua tathmini zilizokamilishwa ili kubaini dawa bora ya kutumia ili kuepuka hatari au madhara ambayo yanaweza kutokea bila kujua zaidi kukuhusu.

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kufikia huduma hizi, tembelea tovuti yetu katika: <https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services.html>

- Matibabu, mpango wa matibabu au mpito wa mpango wa matibabu unaojumuisha afya ya kimwili, kiakili na mdomo.
- Chanzo kinachoendelea cha matibabu ya msingi, mtu anayeshughulikia kuratibu huduma za afya zinazolipiwa na bima.

- Kwa wanawake wajawazito: Walio na dharura ya meno wataonwa au kutibiwa ndani ya saa 24, wiki 1 kwa matibabu ya haraka ya meno, wastani wa wiki nne kwa matibabu ya mara kwa mara ya meno, na wiki nne kwa uchunguzi wa awali wa meno.

Uchunguzi wa Hatari ya Afya ni Nini?

Uchunguzi wa Hatari kwa Afya ni hojaji ya haraka ya simu tunayotumia ili kupata uelewa bora wa maeneo katika maisha yako ambayo yanaweza kufaidika kutokana na usaidizi wa ziada. Uchunguzi huo huuliza maswali kuhusu afya yako na vitu ambavyo vinaweza kuathiri afya yako. Kwa mfano, tutauliza kuhusu unavyohisi. Tutauliza ikiwa ulitembelea idara ya dharura hivi karibuni. Pia tutauliza kuhusu hali yako ya maisha na ikiwa unaweza kuhitaji usaidizi katika shughuli zako za maisha ya kila siku. Timu yetu inaweza pia kkuunganisha na usaidizi wa kijamii na kuratibu matibabu.

JE, MAELEZO HAYO HUKUSAIDIA VIPI?

Pindi baada ya Uchunguzi wa Hatari ya Afya kukamilika, timu zetu za usaidizi zinaweza kuwasiliana nawe ili kuungana nawe. Tutabainisha jinsi tunavyoweza kukusaidia katika uzoefu wako wa huduma za afya. Timu yetu ya Usimamizi wa Matibabu inaweza kuzungumza nawe kuhusu:

- kufikia matibabu
- matatizo ya kudumu ya afya
- kuzuia kuanguka na usalama
- malengo yako ya afya ya kimwili, kiakili au meno Unapozungumza na timu yetu, tunaweza kufanya tathmini zaidi. Hili litatusaidia kubainisha malengo ya mpango wako wa matibabu.

JE, UNAPASWA KUKAMILISHA UCHUNGIZI WA HATARI YA AFYA MARA NGAPI?

Tutawasiliana nawe punde tu baada ya kuwa mwanachama wa Trillium ili kukukaribisha kwenye mpango na kutoa Uchunguzi wa Hatari ya Afya. Uchunguzi wa Hatari za Afya utasaidia kkuunganisha na mafao ya afya tunayotoa ili kuhakikisha mabadiliko rahisi hadi kwenye mpango wetu. Pia tunatoa uchunguzi kila baada ya miezi 12 au mara tu mahitaji yako ya kiafya yanapobadilika. Hili litaendelea mradi wewe ni mwanachama wa Trillium CCO.

NANI ANAWEZA KUPATA MAELEZO YANGU YA UCHUNGIZI WA HATARI YA AFYA?

Maelezo kutoka kwa Uchunguzi wa Hatari ya Afya ni sehemu ya rekodi yako ya afya. Tutashiriki matokeo ya

uchunguzi wako wakati ambapo yanaweza kusaidia kutoa mabadiliko rahisi ya matibabu. Pia tutashiriki matokeo hayo wakati yanaweza kusaidia mtoa(watoa) huduma wako kupanga matibabu yako. Tutaomba ruhusa yako wakati ambapo kanuni za jimbo au taifa zinahitaji tufanye hivyo. Pia tunaweza kuwasiliana nawe kwa barua ya posta ikiwa hatuwezi kukupata kwa simu. Ikiwa unahitaji kitu kabla tuwasiliane nawe, tafadhalii piga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472.

Je, Huduma za Kuratibu Uangalizi Makini wa Wagonjwa (Intensive Care Coordination Services au ICC kwa ufupi) ni Zipi?

Huduma za ICC hutoa usaidizi na rasilimali kwa wanachama walio na mahitaji maalum ya huduma za afya. Watu waliopewa kipaumbele kwa ICC wanaweza kuwa ni pamoja na wanachama ambaao:

1. Ni wazee, watu walio na matatizo ya kusikia, viziwi, vipofu, au wenyewe ulemavu mwingine;
2. Wana mahitaji changamano au ya juu ya huduma za afya, au matatizo mengi au ya kudumu ya afya;
3. Wana Ugonjwa Mbaya na wa Kudumu wa Akili, au
4. Wanapokea huduma za matibabu na usaidizi wa muda mrefu (LTSS) zinazofadhiliwa na Medicaid;
5. Ni watoto wenyewe umri wa miaka 0-5 ambaao:
 - a) Wanaonyesha dalili za mapema za matatizo ya kijamii/kihisia au kitabia au;
 - b) Wamebainishwa kuwa na Ugonjwa Mbaya wa Kihisia (Serious Emotional Disorder au SED kwa ufupi);
6. Wanapokea matibabu yanayosaidiwa na dawa kwa Ugonjwa Unaotokana na Matumizi ya Dawa za Kulevyta (Substance Use Disorder au SUD kwa ufupi);
7. Ni wanawake ambaao wamebainishwa kuwa na ujauzito wenyewe hatari kubwa;
8. Ni watoto walio na ugonjwa wa kujihini unaotokana na watu kutumia dawa za kulevyta karibu nao wakati wa ujauzito;
9. Ni watoto wanaopokea ulinzi wa Idara ya Ustawi wa Watoto (Child Welfare);
10. Ni watumiaji wa dawa za kujidunga za kulevyta;

11. Wana ugonjwa unaotokana na matumizi ya dawa za kulevyta na wanahitaji usimamizi wa kuacha kutumia dawa;
12. Wana virusi vya ukimwi/ukimwi au wana kifua kikuu;
13. Ni askari wa zamani na familia zao; na
14. Wako katika hatari ya ugonjwa wa kichaa wa hatua ya kwanza, na
15. watu ambaao ni sehemu ya walio na ulemavu wa Kiakili na ukuaji (Intellectual and developmental disability au IDD kwa ufupi).

Ili kupata huduma za ICC au kuomba uchunguzi wa hatari ya afya kwa huduma za ICC, unaweza kutafuta huduma kupewa rufaa. Pia, mtu aliye katika timu yako ya afya anaweza kutoa rufaa kwa niaba yako. Ili kutoa rufaa au kuomba uchunguzi wa hatari ya afya, unaweza kupigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kwa 1-877-600-5472 na uombe Huduma za ICC. Utapokea jibu ndani ya siku moja ya kazi.

Huenda kukawa na nyakati ambapo tutawasiliana nawe moja kwa moja ili kutoa huduma za ICC. Hili hufanyika tunapopata taarifa kuwa huenda mahitaji yako ya matibabu yanaongezeka. Hili hufanyika pia unapokuwa na utambuzi wa ugonjwa mpya ambaao ni sehemu ya watu waliopewa kipaumbele.

Iwe utaomba kupewa rufaa au tutawasiliana nawe ili kutoa Huduma za ICC, tutakuomba ukamilishe uchunguzi wa hatari wa ICC. Uchunguzi huo huangazia sehemu nyingi ili kubainisha unachowenza kuhitaji kutoka kwa kipengele cha afya ya kijamii, kimwili na akili.

Ikiwa unastahiki, utapewa huduma za ICC.

Ikiwa utachagua kupoakea Huduma za ICC, utapewa Mratibu wa Matibabu ya ICC. Mratibu wa Matibabu ya ICC atakuwa mtu wa kipekee wa kushughulikia mawasiliano kuhusu mahitaji yako ya matibabu. Utapewa jina lake na nambari yake ya simu. Anapatikana katika saa za kawaida za kazi, Jumatatu hadi Ijumaa.

Ikiwa hustahiki au hutaki Huduma za ICC, unaweza kupewa mipango mingine ya ndani ya Kuratibu Matibabu au Usimamizi wa Matibabu, kulingana na matokeo ya uchunguzi wako.

Mratibu wa Matibabu wa ICC atashirikiana nawe, mwakilishi wako (ikiwa una mwakilishi) na timu yako ya matibabu ili kuratibu matibabu yako.

Mpango wa ICC utabuniwa ndani ya siku 10 baada yako kuchagua kujiunga kwenye Huduma za ICC. Utajumuisha mahitaji yako yaliyobainishwa, vizuizi, shughuli na rasilimali ili kusaidia kutimiza na kudumisha malengo yako ya kibinagsi, afya na usalama. Huu ni mpango wako na ni muhimu kwamba unabuniwa kikamilifu nawe na timu yako.

Kwa kategemea mahitaji na vizuizi vyako, mpango huo unaweza kuwa na wanachama wengi wa timu wanaowajibikia nyanja zao za ustadi. Nyanja hizi zinaweza kuwa ni pamoja na lakini bila kikomo kwa, mahitaji ya kimwili, mdomo, mwenendo, kijamii, ukuaji, elimu, kiroho, kitamaduni na kifedha. Mpango wa ICC husasishwa kwa maoni yako na timu yako angalau kila siku 90, au mapema, ikiwa inahitajika.

TUKO HAPA KUKUSAIDIA WAKATI WA MABADILIKO YA MATIBABU:

Trillium inafahamu kuwa kujiunga kwenye mpango mpya wa afya kunaweza kuwa na changamoto. Ikiwa unakuja kwa Trillium Community Health Plan kutoka kwa shirika lingine la matibabu yanayoratibiwa (CCO) au kutoka kwa kadi huru ya OHP, tunaweza kuwasiliana nawe ili kutoa usaidizi wa kupata mpito rahisi hadi kwa mafao yako mapya. Wakati wa mabadiliko kati ya mipango, bima yako kwa watoa huduma wako huendelea ifuatavyo:

Matibabu ya wanachama ambao hupokea mafao kamili ya Medicare na Medicaid (Full Benefit Dual Eligible au FBDE kwa ufupi) yatalipiwa kwa:

- Mto Huduma wa Msingi wa Matibabu kwa hadi siku tisini (90)
- Mto Huduma wa Afya ya Mdomo kwa hadi siku tisini (90)
- Mto Huduma wa Afya ya Akili kwa hadi siku tisini (90)

Matibabu ya wanachama wengine wote yatalipiwa kwa:

- Mto Huduma wa Msingi wa Matibabu kwa hadi siku thelathini (30)
- Mto Huduma wa Afya ya Mdomo kwa hadi siku thelathini (30)
- Mto Huduma wa Afya ya Akili kwa hadi siku sitini (60)

Kumbuka: Kipindi cha wakati kinaweza kubadilishwa ili kukidhi mpango unaoendelea wa matibabu au mfululizo ulioagizwa wa matibabu.

WANACHAMA WAGENI WANAOHITAJI HUDUMA MARA MOJA

Ikiwa wewe ni mwanachama mgeni wa Trillium au mgeni kwa Medicare na umesajiliwa kwenye Trillium, unaweza kuhitaji matibabu, dawa zilizoagizwa na daktari, au bidhaa na huduma nyingine muhimu. Ikiwa unahitaji lolote kati ya haya katika mwezi wako wa kwanza wa kusajiliwa na huwezi kukutana na PCP, Daktari wa Msingi wa Matibabu ya Meno (Primary Care Dentist au PDP kwa ufupi) au mto huduma mwingine, tunaweza kusaidia. Piga Simu kwa Nambari Isiyotozwa Ada ya Huduma kwa Wanachama: 1-877-600-5472 (TTY 711).

Tutakusaidia kupata huduma zozote muhimu (zinazohitajika) zinazohusiana na afya unazohitaji mara moja. Ikiwa wewe ni mgeni kwenye Trillium au Medicare, tutakusaidia na kukupatia taarifa.

Ni muhimu kwetu kwamba unapata mabadiliko rahisi. Wanachama wote wanaweza kupata huduma za kina za afya za mpito ikiwa ni pamoja na kukabidhiwa vyema kwa matibabu ya ufuutiliaji wakati wa kuingia au kutoka katika kituo cha uangalizi makini au mazingira ya matibabu ya muda mrefu.

Kwa wanachama walio na magonjwa ambayo hayajapona au ya kudumu, au ambaa wanahitaji Matibabu ya Muda Mrefu na Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu, Trillium itashirikiana na watoa huduma wako, ikiwa ni pamoja na Watoa Huduma wa Medicare, ili kuhakikisha kwamba mpito wa mpango wa matibabu umewekwa kwa wanachama:

- Wenye Mahitaji Maalum ya Huduma za Afya,
- Wanaopokea Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu,
- Ambao wanatoka katika Hospitali au Utunzaji wa Kituo Stadi cha Uuguzi,
- Ambao wanatoka kwa taasisi au vituo vya utunzaji wa wagonjwa wanaolazwa wa Afya ya Akili,
- Ambao wanapokea Huduma za Nyumbani au Jamii kwa matatizo ya Afya ya Akili, na
- Wanachama ambao hupokea mafao kamili ya Medicare na Medicaid (FBDE) ambao wamesajiliwa katika Mipango ya Washirika wa MA wa Mkandarasi au Mipango ya Wanachama Rudufu wa Mahitaji Maalum (DSN).

Hili litapunguza kurudufiwa kwa uchunguzi na shughuli za kupanga matibabu kwa uratibu ulioboreshwa.

TUTAHAKIKISHA KWAMBA UFIKIAJI WA MATIBABU UNAENDELEA KWA;

- Watoto Dhaifu Kiafya
- Watu walio katika mipango ya matibabu ya saratani ya matiti na mlango wa kizazi
- Watu wanaotumia usaidizi wa CareAssist kutokana na virusi ya ukimwi/ukimwi
- Watu walio katika mipango ya matibabu kwa:
 - Hatua ya mwisho ya ugonjwa wa figo
 - Matibabu ya kabla na baada ya kujifungua (kabla na baada ya ujauzito)
 - Huduma za kupandikiza sehemu za mwili
 - Huduma za tiba mionzi na tibakemikali (matibabu ya saratani)
- Mtu yeьте ambaye atakabiliwa na hatari kubwa za kiafya ikiwa hataendelea kupokea matibabu

Katika mabadiliko haya, unaweza kuendelea kuona mto huduma wako wa awali hata kama hayuko kwenye mtandao wetu.

Bidhaa ambazo unapokea kwa sasa, kama vile dawa zilizoagizwa na daktari au vifaa vya matibabu, zitaendelea kupatikana kwako wakati wa mpito na/au hadi utakapoweza kukutana na PCP, Daktari wa Meno, na/au Mto Huduma mpya wa Afya ya Akili ili kupata maagizo mapya au kusasisha mpango wako wa matibabu. Hakikisha tu kwamba unamwonyesha mto huduma wako kadi yako mpya ya bima au kumwambia kwamba una bima mpya.

Ikiwa utajaribu kuchukua dawa mpya au kupata huduma za awali na uambiwe kwamba huna bima, tafadhali tujulishe mara moja ili tuweze kusaidia!

Kwa baadhi ya wanachama, Trillium itapokea maelezo kutoka kwa shirika lako la awali la matibabu yanayoratibiwa (CCO) ili kusaidia katika ufikiaji wako endelevu kwa matibabu, huduma za afya za mdomo, na/au afya ya akili.

Baadhi ya wanachama wanastahiki kwa Medicare pamoja na Medicaid (OHP). Ikiwa wewe ni Msajiliwa mpya wa Medicare, kwa kutegemea kiwango chako cha mpango wa afya na bima ya Medicare, tunaweza kusaidia kuunganisha au kuwasiliana ili kukusaidia kupanga matibabu yako chini ya mpango wako mpya. Ikiwa utaendelea kuwa na Trillium kama bima ya pili, daima tunapatikana ili kusaidia kwa mahitaji yako ya vitu ambavyo havilipiwi na bima yako ya Medicare.

Usaidizi unapatikana ili kuhakikisha kwamba unaweza kupokea matibabu yanayoendelea na kufuata mipango ya matibabu iliyowekwa na mto huduma wako bila

kuchelewa kwokwote. Ikiwa unahisi unahitaji usaidizi kuhusu hili, tafadhali wasiliana na Mratibu wa Matibabu au Meneja wa Kesi wa Trillium kuititia 1-877-600-5472. Pia unaweza kusoma sera yetu hapa:

<https://www.trilliumohp.com/content/dam/centene/trillium/medicaid/pdfs/CCO%20Transitions%20of%20Care%20Policy%2010.29.2019%20FINAL.pdf>

JE, HUDUMA ZINAZOHUSIANA NA AFYA NI ZIP?

Huduma zinazohusiana na afya hutolewa kama kijalizo cha huduma za afya zinazolipiwa na bima. Kuna aina mbili za huduma zinazohusiana na afya:

- Huduma zinazoweza kubadilishwa kwa kutegemea hali husika, ambazo ni huduma za gharama nafuu zinazotolewa kwa mwanachama binafsi ili kujalizia mafao yanayotolewa na bima, na
- Mipango ya manufaa ya jamii, ambayo ni hatua za kuingilia kati kwa kiwango cha jamii zinazolenga kuboresha afya ya watu na ubora wa huduma za afya. Mipango hii inajumuisha wanachama, lakini sio lazima iwe kwa wanachama pekee.

Huduma Zinazoweza Kubadilishwa kwa Kutegemea Hali Husika ni bidhaa au huduma ambazo hazichakatwi kuititia kwa kutozwa kwa kawaida kwa bili za matibabu. Bidhaa au huduma hizi zinaweza kukusaidia kupata matokeo bora ya afya, ingawa sio za kimatibabu kiasili. Mifano ni pamoja na lakini bila kikomo kwa:

- makazi ya muda kwa mtu ili apone au kupata afueni baada ya kulazwa hospitalini wakati ambapo hana makazi yake mwenyewe
- sanduku la dawa la kielektroniki ili kusaidia kutumia dawa kwa wakati unaofaa
- ufikiaji wa bwawa la matibabu kwa kusonga kulikoimashwa kwa vifundo
- viyoyozi kwa wanachama wanaopata changamoto za kupumua wakati wa joto kali

Ili kufikia Huduma Zinazoweza Kubadilishwa kwa Kutegemea Hali Husika, unaweza kuwasiliana na daktari wako au mwanachama yeьте wa timu yako ya matibabu. Pia unaweza kupigia Trillium simu kwa 1-877-600-5472 na uombi kuzungumza na Meneja wa Matibabu. Mwanachama wa timu yako ya matibabu au Meneja wa Matibabu wa Trillium atajaza fomu. Ni muhimu kuhakikisha kwamba bidhaa au huduma hiyo itakusaidia kwa njia chanya kwa afya. Pia ni muhimu kuhakikisha kwamba bidhaa au huduma hiyo sio sehemu ya mafao mengine yanayopatikana kwako. Inaweza kuchukua hadi siku 10 ili kuchakata ombi hilo. Pindi baada ya ombi hilo kuchakatwa, tutaagiza huduma au bidhaa hiyo. Katika

hali nyingine, inaweza kuchukua muda zaidi ili kuwasilisha bidhaa hiyo. Ikiwa ombi la huduma inayohusiana na afya litakataliwa, Trillium itakuarifu. Una haki ya kuwasilisha nung'uniko.

Je, Wawakilishi wa Muunganisho wa Wanachama (Member Connection Representatives au MCRs kwa ufupi) ni kina nani?

MCRs ni Wafanyakazi wa Afya ya Jamii, walioihinishwa katika Jimbo la Oregon na ambao wameajiriwa na Trillium. MCRs hushughulika ili kuwaunganisha wanachama na huduma zinazohitajika. MCRs wanaweza kukusaidia kufikia mafao yako na kupanga miadi ya matibabu. Pia wanaweza kuratibu mahitaji ya kijamii kama makazi na chakula. Wanaweza kukuunganisha na rasilimali za jamii. MCRs hushirikiana kwa karibu na kituo chako cha msingi cha matibabu na timu ya ndani ya Trillium. Wanaweza kukutana nawe kuptitia kwa simu, video au nyumbani kwako. Wanaweza kusaidia kwa mambo kama jinsi ya kukumbuka kutumia dawa zako kwa wakati unaofaa. Pia wanaweza kusaidia katika kutuma maombi ya makazi au kupasha nyumba joto au kutafuta bidhaa zinazohitajika kuptitia kwa mifumo ya kijamii. MCRs wanaweza kutoa mafunzo ya afya kuhusu kisukari na pumu. MCRs wana uwezo mkubwa wa kutatua matatizo na wanajua jamii zao. Ikiwa ungependa kushirikiana na MCR, tafadhali piga simu kwa 1-877-600-5472 na uombe Mwakilishi wa Miunganisho ya Wanachama.

Je, Uratibu wa Matibabu na Usimamizi wa Kesi ni nini?

Trillium iko hapa ili kukusaidia kutimiza malengo yako ya afya. Kuptitia kwa mbinu ya kushirikiana, tunashughulika ili kuratibu matibabu kulingana na mahitaji yako maalum. Tunashirikiana nawe, watoa huduma wako na mtu yeyote ambaye unaweza kuteua, ili kubuni mwelekeo changamano wa kupata afya bora na kuzuia magonjwa. Tunatumia mbinu ya ushirikiano pamoja na rasilimali za jamii na timu yetu ya matibabu ili kuhakikisha kwamba mahitaji yako yanatimizwa. Mbinu hii hukusaidia kutumia mfumo wa huduma za afya ili kupata afya njema ya mtu kamilifu, ikiwa ni pamoja na afya ya kimwili, matibabu ya afya ya akili na afya ya mdomo/meno, pamoja na kusaidia katika kuondoa vizuizi.

Wakati ambapo uko katika Mpango wa Uratibu wa Matibabu, Usimamizi wa Kesi, au Huduma za Uratibu

wa Uangalizi Makini, utakuwa na meneja wa matibabu aliyetengwa kukuhudumia. Meneja wako wa matibabu atashirikiana na wewe ili kubuni mpango wa matibabu. Mpango huu utakuwa na shughuli za kusaidia kutimiza mahitaji yako. Wewe na timu yako ya matibabu mtashiriki katika kuunda malengo ya kuboresha afya yako na ustawi. Timu hii ya matibabu inaundwa na daktari wako, tabibu, mwanafamilia, au mtu mwingine yeyote ambaye ni muhimu kwa matokeo ya afya yako. Mpango ya matibabu itasasishwa angalau kwa kila mwaka, lakini itasasishwa mapema zaidi, inavyohitajika, utakapotimiza malengo yako au mahitaji yako yatakapobadilika. Unaweza kuomba mratibu wa matibabu wakati wowote. Pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuptitia 1-877-600-5472 (TTY: 711). Omba kuzungumza na mratibu wa matibabu. Pia tunaweza kuwasiliana na wewe ikiwa mto huduma wako au mhudumu mwingine wa kijamii atatuomba kusaidia.

Elimu ya afya inayozingatia utamaduni

Tunaheshimu hadhi na utofauti wa wanachama wetu na jamii wanamoishi. Tunataka kuhudumia mahitaji ya watu wa tamaduni zote, lugha, rangi, asili za kikabila, uwezo, dini, jinsia, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, na mahitaji mengine maalum ya wanachama wetu. Tunataka kila mtu ajihisi amekaribishwa na anahudumiwa vyema katika mpango wetu.

Tuna mipango na shughuli nyingi za kuishi maisha yenyе afya njema unazoweza kutumia. Mipango yetu ya elimu ya afya ni pamoja na kujitunza, kuzuia magonjwa, na kudhibiti magonjwa mwenyewe. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma hizi, tafadhali pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuptitia 1-877-600-5472, TTY 711.

Baraza ya Ushauri wa Jamii

Trillium ina Baraza mbili za Ushauri wa Jamii (Community Advisory Councils au CACs kwa ufupi). CAC moja inawakilisha kaunti ya Lane katika eneo la Kusini. CAC moja inawakilisha kaunti za Clackamas, Multnomah, na Washington katika eneo la Kaskazini. Zaidi ya nusu ya wanachama wa CAC ni wanachama wa Trillium OHP au wazazi/babu au nyanya wa wanachama wa Trillium OHP. Wanachama wengine wanatoka kwa mawakala na mashirika ambayo hushirikiana na wanachama wa Trillium. CAC hushiriki uzoefu wao na kutoa maoni ili kusaidia kuboresha mipango na huduma za Trillium.

Pia huishauri Trillium kuhusu mipango ya kijamii. CAC ni mshirika mkuu katika Tathmini ya Mahitaji ya Afya ya Jamii na Mpango wa Uboreshaji wa Afya ya Jamii. Ikiwa unataka kuijunga kwenye CAC, kujifunza zaidi, au kushiriki wazo, tafadhali tupigie simu au utembelee

<https://www.trilliumohp.com/about-us/public-notices/community-advisory-council-public-notices.html>

Barua ya bima ya OHP

Mamlaka ya Afya ya Oregon itakutumia barua ya bima ambayo inataja nambari ya simu ya kitengo cha Huduma kwa Wanachama wa OHP, kifurushi chako cha mafao, na mpango wa matibabu yanayodhibitiwa. Barua hii inatoa maelezo kwa kila mtu katika nyumba yako aliye na Kitambulisho cha Afya cha Oregon.

Kadi za kitambulisho

Kadi ya kitambulisho cha Afya cha Oregon

DHS itakutumia Kitambulisho cha Afya cha Oregon ambacho kitakuwa na jina lako, nambari ya mteja na tarehe ya kutolewa. Kila mtu aliye na OHP atapokea kadi yake mwenyewe ya Kitambulisho cha Afya cha Oregon. Tafadhali peleka kadi hii kwa kila miadi.

Kadi ya kitambulisho cha Trillium

Trillium pia itakutumia kadi ya kitambulisho inayosema kwamba wewe ni mwanachama wa Trillium OHP. Itakuwa na jina lako, jina la PCP wako, Shirika lako la Matibabu ya Meno, na nambari za simu za kitengo cha Huduma kwa Wanachama, uidhinishaji wa awali, dharura, usafirishaji (usafiri), na maswali kuhusu famasia. Tafadhali peleka kadi hii pamoja na kadi ya Kitambulisho cha Afya cha Oregon kwa kila miadi.

Itakuwaje ikiwa nina Medicare na OHP?

Ikiwa una OHP na unastahiki kupata Medicare, Trillium itaratibu huduma zako. Huhitaji kulipa sehemu ya ghamama ya matibabu na kiasi cha pesa kabla ya bima yako kuanza kulipia huduma unazopokea isipokuwa iwe:

- Ulipokea huduma kutoka kwa watoa huduma wasio wa Trillium na huduma hizo hazikuwa za dharura;

- Ulipokea huduma ambazo zilikuwa hazilipiwi na mafao yako ya Medicare na OHP wakati ambapo ulipokea huduma.

Kwa kategemea kiwango chako cha mpango wa afya na bima ya Medicare, tunaweza kusaidia kuunganisha au kuwasiliana ili kukusaidia kuratibu matibabu kati ya kampuni zako tofauti za bima. Wakati ambapo una Medicare, inakuwa ya kwanza kwa matumizi ya bima. Trillium itashirikiana nawe, mto huduma wako na kampuni yako ya bima ya Medicare ili kuhakikisha kwamba unapata matibabu yote unayohitaji na unayotaka.

Ikiwa wewe ni Mwanachama Rudufu wa Mahitaji Maalum katika bima ya Trillium Medicare na Trillium Medicaid, daima utakuwa na meneja wa kesi aliyetengwa kukuhudumia ambaye atawasiliana nawe mara kwa mara ili kusaidia mahitaji yako kamili ya kibinadamu. Usaizidi unapatikana ili kuhakikisha kwamba unaweza kupata matibabu bora na kufuata mipango ya matibabu iliyowekwa na mto huduma wako bila kuchelewa kwokwote. Ikiwa unahisi unahitaji usaizidi kuhusu hili, tafadhali wasiliana na Mratibu wa Matibabu au Meneja wa Kesi wa Trillium kuitia 1-877-600-5472.

Je, nitapata mkalimani vipi?

Unaweza kupata mkalimani wa lugha inayozungumzwa au ya ishara katika miadi yako ikiwa unamhitaji. Unapopiga simu kwa miadi, iambie ofisi ya mto huduma wako kwamba unahitaji mkalimani na kwa lugha ipi. Huduma hii haikugharimu chochote. Ikiwa unahitaji mkalimani wa lugha fulani au wa ishara kwa ziara za huduma za afya, unaweza:

1. Kupigia Trillium simu.
2. Kupiga simu kwa ofisi ya daktari wako na kuwaomba kuratibu mkalimani kwa ziara yako Maelezo kuhusu Wakalimani wa Huduma za Afya yanapatikana katika: www.Oregon.gov/oha/oei.

JE, HAKI NA MAJUKUMU YANGU YA MWANACHAMA NI YAPI?

Taarifa hii inafafanua haki na majukumu yako kama mwanachama wa Trillium Community Health Plan (Trillium).

Kama mwanachama wa Trillium Community Health Plan, una haki fulani. Pia kuna mambo fulani unayowajibikia. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu haki na majukumu yaliyoorodheshwa hapa, wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472. Omba kuzungumza na Usimamizi wa Matibabu.

Una haki ya kutumia haki zako za mwanachama bila hatua yoyote inayoweza kukuathiri vibaya au ubaguzi. Ikiwa unahisi kwamba haki zako zimehujumiwa, unaweza kuwasilisha nung'unico. Pia unaweza kuwasiliana na Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson) kuititia kwa Mamlaka ya Afya ya Oregon kuititia 1-877-642-0450 au TTY 711.

Pia unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Kutobaguliwa wa Trillium:

Geno Allen, Non-Discrimination Coordinator,

gilbert.e.allen@trilliumchp.com.

555 International Way, Building B,
Springfield, OR 97477

Simu: 541-650-3618, Nambari isiyotozwa ada
877-600-5472 au TTY 711.

Kuna nyakati ambapo watu walio na umri wa chini ya miaka 18 (watoto) wanaweza kutaka au kuhitaji kupata huduma za afya wakiwa peke yao. Ili kujifunza zaidi, soma "Haki za Watoto: Ufikiaji na Idhini ya Huduma za Afya." Mwongozo huu unakwambia aina za huduma ambazo watoto wanaweza kupata wakiwa peke yao. Pia unakwambia jinsi maelezo ya huduma za afya ya watoto yanaweza kushirikiwa. Unaweza kusoma mwongozo huu mtandaoni katika <https://www.oregon.gov/oha/PH/HEALTHYPEOPLEFAMILIES/YOUTH/Documents/minor-rights.pdf>

Haki za Mwanachama

KAMA MWANACHAMA WA TRILLIUM UNA HAKI YA:

- Kushughulikiwa kwa hadhi, heshima na kuzingatiwa kwa faragha yako.
- Unaweza kubainisha ikiwa mtoe huduma anakubali wanachama wapya kwa kutazama sajili ya mtoe huduma.
- Kushughulikiwa na watoa huduma kwa njia sawa kama watu wengine wanaotafuta huduma za afya.
- Kuchagua watoa huduma wako na kubadilisha uteuzi huo.
- Kutafuta huduma za afya ya akili au kupanga uzazi moja kwa moja bila kupewa rufaa na PCP wako au mtoe huduma mwingine.
- Kuandamana na rafiki, mwanafamilia au msaidizi hadi kwa miadi yako.
- Kuhuishwa katika kubuni mpango wako wa matibabu.
- Kupata taarifa kuhusu ugonjwa wako, huduma zinazolipiwa na zisizolipiwa na bima, ili uweze kufanya maamuzi mema kuhusu matibabu yako. Kupata taarifa hizi katika lugha na muundo unaokufaa zaidi.
- Kukubali au kukataa matibabu na kuambiwa kinachoweza kufanya kulingana na uamuzi wako. Huduma ilioagizwa na mahakama haiwezi kukataliwa.
- Kupata nyenzo zilizoandikwa zinazokuambia haki zako, majukumu, mafao, jinsi ya kupata huduma, na unachopaswa kufanya katika dharura.
- Kupata nyenzo zilizoelezwa kwa njia kwamba unaweza kuzielewa na katika lugha yako.
- Kujifunza kuhusu mashirika ya matibabu yanayoratibiwa (CCOs) na mfumo wa huduma za Afya.

- Kupata huduma ambazo huzingatia mahitaji yako ya kitamaduni na lugha na zilizo karibu na unakoishi. Ikiwa yanapatikana, unaweza kupata huduma katika mazingira ya kisasa.
 - Kupata uratibu wa matibabu, matibabu ya kijamii, na usaidizi katika mabadiliko ya matibabu kwa njia inayolingana na lugha na utamaduni wako ili kupunguza hitaji la kutembelea hospitali au kituo cha uuguzi.
 - Kupata huduma ambazo zinahitajika ili kutambua tatizo lako la afya.
 - Kupata matibabu na huduma zinazolenga mtu binafsi ambazo hukupatia uwezo wa kuchagua, uhuru na hadhi. Matibabu haya yatalingana na mahitaji yako ya afya na kutimiza viwango vinavyokubalika kwa ujumla vya utendaji.
 - Kuwa na uhusiano thabit na timu ya matibabu inayowajibikia usimamizi wa jumla wa matibabu yako.
 - Kupata usaidizi wa kutumia mfumo wa huduma za afya na kupata rasilimali unazohitaji. Hii inaweza kuwa ni pamoja na:
 1. Wakalimani waliodhinishwa au waliohitimu wa huduma za afya
 2. Wafanyakazi wa kawaida wa jamii wa afya waliodhinishwa
 3. Wafanyakazi wa afya ya jamii
 4. Wataalamu wenza wa ustawi
 5. Wataalamu wa usaidizi wa wenza
 6. Doula
 7. Mwelekezi wa kibinafsi wa afya
 - Kupata huduma zinazolipiwa na bima za kuzuia magonjwa.
 - Kupata huduma za haraka na dharura kwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki bila idhini ya mapema.
 - Kupata rufaa kwa watoa huduma bobesi kwa huduma zinazoratibiwa zinazolipiwa na bima ambazo zinahitajika kulingana na afya yako.
 - Kuwa na rekodi ya matibabu ambayo hufuatilia matatizo yako ya afya, huduma unazopata na rufaa.
 - Kuweza kufikia rekodi zako za matibabu. Kunaweza kuwa na nyakati ambapo sheria huweka kizuizi kwa ufikiaji wako.
 - Kuhamisha rekodi yako matibabu kwa mtoe huduma mwengine.
- Rekodi yako ya matibabu kurekebishwa au kubadilishwa ili iwe sahihi zaidi.
 - Kutoa taarifa kuhusu matamanio yako ya matibabu. Inaweza kuwa na matamanio yako ya kukubali au kukataa matibabu, upasuaji, au matibabu ya afya ya akili. Pia inaweza kutoa maelekezo na mamlaka ya kisheria ya usimamizi wa matibabu yako.
 - Kupata taarifa iliyoandikwa ya kukataliwa au kubadilishwa kwa mafao kabla hilo kutekelezwa. Unaweza kukosa kupokea taarifa ikiwa kanuni za taifa na jimbo haziagizi kutolewa kwa taarifa.
 - Kuwasilisha nung'uniko au ukate rufaa.
 - Kuomba kusikizwa kwa kesi ikiwa hukubaliani na uamuzi uliofanywa na Trillium Community Health Plan au OHP.
 - Kupata huduma za wakalimani waliodhinishwa au waliohitimu wa huduma za afya, ikiwa ni pamoja na ufasiri wa lugha ya ishara.
 - Kupata taarifa ya kukatishwa kwa miadi kwa wakati unaofaa.
 - Kutozuiliwa au kutengwa na watu ili kukufanya ufanye jambo ambalo hutaki kufanya, kunakotumiwa kama njia ya kukuadhibu, au kufanya iwe rahisi zaidi kukutibu.
 - Kushughulikiwa kwa haki na kuwasilisha lalamiko la kubaguliwa ikiwa unafikiri umeshughulikiwa bila haki kwa sababu ya:
 1. Umri
 2. Rangi
 3. Ulemavu
 4. Utambulisho wa Kijinsia
 5. Hali ya ndoa
 6. Umbari
 7. Dini
 8. Jinsia
 9. Mwelekeo wa Kingono
 - Kushiriki maelezo na Trillium Community Health Plan kielektroniki. Unaweza kuchagua kufanya hili au kutofanya.

Majukumu ya Mwanachama

KAMA MWANACHAMA WA TRILLIUM UNA HAKI YA:

- Kuchagua au kusaidia kuchagua mtoe huduma wa msingi wa matibabu na daktari wa msingi wa meno.

- Kuwashughulikia wafanyakazi wa Trillium Community Health Plan, watoa huduma na wafanyakazi wa kliniki kwa heshima.
 - Kufika katika miadi kwa wakati unaofaa.
 - Kupiga simu mapema ikiwa unatarajia kuchelewa au kukatisha miadi yako ikiwa huwezi kuhudhuria.
 - Kupata uchunguzi wako wa afya wa kila mwaka, ziara za afya, na matibabu ya kuzuia magonjwa ili kukufanya uendelee kuwa na afya njema.
 - Kutumia PCP wako kwa mahitaji yako ya huduma za afya ila tu ikiwa ni dharura.
 - Kutumia matibabu ya haraka na dharura kwa njia inayofaa.
 - Kumjulisha PCP wako ndani ya saa 72 ikiwa ulitumia huduma za dharura.
 - Kupata rufaa kutoka kwa PCP wako ili kuona mtaalamu ikiwa unaihitaji. Kuna hali fulani ambapo huhitaji rufaa.
 - Kuwa mkweli kwa watoa huduma wako ili waweze kukupatia matibabu bora zaidi.
 - Kumsaidia mtoe huduma wako kupata rekodi yako ya afya. Unawenza kuhitajika kutia saini kwenye idhini ya kutoa rekodi zako.
 - Kuuliza maswali ikiwa kuna jambo lisiloelewka kwa uwazi.
 - Kutumia maelezo kutoka kwa Trillium Community Health Plan, watoa huduma wako au timu yako ya matibabu ili kufanya maamuzi bora zaidi kuhusu afya yako.
 - Kumsaidia mtoe huduma wako kubuni mpango wako wa matibabu.
 - Kufuata maagizo ya watoa huduma wako au kuomba chaguo lingine.
 - Kumjulisha mtoe huduma wako kwamba una OHP na kuleta kadi zako za kitambulisho cha matibabu katika miadi.
 - Kuambia Oregon Health Plan (OHP):
 1. Ikiwa utabadilisha nambari yako ya simu.
 2. Ikiwa utabadilisha anwani yako.
 3. Ikiwa utapata ujauzito na utakapojifungua.
 - 4. Ikiwa mwanafamilia yeoyote atahamia nyumbani kwako au kutoka kwenye nyumba yako.
 - 5. Ikiwa una bima nyingine yoyote.
 - Ukilipia huduma zisizolipiwa na bima.
 - Kuisaidia Trillium Community Health Plan kurejeshewa pesa ilizotumia kutoka kwa pesa zozote utakazopokea kutokana na jeraha. Kiasi hicho kinalingana tu na kile tulicholipa katika mafao yanayohusiana na jeraha hilo.
 - Kuwasilisha matatizo, malalamiko au manung'uniko kwa Trillium Community Health Plan.
- Ikiwa utapokea huduma za usafiri usio wa dharura hadi kwa miadi yako, pia una haki na majukumu yafuatayo ya abiria:

Haki za Abiria

KAMA MWANACHAMA WA OHP UNA HAKI YA:

Kufikia usafiri salama, kwa wakati unaofaa, na unaostahili kwa saa 24 kwa siku, siku 365 kwa mwaka;

- Kusafiri kwa gari linalofaa zaidi kulingana na mahitaji yako, eneo la miadi yako na gharama;
- Kutotozwa kwa huduma za usafiri wa matibabu usio wa dharura na Trillium;
- Kutotozwa kwa huduma za usafiri wa matibabu usio wa dharura na watoa huduma wa usafiri wenye mikataba midogo;
- Kufikia sera na taratibu za Trillium za usafiri wa matibabu usio wa dharura;
- Kupokea taarifa zilizoandikwa za kukataliwa kwa ombi lako la usafiri ndani ya saa 72 baada ya kutolewa kwa uamuzi huo. Wafanyakazi wawili hukagua ombi kabla likataliwe ili kuhakikisha kwamba hilo linafaa;
- Nakala ya kukataliwa itatolewa kwa mtoe huduma uliyeratibiwa kuona. Hili litafanyika ikiwa mtoe huduma huyo ni sehemu ya mtandao wa Trillium na aliomba usafiri kwa niaba yako;
- Kupokea taarifa wakati ambapo usafiri wako umeratibiwa;
- Kutofikishwa katika eneo la miadi zaidi ya dakika 15 kabla ya miadi yako au kabla ya jengo kufunguliwa isipokuwa iwe hilo liliombwa nawe au, anapohusika, mlezi, mzazi au mwakilishi wako; na

- Kutochukuliwa zaidi ya dakika 15 baada ya jengo la miadi yako kufungwa au zaidi ya saa moja baada ya kuomba kuchukuliwa isipokuwa ukiomba hilo lifanyike au miadi yako itakamilika baada ya kufungwa au kama ilivyoombwa na mwanachama, ama anapohusika, mlezi, mzazi, au mwakilishi wa Mwanachama;
- Kusafiri kwa gari:
 - Ambalo ni safi na lisilo na mabaki yanayoathiri uwezo wako wa kusafiri vyema;
 - Lililo na mikanda inayofaa ya usalama, ikiwa gari hilo linastahili kuwa na mikanda ya usalama kisheria;
 - Lililo na kifaa cha huduma ya kwanza, kizimamoto, vifaa vya kuakisi nuru vya barabarani au vya kuonya, tochi, vifaa vya kuvuta tairi katika hali mbaya ya hewa, na glavu zinazoweza kutupwa baada ya matumizi;
 - Lililo na vifaa vyote vinavyohitajika ili kufunga kitu cha magurudumu au machela inapohitajika;
 - Lililo katika hali nzuri ya utendakazi, ikiwa ni pamoja na vioo vya kando na vya nyuma, honi, na ishara zinazofanya kazi za kubadilisha uelekeo, taa za mbele, taa za nyuma, na waipa za kioo cha mbele cha gari.
- Kuendeshwa na dereva anayetimiza masharti ya Jimbo ya kuwa dereva wa usafiri wa matibabu usio wa dharura:
 - Kuwa na usajili halali na leseni ya dereva ya jimbo
 - Ukaguzi wa usuli ulioidhinishwa ikiwa ni pamoja na historia ya uhalifu, historia ya dereva, hali ya mhalifu wa ngono na upimaji wa matumizi ya dawa za kulevyo
 - Kuwa na mafunzo yaliyorekodiwa ya kuendesha gari na kusaidia wanachama wenyenye ulemavu na mahitaji maalum.
- Kuomba marekebisho yanayofaa ya gari au safari yako inapofaa kulingana na sheria za jimbo na taifa. Hii ni pamoja na wakati ambapo:
 - Dereva anatishia kukuumiza wewe au wengine walio kwenye gari,
 - Anaendesha gari au kufanya mambo ambayo yanakuweka wewe au wengine walio kwenye gari katika hatari ya madhara, au
 - Anakutishia wewe au wengine walio kwenye gari moja kwa moja.
- Kuomba marekebisho ya gari au safari yako ili kutimiza Sheria ya Wamarekani wenyenye Ulemavu na sheria na kanuni nyingine zinazohusika;
- Kuweza kutoa lalamiko au kukata rufaa kwa kukataliwa kwa ombi lako la usafiri kwa Trillium na kupokea jibu;
- Kutoa mapendekezo kuhusu sera ya Trillium ya haki na majukumu ya abiria;
- Kuwasilisha nung'uniko na kuomba rufaa au kuangaziwa upya kwa ombi lako;
- Kurejeshewa pesa kwa gharama ulizolipia kwa huduma zinazolipiwa na bima.

Majukumu ya Abiria

KAMA MWANACHAMA WA OHP, UNAKUBALI:

- Kukamilisha tathmini ya mahitaji yako ya usafiri unapoomba usafiri;
- Kuarifu MTM hali zako za afya zinapobadilika, zinazoweza kuathiri gari ambalo limeratibiwa kwa usafiri wako;
- Kuratibu usafiri mapema uwezavyo. Wewe au mwakilishi wako anaweza kuratibu:
 - Miadi za wakati mmoja - mapema kwa hadi siku 90;
 - Miadi zinazorudiwa - kuweka safari zote zinazohitajika kwa wakati mmoja, mapema kwa hadi siku 90;
 - Miadi za siku sawa - pigi simu mapema uwezavyo
- Kutovuta sigara, kutumia erosoli au, kuvuta vepu kwenye gari wakati wowote;
- Kuchukua vitu vyote ulivyoleta unapoondoka kwenye gari;
- Kufuata sheria za usafiri za eneo lako, jimbo na taifa kuhusu viwango vya usalama wa abiria;
- Kusafiri kwelekea na kutoka kwa miadi ukiwa na mhudumu ikiwa una umri wa miaka 12 au michache au ikiwa unahitaji usaidizi unaposafiri.

- Mhudumu anaweza kuwa mzazi, mlezi, mzazi wa kambo, nyanya au babu, au mwakilishi wako. Ikiwa sio mmoja wa watu hawa, basi mzazi au mlezi wako ni lazima atoe idhini iliyoandikwa ili mtu yeyote mzima aliye na umri wa miaka 18 au zaidi awe mhudumu wako. Wahudumu hawawezi kuwa na umri wa chini ya miaka 18;
- Kutoa au kuweka viti vyovvye vya usalama vinavyohitajika na sheria ya Oregon kwa usafiri salama;
- Kutoa vifaa vingine vyovvye vya matibabu vinavyohitajika kwa usafiri wako kama vile, oksijeni, viti vya magurudumu au fimbo;
- Kushirikiana na Trillium na MTM kuhusu marekebisho yoyote yanayohitajika ya gari au safari yako ikiwa:
 - Utatishia kumuumiza dereva au wengine walio kwenye gari,
- Utamtishia dereva au wengine walio kwenye gari moja kwa moja,
- Utafanya mambo au kuhusika katika hali ambazo zinaweka dereva au wengine walio kwenye gari katika hatari ya madhara, au
- Kufanya mambo ambayo kwa mujibu wa uamuzi wa Trillium yanafanya madaktari au vituo vya eneo husika kukataa kutoa huduma zaidi bila mabadiliko,
- Kutofika kwa usafiri ulioratibiwa mara kwa mara, au
- Kukatisha usafiri katika siku ya usafiri mara kwa mara;
- Kutoa taarifa zote zilizombwa kwa maombi ya kurejeshewa pesa kwa gharama ulizolipa;
- Kurejesha kiasi chochote kinachozidi kiasi ulichostahili kupokea kwa gharama ulizolipa kama inavyotakikana na kanuni za jumbo;
- Kuwasilisha matatizo, malalamiko au manung'uniko kwa Trillium.

JINSI YA KUPATA MATIBABU UNAPOYAHITAJI

Je, nitapata daktari au mto huduma vipi?

Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium haijajumuishwa kwenye mwongozo huu. Nakala ilitumwa kwako kwa barua ya posta pamoja na mwongozo huu mara ya kwanza ulipojisajili. Ikiwa unataka nakala nyingine, tupigie simu. Ikiwa una intaneti, unaweza kutafuta mtoa huduma au kuchapisha sajili ya watoa huduma katika:

<https://findaprovider.trilliumhealthplan.com/location>

Baadhi ya watoa huduma wa Trillium hawakubali wagonjwa wapya. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kupata mto a huduma anayekubali wagonjwa wapya au mto a huduma anayezungumza lugha nyingine kando na Kiingereza, pigia Trillium simu. Kwa matibabu ya hospitalini ya mara kwa mara, ni sharti uchague hospitali iliyoordheshwa katika Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium:

Legacy Meridian Park Hospital

19300 SW 65th Ave., Tualatin, OR 97062

503-692-1212 watumiaji wa TTY hupiga simu kwa 711
<https://www.legacyhealth.org/locations/hospitals/legacy-meridian-park-medical-center.aspx>

Legacy Mt Hood Medical Center

24800 SE Stark St., Gresham, OR 97030
 503-674-1122 watumiaji wa TTY hupiga simu kwa 711
<https://www.legacyhealth.org/locations/hospitals/legacy-mount-hood-medical-center.aspx>

Legacy Emanuel Medical Center

2801 North Gantenbein Ave., Portland, OR 97227
 503-413-2200 watumiaji wa TTY hupiga simu kwa 711
<https://www.legacyhealth.org/doctors-and-locations/hospitals/legacy-emanuel-medical-center>

Legacy Good Samaritan Hospital and Medical Center

1015 NW 22nd Ave., Portland, OR 97210
 (503) 413-7711 Watumiaji wa TTY Hupiga Simu kwa 711
<https://www.legacyhealth.org/doctors-and-locations/hospitals/legacy-good-samaritan-medical-center>

Oregon Health & Science University

3181 SW Sam Jackson Park Rd., Portland, OR 97239
 503-494-8311 watumiaji wa TTY hupiga simu kwa 711
<https://www.ohsu.edu/visit/ohsu-hospital-portland>

Adventist Health Portland

10123 SE Market St., Portland, OR 97216
 503-257-2500 watumiaji wa TTY hupiga simu kwa 711
www.adventisthealth.org/portland/

Je, Matibabu ya Msingi ni Yapi?

Matibabu ya msingi ni utunzaji wa jumla wa tiba na matibabu yanayotolewa na Mtoa Huduma wa Msingi wa Matibabu (PCP). Yanajumuisha:

- Huduma za afya za kuzuia magonjwa ambazo hutambua tatizo la afya mapema au kulizua kutokea. Kwa mfano, mamogramu (eksirei za matiti), uchunguzi wa saratani wa mlango wa kizazi, au chanjo (sindano za chanjo);
- Matibabu ya matatizo ya kudumu ya afya, kwa mfano: kisukari au pumu;
- Dawa zinazoagizwa na daktari;
- Rufaa kwa matibabu bobezi; na
- Kulazwa hospitalini ikiwa kunahitajika.

Je, Nitachagua Mtoa Huduma wa Msingi wa Matibabu Vipi?

Kumjua Mtoa Huduma wako wa Msingi wa Matibabu (PCP) ni muhimu. Wanachama wa Trillium ni lazima wawe na PCP. Unaweza kuchagua PCP ambaye ni mshirika wa Trillium, au tunaweza kukupatia mmoja. Ili kuchagua PCP, tupigie simu na utuambie PCP unayetaka kumuona. Ikiwa hutatupigia simu ndani ya siku 30 ili kutuambia PCP unayetaka kumuona, tutakupatia mmoja. Utahitaji kutumia PCP tutakayekupatia hadi utakapochagua mwenyewe. Pindi baada ya kupigia Trillium simu ili kubadilisha PCP wako, mabadiliko hayo yataanza kutumika katika siku ya kwanza ya mwezi unaofuata. Pia unaweza kupigia Trillium simu ili kubainisha ni PCP yupi uliyepewa. Ikiwa ungependa kuchagua PCP tofauti, wasiliana na Trillium.

Kliniki za PCP wa Trillium zimeorodheshwa kwenye Sajili yetu ya Watoa Huduma. Huenda baadhi ya watoa huduma waliorodheshwa hawachukui wagonjwa wapya. Tafadhali wasiliana na Trillium kwa orodha ya sasa ya watoa huduma ambao wanachukua wagonjwa wapya na lugha ambazo mtoa huduma anazungumza.

Trillium itakutumia kadi mpya ya kitambulisho ili kukujulisha kwamba PCP wako amebadilishwa. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuchagua PCP wako, pigia kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama simu kupitia: 1-877-600-5472, TTY: 711 Jumatatu hadi Ijumaa, saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni.

Wamarekani wa Kihidi na Wenyeji wa Alaska wanawenza kupokea matibabu yao katika kliniki ya Indian Health Services (IHS) au Native American Rehabilitation Association of the Northwest (NARA). Hili ni kweli iwe uko katika CCO au una OHP ya kulipa kwa kila huduma. Kliniki ni lazima itoze bili sawa na watoa huduma wa mtandao. Ikiwa mwanachama wa kabila ambaye amesajiliwa kwenye CCO hupokea huduma katika I/T/U, I/T/U inaweza kumtuma mwanachama huyo wa kabila kwa NARA ikiwa inahitajika. Akronimu ya I/T/U inabainisha aina tatu za Huduma za Afya za Wazaliwa wa Marekani:

- Huduma za Afya za India (Indian Health Services au IHS kwa ufupi)
- Watoa Huduma wa Afya wa Kikabila (Tribal Health Providers)
- Watoa Huduma wa Afya wa Wahindi wa Mjini (Urban Indian Health Providers)

Je, nitapanga miadi na PCP wangu vipi?

Mara baada ya kuchagua PCP wako au kupewa mmoja, panga miadi haraka uwezavyo. Hii itakusaidia wewe na PCP wako kujuana kabla ya kuwepo kwa tatizo la afya. Tafadhali mpigie PCP wako simu mapema kwa miadi ya mara kwa mara isiyo ya dharura. Piga simu mapema kwa wiki nyingi kabla ya wakati wa uchunguzi wa afya wa kila mwaka. Mpigie PCP wako simu unapohitaji kufanyiwa uchunguzi wa afya au wakati ambapo unaugua.

PCP WAKO:

- Anajua historia yako ya matibabu na anaelekeza matibabu yako yote.
- Huhifadhi rekodi zako za matibabu katika eneo moja ili kukupatia huduma bora zaidi.
- Huhakikisha kwamba unapata matibabu wakati wowote iwe mchana au usiku, kwa siku 7 kwa wiki.
- Hupanga matibabu yako bobezi au ya hospitali.

WAKATI WA MIADI PAMOJA NA PCP WAKO:

- Leta orodha ya maswali yoyote au matatizo ya afya uliyonayo ya kujadili na PCP wako.
- Leta orodha ya dawa zilizoagizwa na daktari na vitaminini unazotumia na umpatie PCP wako.

Je, nitabdalisha PCP wangu vipi?

Ikiwa unataka kubadilisha PCP wako, pigia kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama simu. Unaweza kubadilisha PCP wako ikiwa kuna mto huduma mwingine katika mtandao wetu anayekubali wagonjwa wapya. Unaweza kubadilisha PCP wako hadi mara mbili kwa mwaka.

Hapa ni baadhi ya vidokezo vya kukusaidia kuwa na uhusiano mwema na PCP wako:

1. Ratibu na kuhuduria miadi yako na PCP wako uliyepewa. PCP wako anawajibikia matibabu yote unayopokea, ikiwa ni pamoja na rufaa kwa wataalamu.
2. Ikiwa wewe ni mgonjwa mgeni katika Trillium, piga simu haraka na uratibu uchunguzi wa afya na PCP wako. Kwa kufanya hivyo, PCP wako atawenza kukujua na kusaidia kutimiza mahitaji yako maalum ya huduma za afya. Kumbuka – uchunguzi wa afya na tathmini za kudumisha afya ni matibabu ya mara kwa mara, na inaweza kuchukua wiki nyingi ili kupata miadi. Ikiwa unahitaji matibabu ya haraka, tafadhali ambia kliniki yako.
3. Baadhi ya kliniki zinahitaji kwamba uwasiliane na ofisi yako ya awali ya matibabu kabla ya ziara yako ya kwanza na uwaambie wahamishe rekodi zako za matibabu kwa PCP wako mpya. Rekodi hizi husaidia kutoa picha kamili ya historia yako ya afya na kusaidia PCP wako mpya kuendeleza huduma zako za matibabu.

JE, WAFANYAKAZI WA KAWAIDA WA JAMII WA AFYA NI KINA NANI?

Mfanyakazi wa kawaida wa jamii wa afya (traditional health worker au THW kwa ufupi) ni mtu ambaye hushirikiana na wanachama kuhusu uratibu wa matibabu, kuelekezwa kwa huduma na rasilimali katika mazingira ya jamii au kliniki: Wanasihamiwa na watoa huduma wa afya walio na leseni na huidhinishwa kuitia jimbo la Oregon. Trillium hulipia idadi kubwa ya huduma za wafanyakazi wa kawaida wa jamii wa afya. Trillium inaweza kukusaidia kufikia huduma zao.

Kuna aina tano tofauti za wafanyakazi wa kawaida wa jamii wa afya. Kila aina ya THW ina uwanja wake maalum wa ustadi.

1. Doula (wa Kujifungua) hutoa usaidizi wa kibinagsi, usio wa kimatibabu kwa wanawake na familia wakati wa ujauzito wa mwanamke, kujifungua, na baada ya kujifungua.
2. Mtaalamu wa Usaidizi wa Wenza (Peer Support Specialist au PSS kwa ufupi) hutoa usaidizi kwa mtumiaji wa sasa au wa zamani wa matibabu ya afya ya akili au uraibu.
3. Mtaalamu Mwenza wa Ustawi (Peer Wellness Specialist au PWS kwa ufupi) amepitia hali ya ugonjwa(magonjwa) wa(ya) akili pamoja na mafunzo ya kina. PWS hufanya kazi kama sehemu ya timu inayoendeshwa na mtu binagsi ya afya ya nyumbani. Huwa wanatumia afya ya akili na matibabu ya msingi ili kuwasaidia na kuwatetea watu ili kupata ustawi.
4. Mwelekezi wa Kibinagsi wa Afya (Personal Health Navigator au PHN kwa ufupi) hutoa maelezo, usaidizi, zana, na msaada ili kumruhusu mgonjwa kufanya maamuzi bora zaidi ya huduma za afya.
5. Mfanyakazi wa Jamii wa Afya (Community Health Worker au CHW kwa ufupi) ni mhudumu wa afya ya umma wa mstari wa mbele ambaye ni mwanachama anayeaminika wa jamii na/au ana ujuzi mpana kuhusu jamii inayohudumiwa.

Trillium ina Mratibu wa THW (mtu anayeshughulikia mawasiliano) ambaye anaweza kusaidia kukuunganisha na huduma zinazofaa za THW. Pia anaweza kusaidia kujibu maswali kuhusu huduma za THW. Ili kuwasiliana na Mratibu wa THW, tafadhali piga simu kuitia 1-877-600-5472. Pia unaweza kutuma ombi kuitia kwa barua pepe kwa: THW@TrilliumCHP.com. Unaweza kupata maelezo haya na masasisho yoyote ya maelezo ya mawasiliano ya THW kwenye tovuti yetu katika: <https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/wellness/traditional-health-workers.html>

Tunalipia maoni ya daktari wa pili

Hii haikugharimu chochote. Ikiwa unataka maoni ya daktari wa pili kuhusu machaguo yako ya matibabu, muombe PCP wako ukupatie rufaa ya maoni mengine, au tunaweza kukupangia rufaa. Ikiwa unataka kuona mto huduma asiyé katika mtandao wetu, Trillium itakupangia hili.

Nitafanya nini ikiwa siwezi kuhudhuria miadi yangu?

Kuhudhuria miadi yako ya matibabu, afya ya akili na meno ni mojawapo ya majukumu yako kama mwanachama wa Trillium. Iwapo ni lazima ukatishe miadi, tafadhali pigia mtoe huduma wako simu haraka uwezavyo, angalau siku 1 kabla ya miadi iliiyoratibiwa. Ulikosa kuhudhuria miadi na ukose kupiga simu kwa ofisi ya PCP wako, wanaweza kukuomba uchague PCP mpya. Watoa huduma hawawezi kukutoza ada kwa miadi ambayo haikuhudhuriwa.

Itakuwaje ikiwa ninahitaji matibabu mara moja?

Ikiwa wewe ni mgeni katika Trillium na unahitaji matibabu au dawa zilizoagizwa na daktari mara moja, tafadhali tupigie simu na uombe kuzungumza na Mratibu wa Matibabu. Tunaweza kusaidia kupata matibabu yanayohitajika na mahitaji mengine kama vile vifaa au dawa zako zilizoagizwa na daktari. Pia ni muhimu kwako kupanga miadi na PCP wako haraka uwezavyo ili kuwa na uhakika kwamba unapokea matibabu unayohitaji.

Itakuwaje ikiwa ninahitaji matibabu baada ya saa za kazi (jioni, wikendi, na likizo)?

PCP wako hushughulikia matibabu yako saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Hata kama ofisi ya PCP wako imefungwa, piga simu kwa nambari ya simu ya ofisi ya PCP wako. Utazungumza na mtu atakayewasiliana na PCP wako au kukupatia ushauri kuhusu cha kufanya. Wakati mwingine PCP wako anaweza kutopatikana. Watahakikisha kwamba mtoe huduma mwingine daima anapatikana ili kukusaidia.

Itakuwaje ikiwa ninahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine?

Unaweza kutafuta matibabu kwa mtaalamu wa afya ya kimwili au akili bila kupewa rufaa kwa matibabu yanayofaa ya magonjwa yako. Hii inamaanisha kwamba unaweza kuchagua mtoe huduma kwa matibabu yanayofaa bila kumuuliza PCP wako. Hata hivyo, sababu (tatizo la afya au ugonjwa uliotambuliwa) ya ziara hiyo ni sharti iwe ya huduma inayolipiwa na bima, na sharti iwe

katika mtoe huduma aliye kwenye mtandao wetu. Ikiwa unafikiri unahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine, zungumza na PCP wako kwanza. PCP wako anaweza kukusaidia kubainisha huduma za mtaalamu unazohitaji.

Itakuwaje ikiwa nina Mahitaji Maalum ya Huduma za Afya?

Ikiwa una mahitaji maalum ya huduma za afya, una ufikiasi wa moja kwa moja kwa wataalamu wa afya ya kimwili na akili kwa matibabu yanayofaa kwa matatizo yako ya afya. Hii inamaanisha kwamba unaweza kuchagua mtoe huduma kwa matibabu yanayofaa bila kumuuliza PCP wako. Hata hivyo, sababu (tatizo la afya au ugonjwa uliotambuliwa) ya ziara hiyo ni sharti iwe ya huduma inayolipiwa na bima, na katika hali nydingi ni sharti iwe kwa mtoe huduma aliye kwenye mtandao wetu.

Ikiwa unafikiri unahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine, zungumza na PCP wako kwanza. PCP wako anaweza kukusaidia kubainisha huduma za mtaalamu unazohitaji.

Pia, Waratibu na Mameneja wa Kesi wanapatikana ili kukusaidia kuhusu mahitaji yako maalum ya huduma za afya. Pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472. Omba kuzungumza na Mratibu wa Matibabu.

Itakuwaje ikiwa ninapokea Huduma na Usaидizi wa Muda Mrefu?

Ikiwa unapokea Huduma na Usaидizi wa Muda Mrefu (Long-Term Services and Supports au LTSS kwa ufupi), una ufikiasi wa moja kwa moja kwa wataalamu wa afya ya kimwili na akili kwa matibabu yanayofaa kwa matatizo yako ya afya. Hii inamaanisha kwamba unaweza kuchagua mtoe huduma bila kumuuliza PCP wako. Sababu (tatizo la afya au ugonjwa uliotambuliwa) ya ziara hiyo ni sharti iwe ya huduma inayolipiwa na bima. Katika hali nydingi ni sharti uone mtoe huduma aliye katika mtandao wetu. Ikiwa unafikiri unahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine, zungumza na PCP wako kwanza. PCP wako anaweza kukusaidia kubainisha huduma za mtaalamu unazohitaji.

Pia, bado unaweza kupokea Huduma za Uratibu wa Uangalizi Makini wa Wagonjwa (Intensive Care Coordination au ICC kwa ufupi) kutoka kwa Trillium kwa kupigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472. Omba kuzungumza na mratibu wa ICC au meneja wa kesi.

Hapa chini kuna orodha ya huduma unazoweza kupokea bila kupewa rufaa na PCP wako.

Ili kutafuta huduma hizi bila kupewa rufaa, ni sharti uende kwa mto huduma aliye katika mtandao wetu. Pigia mto huduma huyo simu ili kubainisha ikiwa yuko katika mtandao wetu. Kisha unaweza kupanga miadi yako mwenyewe.

- Matibabu Yanayosaidiwa na Dawa ya uraibu wa dawa za afyuni (Opioid); (siku 30 za kwanza za matibabu). Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.
- Huduma za Mfanyakazi wa Kawaida wa Jamii wa Afya. Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma au upige simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium.
- Matibabu ya dawa za kulevyta na pombe. Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.
- Wanachama wa kike wanaweza kufikia wataalamu wa afya ya wanawake moja kwa moja ndani ya mtandao wa watoa huduma kwa huduma zinazolipiwa na bima zinazohitajika ili kutoa uchunguzi wa afya wa mara kwa mara wa wanawake na huduma za kuzuia magonjwa za wanawake. Hizi ni pamoja na lakini bila kikomo kwa matibabu ya kabla ya kujifungua, uchunguzi wa matiti, mamogramu, na uchunguzi wa saratani wa mlango wa kizazi.
- Matibabu ya wakati wa ujauzito. Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.
- Uchunguzi wa dhuluma ya kingono. Pigia mto huduma wako simu.
- Huduma za kupanga uzazi. Unaweza kupata huduma hizi kutoka kwa mto huduma yeyote ambaye ameafikiana na Mamlaka ya Afya ya Oregon na aliye na leseni ya kutoa huduma hizi.
- Huduma za afya ya akili. Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.
- Usaидizi wa kuacha kuvuta sigara. Piga Simu kwa Kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama.
- Huduma za kusafisha figo. Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.

- Chanjo (sindano za chajo). Tumia kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find-a-Provider ili kuchagua mto huduma.
- Huduma za Uratibu wa Uangalizi Makini wa Wagonjwa (ICC)
- Ikiwa wanapokea huduma za ICC, LTSS, au wana mahitaji maalum ya huduma za afya, wanachama wanaweza kufikia mtaalamu na matibabu yanayofaa ya afya ya kimwili au akili moja kwa moja kwa matibabu ya tatizo la afya la mwanachama na mahitaji yaliyotambuliwa.

Itakuwaje ikiwa mto huduma sio wa mtandao?

Katika hali nyingi ni sharti utembelee mtaalamu au mto huduma wa Trillium. Ikiwa huduma hiyo inapatikana kwa watoa huduma wa Trillium, tutaomba uone mto huduma wa Trillium. Ikiwa huduma hiyo haipatikani kwa watoa huduma wa Trillium, Trillium inaweza kuidhinisha mto huduma asiye wa mtandao. Tunaidhinisha miadi inayofanyika nje ya jimbo wakati huduma hiyo haipatikani ndani ya Oregon tu. Huwezi kutafuta huduma kwa mto huduma asiye wa mtandao bila kupewa rufaa.

Je, nitapata idhini ya huduma vipi?

Kando na rufaa, baadhi ya huduma za matibabu pia huhitaji idhini ya Trillium kabla ya kuweza kupata huduma hiyo. Idhini hii ya huduma inaitwa uidhinishaji. Mto huduma anayekupatia huduma hiyo atapata idhini kutoka kwa Trillium na kukwambia wakati ambapo huduma itaidhinishwa. Ikiwa huna rufaa au uidhinishaji wa huduma, unaweza kunyimwa huduma hiyo au ulazimike kulipia huduma hiyo.

Mafao Mengine Yanayolipiwa na Bima ya OHP

Kuna baadhi ya huduma ambazo Trillium Community Health Plan hailipii, lakini ambazo OHP italipia. Ikiwa unahitaji usaizidi kuhusu huduma hizi, tafadhali piga simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472. Omba kuzungumza na mratibu wa matibabu. Ikiwa unahitaji usaizidi ili kufika kwa huduma hizi, tafadhali pigia MTM simu bila kutozwa ada kuititia 877-583-1552 (TTY: 711). Baadhi ya mifano ya huduma zinazolipiwa na OHP lakini zisizotolewa na Trillium ni:

HUDUMA ZA AFYA ZISIZOLIPIWA NA CCO	URATIBU WA MATIBABU UNAPATIKANA KUTOKA KWA CCO	USA FIRISHAJI UNAPATIKANA KUPITIA KWA CCO	MTU WA KUWASILIANA NAYE
<p>Kujitoa uhai kunakosaidiwa wa daktari chini ya Sheria ya Oregon ya Kufa kwa Heshima (Oregon Death with Dignity Act), ORS 127.800-127.897</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu wakazi wa Oregon walio na magonjwa yasiyotibika yanayotarajiwa kusabisha kifo karibuni kupata na kutumia dawa kutoka kwa madaktari wao, za kutumia wenyewe za kusaidia katika kukatisha maisha. 	Hapana	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620
<p>Huduma za makao ya wagonjwa kwa Wanachama wanaoishi katika Kituo Stadi cha Uuguzi;</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu wanachama kupata huduma za matibabu, usaidizi kutoka kwa wanafamilia, utetezi wa mgonjwa, ushauri wa kiroho, tathmini ya maumivu na matibabu, na kufikia dawa na vifaa vya matibabu vya kudumu ili kusaidia mpito wa mwisho wa maisha katika kituo stadi cha uuguzi. 	Hapana	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620
<p>Huduma za Afya Zinazotolewa Shulenii ambazo ni huduma zinazolipiwa na bima zinazotolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Elimu ya Walema (Individuals with Disabilities Education Act) ambazo gharama zake za matumizi hurejeshwa kwa mpango wa huduma za elimu;</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu ufikiaji wa wanafunzi wenye ulemavu. Shule ni lazima zitoe huduma za matibabu ambazo ni muhimu kwao kupata elimu kama sehemu ya mipango yao ya elimu maalum. 	Hapana	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620
<p>Uchunguzi unaoagizwa na wasimamizi unaoombwa au kuidhinishwa kwa mujibu wa OAR 410-130-0230;</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu wanachama kufanyiwa uchunguzi bobezu wanapokuwa katika viwango fulani vya matibabu. 	Hapana	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620
<p>Huduma zinazotolewa kwa wapokeaji wa Matibabu ya Dharura ambao ni Raia/Wageni wenye Ondoleo la Masharti au Mpango wa CAWEM Plus-CHIP wa Bima ya Kabla ya Kujifungua ya CAWEM;</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu Wanachama Wanaohitaji Matibabu ya Haraka Ambao Sio Raia/Wageni Wenye Ondoleo la Masharti kufikia huduma za dharura za matibabu na matibabu ya wakati wa ujauzito. 	Hapana	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620
<p>Kuharibu Mimba</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu wanachama kupata ufikiaji kwa huduma za kuharibu mimba. 	Ndiyo	Ndiyo	Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO kupitia (800)562-4620

HUDUMA ZA AFYA ZISIZOLIPIWA NA CCO	URATIBU WA MATIBABU UNAPATIKANA KUTOKA KWA CCO	USAFIRISHAJI UNAPATIKANA KUPITIA KWA CCO	MTU WA KUWASILIANA NAYE
<p>Huduma za kujifungua nje ya hospitali (Out-of-hospital birth au OOHB kwa ufupi) zikiwa ni pamoja na matibabu ya kabla na baada ya kujifungua ya wanawake wanaotimiza vigezo vilivybainishwa katika OAR 410-130-0240</p> <ul style="list-style-type: none"> -Huruhusu wanachama kufikia matibabu ya kabla na baada ya kujifungua katika mazingira yasiyo ya hospitali. 	Hapana	Ndiyo	Kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium – 877-600-5472
<p>Huduma na usaidizi wa muda mrefu ambao haujajumuishwa katika kurejeshewa gharama za matumizi na CCO kwa mujibu wa ORS 114.631;</p> <ul style="list-style-type: none"> - Huruhusu wanachama wanaopokea huduma za LTSS kupokea matibabu yanayoratibiwa kati ya CCO na Usaidizi na Huduma za Muda Mrefu 	Ndiyo	Ndiyo	Kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium – 877-600-5472
<p>Kuwasaidia wanachama kupata ufkiaji kwa huduma fulani za afya ya akili. Mifano ya huduma hizo ni pamoja na lakini bila kikomo kwa:</p> <ol style="list-style-type: none"> Baadhi ya dawa za magonjwa fulani ya akili; Dawa za kuponya magonjwa fulani ya akili; Matibabu ya muda mrefu ya magonjwa ya akili kwa wanachama wengine umri wa miaka 18 au zaidi; na Utunzaji binafsi katika makazi ya ulezi ya watu wazima kwa wanachama walio na umri wa miaka 18 au zaidi. <p>Kwa maelezo zaidi au orodha kamili kuhusu baadhi ya huduma hizi za afya ya akili, pigi simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama.</p>	Ndiyo	Ndiyo	Kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium – 877-600-5472
<p>Mpango wa Kuunganisha Familia (Family Connects Program) unaotoa ziara za bila malipo, zinazotokana na ushahidi za muuguzi kuwatembalea nyumbani kwa familia zote zilizo na watoto wachanga.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Mpango wa Family Connects wa Oregon huwasaidia wazazi kwa kuunganisha wauguzi, rasilimali za jamii, na familia. 	Ndiyo	Ndiyo	Kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium – 877-600-5472

Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma hizi, pigi kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja simu kupitia 1-800-273-0557. Ikiwa unahitaji usaidizi wa usafiri, tafadhali tazama sehemu ya “Ninaweza kupata usafiri hadi kwa miadi yangu?”

Je, teknolojia mpya hulipiwa na bima?

OHP huamua ikiwa teknolojia mpya au matumizi mapya ya teknolojia ya sasa yanajumuishwa kwenye kifurushi chako cha mafao. Ikiwa una maswali kuhusu ikiwa huduma inalipiwa na bima, tafadhali pigi simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama.

Bahashishi za daktari

Huwa tunalipa bonasi au tuzo kwa watoa huduma wetu kwa kukufanya uendelees kuwa na afya njema. Hatuwalipi au kuwatuza watoa huduma wetu kwa kupunguza huduma au rufaa. Kufanya uamuzi kuhusu maombi yako ya huduma kunategemea tu kufaa kwa matibabu na huduma na kuwepo kwa malipo ya bima. Una haki ya kuomba na kupokea maelezo ya ziada kuhusu bahashishi za daktari, na muundo na uendeshaji shughuli wa Trillium. Kwa maelezo ya ziada kuhusu bahashishi za daktari, wasiliana na Trillium kupitia 1-877-600-5472 (TTY 711).

Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?

Ikiwa unahitaji usaizidi wa kufika kwa miadi yako, tafadhali pigia MTM simu bila kutozwa ada kuitia 877-583-1552. Tunaweza kusaidia ikiwa huna njia ya kufika kwa daktari, daktari wa meno au mshauri wako. Watu wanaotumia OHP hupata usaizidi wa kulipia usafiri hadi kwa ziara za huduma za afya. MTM pia inaweza kukulipa kwa gharama za kuenda kwa miadi, ikiwa ni pamoa na gesi, vyakula na chumba cha kupanga kwa muda. Utahitaji kupata idhini kabla ya kuenda kwa miadi yako ya huduma za afya. Ili kupata idhini, piga simu kwa 877-583-1552. Jumapili - Jumamosi saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni, au wakati wowote kwa usafiri wa haraka au usafiri baada ya kuondoka hospitalini. Tafadhali pigia 911 simu kwa usafiri wa dharura. Usafiri wa bila malipo, au usafiri wa matibabu usio wa dharura, hutolewa na:

MTM (Usimamizi wa Usafiri wa Matibabu au Medical Transportation Management kwa Kiingereza)

Nambari Isiyotozwa Ada: 877-583-1552 (TTY: 711)

Ikiwa unahitaji kuratibu usafiri kuitia kwa MTM, piga simu mapema uwezavyo. Kumbuka, ikiwa utakatisha au kubadilisha miadi yako, pigia MTM simu mara moja ili kukatisha au kubadilisha usafiri wako. Unaweza kupata maelezo zaidi katika Mwongozo wa Usafiri wa Matibabu kwenye tovuti yetu katika

<https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/transportation.html>

Nitapataje mkalimani katika miadi?

Unaweza kupata mkalimani wa lugha inayozungumzwa au ya ishara katika miadi yako ikiwa unamhitaji. Unapopiga simu kwa miadi, iambie ofisi ya mtoe huduma wako kwamba unahitaji mkalimani na kwa lugha ipi. Hakuna gharama kwako.

Ikiwa unahitaji mkalimani wa lugha fulani au wa ishara kwa ziara za huduma za afya, unaweza:

1. Kupigia Trillium simu.
2. Kupiga simu kwa ofisi ya daktari wako na kuwaomba kuratibu mkalimani kwa ziara yako. Maelezo kuhusu Wakalimani wa Huduma za Afya yanaweza kupatikana katika www.Oregon.gov/oha/oei.

MAFAO NA HUDUMA ZINAZOLIPIWA NA BIMA

OHP hulipia nini?

OHP inaweza kutoa miwani, vifaa vya kusikia, vifaa vya matibabu, matibabu ya nyumbani na usafirishaji hadi kwa miadi ya huduma za afya. OHP hulipii kila huduma. Orodha ya magonjwa na matatizo haya ya afya inaitwa Orodha ya Huduma za Afya Zilizopewa Kipaumbele. Unaweza kusoma hii mtandaoni katika: <https://www.oregon.gov/oha/hsd/ohp/pages/prioritized-list.aspx>.

Magonjwa na matatizo mengine ya afya yanaweza kulipiwa na OHP katika hali fulani. Kwa mfano, mgonjwa anaweza kuwa na tatizo moja la afya linalolipiwa na bima na tatizo lingine la afya ambalo halilipiwi na bima. Tatizo la afya lisilolipiwa na bima linaweza kulipiwa ikiwa linaweza kusaidia kupata afueni kwa tatizo la kwanza. Kwa muhtasari kamili wa mafao, tafadhali tazama "Muhtasari wa Orodha ya Kukagua Mafao."

Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Vifaa vya Teknolojia

Huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia ni huduma za afya zinazotumia mawasiliano ya kielektroniki. Hii inaweza kuwa barua pepe salama. Pia inaweza kuwa akaunti ya mtandaoni ya mwanachama au mikutano ya mtandaoni ya sauti/video. Wanachama wa Trillium wanaweza kuwa na ziara za sauti, video au ziara pepe (ikiwa zinatolewa na mtoe huduma). Trillium itashirikiana na watoa huduma ili kuhakikisha ufikiaji unaofaa wa huduma. Tutatathmini uwezo wa mwanachama wetu wa kutumia mbinu mahususi zilizoidhinishwa za uwasilishaji wa huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia. Ili kuwa na miadi ya huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia, utahitaji kutumia kompyuta. Pia unaweza kutumia kipakatalishi, simu kibao au simu ya

mkononi. Wakati mwininge unaweza kuhitaji simu janja. Muulize mto huduma wako kuhusu huduma zao za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia. Unaweza kufikia huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia katika vituo vyote vya afya vya jamii. Katika mwaka wa 2022, Trillium itahakikisha kwamba kipengele chetu cha kutafuta mto huduma cha Find a Provider na Sajili ya Watoa Huduma inaonyesha ni watoa huduma wapi walio na huduma za kufikia huduma za afya kwa vifaa vya teknolojia. Pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kupitia 1-877-600-5472 (TTY: 711) ikiwa unahitaji usaidizi.

Ikiwa una maswali kuhusu huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia, tafadhali piga simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama. Pia unaweza kumuomba Meneja wako wa Kesi usaidizi.

Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Vifaa vya Teknolojia Zinazolipiwa na Bima

Huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia hulipiwa na bima kwa ziara za afya ya kimwili, akili na mdomo. Unaweza kutaka miadi ya huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia ili kupata dawa za mara kwa mara. Pia unaweza kuuliza maswali katika miadi ya huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia. Unaweza kutumia huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia kwa ziara za matibabu yanayoendelea ya afya ya akili. Wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama ili kupata watoa huduma wanaotoa huduma za afya kwa vifaa vya teknolojia.

Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Vifaa vya Teknolojia za Teladoc

Trillium pia inatoa huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia kutoka kwa Teladoc Health, Inc. Teledoc hutoa huduma za afya kwa vifaa vya teknolojia kwa ziara za afya ya kimwili, akili na meno. Huduma za Teladoc hazihitaji rufaa. Tafadhali pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za Teledoc au utembelee

<https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/telehealth.html>

Uteuzi wa Mgonjwa na Maafikiano

Huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia ni njia moja unayoweza kuona mto huduma wako. Baadhi ya watoa huduma wanaweza kuhitaji kukuona ana kwa ana. Kwa mfano, daktari wako wa moyo anaweza kuhitaji kukuona ana kwa ana. Mto huduma wako hawezikukuwekea kikomo kwa ziara za huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vye teknolojia tu. Trillium hushirikiana na watoa huduma wa mtandao wetu ili kutoa huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia ambazo hukusaidia kupata matibabu yanayofaa. Huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia zitakuwa zinatafaa kwa utamaduni. Njia ambazo Trillium inaweza kutoa huduma za afya kwa vifaa vya teknolojia katika lugha unayopendelea, breli, maandishi makubwa, sauti au njia yoyote ambayo inakufaa zaidi. Tazama sehemu ya "Usaidizi wa Lugha."

Utendaji wa Faragha wa Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Vifaa vya Teknolojia

Mto huduma wa Trillium wa huduma za afya zinazotolewa kwa vifaa vya teknolojia ni Teladoc Health, Inc. Sheria huhitaji Teladoc Health, Inc. ihifadhi maelezo yako binafsi ya afya kwa faragha. Huwa wanalinda maelezo yako kama tu mto huduma wako anavyofanya unapomtembelea ana kwa ana. Teladoc Health, Inc. ni lazima ikuambie kuhusu majukumu yake ya kisheria na utendaji wa faragha.

Itakuwaje ikiwa kuna mabadiliko ambayo yanaathiri uwezo wako wa kufikia matibabu au huduma?

Trillium hutoa taarifa ilioandikwa kwa wanachama walioathiriwa angalau siku 30 kabla ya mabadiliko yoyote. Mabadiliko hayo yanaweza kuwa kwa mto huduma, mpango au huduma inayolipiwa na bima. Tunaweza kufanya mabadiliko haraka ziasi kwa masuala makuu ya usalama. Kisha tutatumtaa taarifa kwa wanachama walioathiriwa baadaye. Ikiwa kuna mabadiliko katika mto huduma wako na mto huduma huyo akose kutoa taarifa ya kutosha ya mabadiliko ndani ya siku 30, tutakuarifu kuhusu mabadiliko hayo ndani ya siku 15.

Miongozo ya Utendaji

Miongozo ya Utendaji hutoa mwelekeo wa kuboresha afya yako. Manufaa na madhara ya machaguo mengi ya matibabu hujumuishwa. Trillium ina Miongozo ya Utendaji ya mada nyingi. Ikiwa unataka kupata mwongozo wa utendaji wa mada, tafadhalii piga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama. Miongozo ya Utendaji pia inapatikana katika tovuti ya Trillium chini ya Rasilimali za Watoa Huduma.

Huduma za Kuzuia Magonjwa

Kuzuia matatizo ya kiafya kabla yafanyike ni muhimu. OHP hulipia huduma za kuzuia magonjwa ili kukusaidia uendelee kuwa na afya njema. Huduma hizi hazihitaji uidhinishaji. Huduma za kuzuia magonjwa ni pamoja na uchunguzi wa afya wa mara kwa mara na vipimo vya kubainisha tatizo. PCP wako atapendekeza ratiba ya uchunguzi wa afya wa mara kwa mara na huduma nyingine

HUDUMA NYINGINE ZA KUZUIA MAGONJWA NI PAMOJA NA:

- Uchunguzi wa mapema na wa mara kwa mara, wa kutambua magonjwa na tiba (EPSDT);
- Chanjo kwa watoto na watu wazima (sio kwa madhumuni ya usafiri wa nje au ajira);
- Uchunguzi wa mara kwa mara wa mwili;
- Vipimo vya maabara;
- Zana za kuacha kuvuta sigara;
- Utunzaji wa kabla na baada ya kujifungua na watoto wachanga;
- Uchunguzi wa afya wa wanawake na uchunguzi wa saratani katika mlango wa kizazi
- Mamogramu (eksirei za matiti) za wanawake;
- Uchunguzi wa tezi kibofu kwa wanaume;
- Uchunguzi wa saratani; na
- Matibabu ya floraidi.

Je, nitapataje usaidizi ili kuacha kutumia tumbaku?

Jambo moja muhimu zaidi unaloweza kufanya ili kuboresha afya yako na afya ya familia yako ni kuacha kutumia tumbaku. Trillium hulipia dawa na ushauri wa simu na kocha aliyefunzwa ili kukusaidia kuacha kutumia tumbaku. Ikiwa unatumia tumbaku, piga simu kwa **Quit for Life** bila kutozwa ada kupitia **1-866-784-8454**.

EPSDT ni Nini?

Uchunguzi wa mapema na wa mara kwa mara, wa kutambua magonjwa na tiba (EPSDT) ni mafao ya huduma za afya ya wanachama walio na chini ya umri wa miaka 21. EPSDT inajumuisha huduma kamili za uchunguzi, uchunguzi wa kutambua magonjwa na matibabu. Uchunguzi huu unaweza kusaidia kupata matatizo ya afya ya kimwili, afya ya akili au afya ya ukuaji yanayohitaji uchunguzi zaidi wa kutambua ugonjwa na/au matibabu. EPSDT inajumuisha uchunguzi wowote wa kutambua ugonjwa na matibabu yanayohitajika ili kurekebisha au kuboresha hali ya afya ya kimwili na ya akili.

EPSDT pia inajumuisha huduma zinazohitajika ili kumsaidia mtoto aliye na kuchelewa kwa ukuaji. Huduma hizi zinaweza kusaidia kufanya matatizo ya afya yasiwe mabaya zaidi. Huduma hizi pia zinaweza kusaidia kupunguza kasi ya athari za tatizo la afya la mtoto. EPSDT huruhusu watoto na vijana kufikia huduma za afya mapema na mara kwa mara. Uchunguzi wa EPSDT wakati mwingine huitwa uchunguzi wa maendeleo ya mtoto.

EPSDT Hujumuisha Nini?

Uchunguzi wa maendeleo ya mtoto, au uchunguzi wa EPSDT, unajumuisha:

- Afya kamili na historia ya maendeleo
 - Uchunguzi kamili wa mwili
 - Elimu ya afya na ushauri kwa kutegemea umri na historia ya afya
 - Vipimo vya uwezo wa kuona
 - Vipimo vya uwezo wa kusikia
 - Vipimo vya maabara
 - Uchunguzi wa uwepo wa risasi kwenye damu
 - Ukaguaji wa matatizo ya kula au kulala
 - Hali ya lishe
 - Uchunguzi wa afya ya mdomo na huduma za afya ya mdomo na PCP aliyehitimu wa ABC Dental (ABCD)
 - Chanjo
 - Uchunguzi wa afya ya akili
 - Uchunguzi wa ugonjwa unaotokana na matumizi ya dawa za kulevyta
 - Huduma za madaktari kama zinavyohitajika kwa mwanachama kwa matatizo ya afya au magonjwa makali, ya misimu au ya kudumu
- Tatizo la afya linapotambuliwa na mtoa huduma wa matibabu wa mtoto, mtoa(watoa) huduma wa mtoto:
- Atamтиbu mtoto huyo ikiwa huduma hiyo iko ndani ya huduma ambazo mtoa huduma huyo hutoa; au

- Atampatia mtoto huyo rufaa kwa mtaalamu kwa matibabu. Hii inaweza kuwa ni pamoja na vipimo zaidi au uchunguzi bobezi, kama vile:
 - Tathmini ya maendeleo,
 - Afya changamano ya akili,
 - Tathmini ya ugonjwa unaotokana na matumizi ya dawa za kuleyya, au
 - Ushauri wa lishe.

Huduma za EPSDT hazijumuishi Mpango wa Msaada wa Lishe ya Ziada (Supplemental Nutrition Assistance Program au SNAP kwa ufupi) au mipango mingine ya huduma za jamii. Kwa maelezo na usaizidi wa kupewa rufaa kwa matibabu na huduma zisizolipiwa na bima chini ya EPSDT, tafadhalii wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia kwa Nambari Isiyotozwa Ada: 1-877-600-5472 (TTY 711).

Watoa huduma wanaota matibabu hutoa taarifa kuhusu matokeo ya huduma zao kwa mto (watoa) huduma wa uchunguzi wa EPSDT aliyetoa (walio) rufaa na historia ya kina ya afya na maendeleo, ikiwa ni pamoja na tathmini za maendeleo ya afya ya mwili na akili itadumishwa.

Nitafikiaje huduma za EPSDT?

Mpango wa EPDST unatolewa bila gharama kwa wanachama walio na hadi umri wa miaka 21. Mwanachama au familia inayostahiki inaweza kupata usafirishaji bila malipo. Mwanachama au familia inayostahiki pia inaweza kupata usaizidi wa kuratibu bila malipo. Ili kuwasiliana na **mpango wa EPSDT**, pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia **1-877-600-5472 (TTY 711)**. Oomba kuzungumza na Mratibu wa Matibabu.

Wanachama walio na umri wa hadi miaka 21 wana ufikiaji kwa mpango wa EPSDT bila malipo. Mwanachama au familia inayostahiki inaweza kupata usafirishaji bila malipo. Mwanachama au familia inayostahiki pia inaweza kupata usaizidi wa kuratibu bila malipo. Ili kuwasiliana na mpango wa EPSDT, pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472 (TTY 711). Oomba kuzungumza na Mratibu wa Matibabu.

Kwa maelezo zaidi kuhusu EPDST, tazama: Makala ya Ukweli Kuhusu Medicaid: https://downloads.aap.org/AAP/PDF/CHIP%20Fact%20Sheets/federaladvocacy_medicaidfactsheet_all_states.pdf Ratiba ya Muda ya AAP: https://downloads.aap.org/AAP/PDF/periodicity_schedule.pdf

Trillium inawahitaji watoa huduma wa msingi wa matibabu (PCP) wanaota huduma za EPSDT kuwa na mkataba ulioandikwa nawe au mwakilishi wako aliyeidhinishwa. Wahusika wote wawili ni lazima watie saini mkataba ulioandikwa. Mkataba huo ulioandikwa huonyesha majukumu yako chini ya EPSDT. Mkataba huu husema kwamba mto huduma huyo atakuwa chanzo chako cha mara kwa mara cha huduma za EPSDT kwa kipindi cha wakati kilichotajwa. Trillium itakusaidia kupata mto huduma anayefaa wa rufaa. Trillium pia itakusaidia kupanga miadi. Kitengo cha Kuratibu Matibabu cha Trillium kinaweza kusaidia kwa mahitaji na maswali yanayohusiana na EPSDT. Unapaswa kuanza kupokea matibabu ya EPSDT ndani ya miezi 6 baada ya ombi lako la huduma za uchunguzi.

Muhtasari wa Orodha ya Kukagua Mafao

Idhini ya awali inahitajika kwa baadhi ya huduma, taratibu za matibabu na vifaa vya matibabu. Kwa kawaida mtoe huduma wako huwasilisha ombi la idhini ya awali kwa ajili yako. Chati hii ina orodha ya huduma, taratibu za matibabu na vifaa vya matibabu. Inakwambia ikiwa idhini ya awali inahitajika au la. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma zinazohitaji idhini ya awali, tafadhalii piga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuitia Nambari Isiyotozwa Ada: 1-877-600-5472 (TTY 711).

MAFAO		GHARAMA YAKO	MASHARTI YA IDHINI YA AWALI	VIKOMO VYA MATIBABU YANAPOPOKEGA NA MTOA HUDUMA WA TRILLIUM
ZIARA ZA DAKTARI	Mtoe huduma wa msingi wa matibabu	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Mtaalamu	\$0	Haihitajiki kwa watoa huduma wa afya wa meno, afya ya wanawake au afya ya akili. Inaweza kuhitajika kwa huduma zingine baada ya ziara mbili.	Inavyopendekezwa au kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
HUDUMA ZA KUZUIA MAGONJWA	Ziara za kuchunguza maendeleo ya watoto wachanga, watoto wakubwa na vijana	\$0	Haihitajiki	Kama ilivyopendekezwa
	Uchunguzi wa mara kwa mara wa mwili	\$0	Haihitajiki	Kama ilivyopendekezwa
	Ziara za uchunguzi wa afya ya jumla wa wanawake	\$0	Haihitajiki	Kama ilivyopendekezwa
	Mamogramu (eksirei za matiti) za wanawake	\$0	Haihitajiki	Kama ilivyopendekezwa
	Uchunguzi wa tezi kibofu kwa wanaume	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Kupanga Uzazi	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Uchunguzi wa magonjwa ya zinaa (STDs)	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Kupimwa na ushauri kwa virusi vya ukimwi na ukimwi	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
DAWA ZINAZOAGIZWA NA DAKTARI	Dawa nyingi japo sio zote zinapatikana unapokuwa na agizo la mtoe huduma. Orodha kamili inaweza kupatikana katika orodha yetu ya dawa zinazopendelewa ya Oregon Health Plan.	Hakuna gharama kwa dawa zinazolipiwa na bima. Dawa za afya ya akili hudhibitiwa na jimbo. Kiasi cha sehemu ya malipo unachopaswa kulipa hutofautiana kwa dawa hizo.	Baadhi ya dawa zinaweza kuhitaji idhini pamoja na agizo la daktari.	Ikiwa dawa inayohitaji idhini itakataliwa, haitalipiwa na bima.

MAFAO		GHARAMA YAKO	MASHARTI YA IDHINI YA AWALI	VIKOMO VYA MATIBABU YANAPOPOKEWA NA MTOA HUDUMA WA TRILLIUM
MAABARA NA EKSIREI	Kutolewa damu ili ipimwe	\$0	Rufaa inahitajika	Hakuna kikomo
	Eksirei	\$0	Rufaa inahitajika	Hakuna kikomo
	Picha za viungo vya ndani za CT	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Hakuna kikomo
	Picha za viungo vya ndani za MRI	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Hakuna kikomo
CHANJO/ SINDANO ZA CHANJO	Chanjo	\$0 kwa chanjo zinazopendekezwa	Haihitajiki	Kama Ilivyopendekewa
MATIBABU YA UJAUZITO	Ziara za kabla ya kujifungua kwa mto huduma wako	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Matibabu ya baada ya kujifungua (matibabu unayopokea baada ya mtoto wako kuzaliwa)	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo
	Huduma za uchunguzi wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona	\$0	Haihitajiki	Unapatikana kwa wanawake wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache
	Usaidizi wa kunyonyesha, ikiwa ni pamoja na pampu za matiti	\$0	Haihitajiki	Wasiliana na Trillium kwa maelezo zaidi
UCHUNGU WA UZAZI NA KUJIFUNGUA	Mpango wetu wa huduma za kabla ya kujifungua unaweza kuwasaidia wanachama wajawazito kijiandaa kwa mtoto	\$0	Haihitajiki	Tafadhalii ijulishe Trillium na Mamlaka ya Afya ya Oregon unapokuwa mjamzito au mimba yako ikiharibika. Utahitaji kutuma ombi la OHP kwa ajili ya mtoto wako. Kujifungua ukiwa nyumbani hakulipiwi na Trillium lakini hulipiwa na OHA. Tafadhalii wasiliana na kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja kwa machaguo ya kujifungua ukiwa nyumbani
KULAZWA HOSPITALINI	Dharura	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo wakati ambapo hilo linahitajika kimatibabu
	Upasuaji uliopangwa ikiwa ni pamoja na huduma za hospitali ambapo mgongwa hulazwa na kurejea nyumbani baada ya kutibiwa	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Hakuna kikomo wakati ambapo hilo linahitajika kimatibabu

MAFAO		GHARAMA YAKO	MASHARTI YA IDHINI YA AWALI	VIKOMO VYA MATIBABU YANAPOPOKEWA NA MTOA HUDUMA WA TRILLIUM
	Huduma za kusaidia kurejea kwa hali ya kawaida ya maisha	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Hakuna kikomo wakati ambapo hilo linahitajika kimatibabu
	Huduma za Kulazwa Hospitalini	\$0	Haihitajiki kwa huduma za haraka au za dharura	Hakuna kikomo wakati ambapo hilo linahitajika kimatibabu
	Huduma za kusaidia kurejea kwa hali ya kawaida ya maisha ukiwa umelazwa hospitalini	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP, Pigia Trillium Simu kwa maelezo
	Huduma za Hospitalini za Kurejea Nyumbani Baada ya Kutibiwa	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP, Pigia Trillium Simu kwa maelezo
ZIARA ZA DHARURA, MATIBABU YA HARAKA AU HUDUMA NYINGINE ZA DHARURA ZINAZOHITAJIKA	Ziara za chumba cha dharura na matibabu ya haraka	\$0	Haihitajiki	Hakuna kikomo wakati ambapo hilo linahitajika kimatibabu
	Usafiri wa dharura wa matibabu	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Huduma za Matibabu ya Haraka	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP, Pigia Trillium Simu kwa maelezo
TIBA	Tiba ya mwili (Physical therapy au PT kwa ufupi)	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Tiba ya kuhusishwa kwa shughuli za kila siku (Occupational therapy au OT kwa ufupi)	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Tiba ya kuzungumza (Speech therapy au ST kwa ufupi)	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
UWEZO WA KUONA	Uchunguzi wa macho	\$0	Rufaa inahitajika	Unapatikana kwa wanawake wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache

MAFAO		GHARAMA YAKO	MASHARTI YA IDHINI YA AWALI	VIKOMO VYA MATIBABU YANAPOPOKEWA NA MTOA HUDUMA WA TRILLIUM
	Miwani	\$0	Rufaa inahitajika	Unapatikana kwa wanawake wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache
	Uchunguzi wa macho wa matibabu	\$0	Rufaa inahitajika	Idadi ya ziara inafuata idhini ya mpango
HUDUMA MAALUM	Vifaa na bidhaa za matibabu	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Vifaa vya kusikia na uchunguzi	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Afya ya nyumbani	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Vituo stadi vya uuguzi	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Huduma za matibabu ya kupunguza ukali au uzito wa maumivu	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Mtaalamu wa kurekebisha maungo	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Mtaalamu wa tiba vitobo	\$0	Uidhinishaji unatakiwa	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Wafanyakazi wa Kawaida wa Jamii wa Afya - Doula - Mtaalamu wa Usaidizi wa Wenza* - Mtaalamu Mwenza wa Ustawi* - Mwelekezi wa Kibinafsi wa Afya - Mfanyakazi wa Afya ya Jamii *Afya ya Akili	\$0	Wasiliana na Mtaalamu wa Usaidizi wa Wenza (Afya ya Akili) wa Trillium ukiwa na shirika au mtu anayeweza kusaidia kwa mahitaji yako mahususi.	Hakuna kikomo

MAFAO		GHARAMA YAKO	MASHARTI YA IDHINI YA AWALI	VIKOMO VYA MATIBABU YANAPOPOKEWA NA MTOA HUDUMA WA TRILLIUM
	Huduma za Usafirishaji Usio wa Dharura wa Matibabu (NEMT)	\$0	Haihitajiki	Wasiliana na Trillium kwa maelezo zaidi
	Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Vifaa vya Teknolojia	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Huduma za mkalimani	\$0	Haihitajiki	Wasiliana na Trillium kwa maelezo zaidi
AFYA YA AKILI	Matibabu Yanayosaidiwa na Dawa ya Ugonjwa Unaotokana na Matumizi ya Dawa za Kulevyta	\$0	Haihitajiki	Idhini ya awali inahitajika baada ya siku 30 za kwanza
	Huduma za Uangalizi Makini wa Mtu Binafsi	\$0	Haihitajiki	Hakuna Kikomo
	Huduma za Afya ya Akili Ambapo Mgonjwa Hurejea Nyumbani Baada ya Kutibiwa	\$0	Haihitajiki	Idhini ya awali inahitajika baada ya siku 30 za kwanza
	Huduma za Wagonjwa wa Kulazwa na Magonjwa ya Akili	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Unahitaji uidhinishaji
	Uchunguzi wa Nyurolojia (neva na mfumo wa neva) na Uchunguzi Maalum	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Unahitaji uidhinishaji
	Huduma Thabiti za Matibabu ya Jamii	\$0	Haihitajiki	Hakuna Kikomo
	Tathmini na Uchunguzi wa Afya ya Akili	\$0	Haihitajiki	Hakuna Kikomo
	Uchambuzi wa Mabadiliko ya Tabia Kulingana na Hali Husika	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Unahitaji uidhinishaji
URATIBU	Huduma za Kuratibu Matibabu	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Huduma za Usimamizi wa Kesi	\$0	Haihitajiki	Idhini hutolewa kwa mujibu wa miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo
	Huduma za Uratibu wa Uangalizi Makini wa Wagonjwa (ICC)	\$0	Uidhinishaji unahitajika	Unahitaji uidhinishaji

Huduma za kupanga uzazi

Huduma za kupanga uzazi na zinazohusiana zinapatikana kwa wanawake, wanaume, na vijana. Huhitaji rufaa kutoka kwa PCP wako ili kupata huduma za kupanga uzazi na zinazohusiana. Huduma hizi zinaweza kupatikana kutoka kwa mtoe huduma yeoyote ameafikiana na Mamlaka ya Afya ya Oregon na aliye na leseni ya kutoa huduma hizi. Huduma za kupanga uzazi na zinazohusiana ambazo hazihitaji rufaa ni pamoja na:

- Ziara za kupanga uzazi (uchunguzi wa mwili na elimu ya kupanga uzazi);
- Bidhaa za kupanga uzazi, kama tembe za kupanga uzazi na kondomu;
- Huduma za kufunga kizazi (kufunga neva za falopia na upasuaji mdogo wa kumhasi mwanaume);
- Upimaji wa saratani wa mlango wa kizazi;
- Upimaji wa ujauzito; na
- Uchunguzi wa magonjwa ya zinaa (STDs) na magonjwa yanayoambukizwa kwa ngono (STIs).

Kwa maelezo kuhusu kuharibu mimba, upimaji wa ukimwi na virusi vya ukimwi na ushauri, pigia kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja bila kutozwa ada kupitia 1-800-273-0557 (TTY 711).

Itakuwaje ikiwa mimi ni mjamzito?

Matibabu yanayotolewa unapokuwa mjamzito ni muhimu sana. Matibabu ya kabla ya kujifungua ni muhimu kwa afya yako na afya ya mtoto wako.

TRILLIUM HULIPIA:

- Matibabu ya kabla ya kujifungua (matibabu unayopokea kabla ya mtoto wako kuzaliwa);
- Uchungu wa uzazi na kujifungua;
- Matibabu ya baada ya kujifungua (matibabu unayopokea baada ya mtoto wako kuzaliwa); na,
- Matibabu kwa ajili ya mtoto wako mchanga.

Pindi tu ukijua kwamba una ujauzito, pigia kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wanachama simu. Kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wanachama kitahakikisha kwamba hupotezi mafao yako ya OHP ukiwa mjamzito.

Trillium ina mpango wa ujauzito. Pindi baada ya DHS kutuambia kuhusu ujauzito wako, tutakupigia simu ili kukuandikisha katika mpango huu.

Wanachama wa timu Trillium ya mpango wa Start Smart for Baby watawasiliana nawe wakati wa ujauzito wako ili kuhakikisha kwamba unapata matibabu unayohitaji. Timu yetu pia itakutumia maelezo kuhusu usaidizi mwingine unaoweza kupata.

Kujifungua Kusikofanyika Hospitalini:

Ikiwa ungependa kujifungua bila kuenda hospitalini (ikiwa nyumbani au kituo cha kujifungua), huduma hizi zinapatikana kuitia kwa OHP. Huduma hizi zinajumuisha matibabu ya kabla ya kujifungua na baada ya kujifungua kwa wanawake ambao wana ujauzito usio na hatari kubwa.

Ili kujifunza zaidi, tafadhali shirikiana na mtoe huduma wako. Pia unapaswa kuipigia Timu ya Kuratibu Matibabu ya KEPERO simu kuitia 1-800-562-4620. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuratibu au usafirishaji, tafadhali pigia Trillium simu kuitia 1-877-600-5472.

MUHIMU: Haraka uwezavyo baada ya mtoto wako kuzaliwa:

- Pigia Simu kwa kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wanachama. Watamwandikisha mtoto wako katika OHP.
- Ikiwa ulipokea matibabu yako yote kutoka kwa daktari wa uzazi au mtoe huduma wa matibabu ya kabla ya kujifungua wakati wa ujauzito, unahitaji kuchagua PCP mpya sasa. Pigia Trillium simu kwa usaidizi wa kuchagua PCP.
- Utapokea simu kutoka kwa wanachama wa timu ya mpango wa Start Smart for Baby ili kuona unavyoendelea na kutoa usaidizi wa ziada baada ya kujifungua, ikiwa ni pamoja na kukusaidia kupanga ziara yako ya baada ya kujifungua.

HUDUMA ZIFUATAZO ZA AFYA YA AKILI ZINAPATIKANA KATIKA MIPANGO YA KUREJEA NYUMBANI BAADA YA KUTIBIWA NA YA KIJAMII.

- Huduma za kutibiwa: tiba ya ana kwa ana, tiba ya kikundi (matibabu ya kisaikolojia na elimu ya kisaikolojia), tiba ya familia
- Huduma za matibabu ya Matumizi ya Dawa za Kulevyta
- Ufuatiliaji wa Afya ya Akili na Dawa
- Mafunzo ya ujuzi
- Ukuzaaji wa afya

- Huduma za kutunza mtoto ili uweze kupumzika
- Huduma za kazi
- Usimamizi wa kesi
- Utunzaji Binafsi
- Usaizidi wa Wenza
- Za Nyumbani
- Makazi Yanayofadhiliwa
- Usafirishaji (usafiri)
- Huduma za Migogoro

Ninaweza kufanyiwa uchunguzi wa macho na kupewa miwani?

WANACHAMA (WENYE UMRI WA BAADA YA KUZALIWA HADI MIAKA 20) WANA MAFAO YAFUATAYO:

- Uchunguzi wa uwezo wa kuona, lenzi, fremu, na kupima ikiwa miwani inafaa (wakati mwingine huitwa huduma za uchunguzi wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona).
- Uchunguzi wa matibabu wa magonjwa ya macho, majeraha ya macho, na dharura (wakati mwingine huitwa huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona).
- OHP italipia lenzi za kuweka machoni wakati ambapo miwani haiwezi kuvaliwa kwa sababu za kimatibabu. Huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona zinaweza kuhitaji idhini ya awali ili kuona mtaalamu.

WANACHAMA AMBAO NI WATU WAZIMA (UMRI WA MIAKA 21 NA ZAIDI) AMBAO NI WAJAWAZITO WANA MAFAO YAFUATAYO:

- Uchunguzi wa uwezo wa kuona, lenzi, fremu, na kupima ikiwa miwani inafaa kuliko na kikomo cha mara moja kwa kila miezi 24 (wakati mwingine huitwa huduma za uchunguzi wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona).
- Uchunguzi wa matibabu wa magonjwa ya macho, majeraha ya macho, na dharura (wakati mwingine huitwa huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona).
- OHP italipia lenzi za kuweka machoni kwa matatizo machache tu ya afya.

- Kubadilisha miwani sio mafao yanayolipiwa kwa watu wazima bila uidhinishaji wa awali. Huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona zinahitaji rufaa ili kuona mtaalamu.

WANACHAMA AMBAO NI WATU WAZIMA (UMRI WA MIAKA 21 NA ZAIDI) AMBAO SI WAJAWAZITO WANA MAFAO YAFUATAYO:

- Uchunguzi wa matibabu wa magonjwa ya macho, majeraha ya macho, na dharura (wakati mwingine huitwa huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona).
- Uchunguzi wa uwezo wa kuona ulio na kikomo cha mara moja kwa kila miaka 2 (miezi 24) baada ya kuondolewa kwa mtoto wa jicho au upandikizaji wa konea.
- Lenzi, fremu na kupima ikiwa miwani inafaa hulipiwa ndani ya siku 120 baada ya kuondolewa kwa mtoto wa jicho tu.
- OHP italipia lenzi za kuweka machoni kwa matatizo machache tu ya afya.
- Huduma za uchunguzi usio wa mara kwa mara wa uwezo wa kuona zinahitaji rufaa ili kuona mtaalamu.

Je, nitapataje dawa zangu zinazoagizwa na daktari?

Trillium hulipia dawa katika maduka mengi ya dawa ndani ya Oregon. Peleka agizo la dawa ulilopewa na daktari katika duka la dawa ambalo ni rahisi zaidi kwako kufika. Ikiwa unahitaji kuchukua dawa nje ya Oregon, duka la dawa na daktari aliyeyagiza ni lazima awe amesajiliwa na Jimbo la Oregon. Ikiwa ni dharura, pigia Trillium simu ili kuomba ondoleo la masharti ya kawaida. Trillium itakubali kuchukuliwa kwa dawa katika eneo lisilo la kuchukua dawa katika hali fulani tu. Ikiwa utalipia dawa zako, unaweza kuwasilisha ombi la kurejeshewa pesa ulizotumia. Trillium itawezekukurejeshea pesa ulizotumia katika hali fulani tu.

Trillium ina orodha rasmi ya dawa zinazoweza kuagizwa, orodha ya dawa zilizoidhinishwa, ya dawa zinazoagizwa na daktari ambazo hulipiwa na Trillium. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu dawa zinazoagizwa na daktari zinazolipiwa na bima na taratibu za usimamizi wa famasia katika www.trilliumohp.com. Dawa zilizoorodheshwa hutumiwa kwa sababu zinafanya kazi kwa ufanisi katika kutibu tatizo lako la afya na gharama yake ni

ndogo. Trillium inaweza kuungeza au kuondoa dawa au kubadilisha masharti ya kulipiwa na bima ya dawa. Ikiwa tutaondoa dawa kutoka kwenye orodha au kuungeza kizuizi kwa dawa unayotumia, tutakwambia mapema. Ikiwa daktari wako atakuagiza kutumia dawa ambayo haipo kwenye orodha ya Trillium, na daktari huyo aitumie Trillium ombi la kulipia dawa hiyo, tutazingatia ombi hilo. Tutakujulisha ikiwa ombi hilo limeidhinishwa au la. Wasiliana na daktari aliyeagiza dawa au PCP wako ili kuzungumza kuhusu machaguo yako.

Je, ni dawa zipi hazilipiwi na bima?

- Dawa ambazo hazina matumizi yaliyoidhinishwa na FDA;
- Dawa ambazo sio za lazima kimatibabu;
- Dawa za majoribio au za kufanya uchunguzi;
- Dawa za kukusaidia kupata ujauzito;
- Dawa zinazotumiwa ili kupunguza uzani;
- Dawa za vipodozi na kuwezesha kukua kwa nywele.

Trillium hulipia baadhi ya dawa zinazouzwa bila agizo la daktari (over-the-counter au OTC kwa ufupi) ambazo ziko katika orodha yetu, kama vile aspirini, ikiwa daktari wako amekuandikia agizo la dawa hiyo. Tazama orodha rasmi ya dawa zinazoweza kuagizwa katika <https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services.html> ili kuona ni dawa zipi zinazouzwa bila agizo la daktari (OTC) hulipia na bima.

Hutulipii dawa zote zinazoagizwa na daktari. Dawa nyingi ambazo watu hutumia kwa afya ya akili hulipia moja kwa moja na Mamlaka ya Afya ya Oregon (OHA). Tafadhalii mwonyeshe mfamasi wako kadi zako za Kitambulisho cha Afya cha Oregon na Kitambulisho cha Trillium. Duka hilo la dawa litajua mahali pa kutuma bili.

Ninaweza kupata dawa zangu wapi?

Unaweza kutumia duka lolote la dawa upendalo ambalo litakubali kadi yako ya Kitambulisho cha Matibabu cha Trillium. Jiandae kuonyesha kadi yako ya Kitambulisho cha Afya cha Oregon. Trillium ina maafikiano na maduka mengi ya dawa katika eneo la Kaunti ya Clackamas, Multnomah na Washington.

Unaweza kupata dawa zako zinazoagizwa na daktari kutoka kwa duka la dawa linalokubali maagizo ya barua ya posta. Huduma za Posta za Dawa Zinazoagizwa na Daktari (Postal Prescription Services) na Duka la Dawa la Maagizo ya Barua ya Posta la CVS Caremark (CVS Caremark Mail Order Pharmacy) hutoa huduma za maagizo ya barua ya posta. Ikiwa una Intaneti, unaweza kutafuta maelezo kuhusu maagizo ya barua ya posta katika: <https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services.html>

Ikiwa huna Intaneti, unaweza kupiga simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama.

Vizuizi Vingine vya Kulipiwa kwa Dawa

Baadhi ya dawa zilizo kwenye orodha zina masharti ya ziada ya kulipiwa na bima au vikomo ambavyo vinaweza kuwa ni pamoja na:

- Matumizi ya dawa za jenasi zinapopatikana
- Idhini ya awali ya Trillium
- Tiba ya hatua - kujaribu dawa zingine za gharama ya chini kwanza
- Vikomo vya kiasi

Maamuzi ya Trillium ya idhini ya awali na maondoleo ya masharti ya kawaida ya orodha ya dawa hutegemea matibabu yanayofaa na bima tu. Wafanyakazi wa Trillium hawatuzwi kwa kukataa maombi na hawatumii bahashishi za kifedha ambazo hutuza kukataliwa kwa huduma.

Trillium inaweza kuidhinisha hadi mara tatu za kuchukua dawa ya mpito ambayo haijaorodheshwa kwa wanachama ambaao walikuwa wanatumia dawa hiyo kabla ya kuwa wanachama wa Trillium au baada ya kuachiliwa kutoka hospitalini au kituo cha uuguzi. Wewe au daktari wako anaweza kuwasiliana na Trillium ili kuomba usaidizi wa kulipia dawa ya mpito.

Itakuwaje ikiwa nina Medicare?

Taarifa hii ni ya mwanachama yeote wa nyumba yako ambaye anatumia bima za Medicare na Oregon Health Plan (OHP). Mafao yao ya dawa yanaitwa Medicare Part D. Medicare huhitaji watu kulipia sehemu ya gharama kwa bima ya dawa ya Part D. Mipango mingi inayotoa mafao ya dawa hutoza malipo ya sehemu ya gharama. Trillium itaendelea kulipia huduma nyingine zote za afya zinazolipiwa na bima.

Usaidizi wa Dawa Zinazoagizwa na Daktari-Mpango wa Oregon wa Dawa Zinazoagizwa na Daktari

Mpango wa Oregon wa Dawa Zinazoagizwa na Daktari (Oregon Prescription Drug Program) unaweza kusaidia kupunguza gharama za dawa zinazoagizwa na daktari ambazo hazilipiwi na kifurushi chako cha mafao cha OHP. Mpango huu unapatikana kwa Wanaoregon wote.

Ili kujiandikisha kwa simu, piga simu kupitia 1-800-913-4284 au tembelee tovuti ya Oregon Prescription Drug katika: www.oregon.gov/OHA/pharmacy/OPDP/pages/applicationpage.aspx#What_is_O_PDP

Mpango wa Msaada wa Wagonjwa (Patient Assistance Program au PAP kwa ufupi)

Unaweza kupata dawa ambayo hailipiwi na bima bila malipo kutoka kwa kampuni inayoitengeneza. Tembelea tovuti ya kampuni inayotengeneza dawa yako ilyoagizwa na daktari kwa maelezo kuhusu mpango wao wa msaada wa wagonjwa (PAP).

Vifaa Vya Kupima Covid-19 Ni Mafao Kupitia Kwa Duka La Dawa La Eneo Lako

Je, ninawezaje kupata kipimo cha nyumbani cha COVID-19 bila malipo?

Unaweza kupata kifaa cha upimaji wa nyumbani wa COVID-19 kinachouzwa bila agizo la daktari (OTC), kilichoidhinishwa na FDA cha Uidhinishaji wa Matumizi ya Dharura (EUA), bila malipo ukitembelea mojawapo ya maduka ya rejareja ya dawa ya mtandao wa Trillium Community Health Plan. Kifaa cha kupima hakitahitaji agizo la daktari.

MUHIMU: Pata kipimo katika duka la dawa lenyewe. Usipate kipimo na kukilipia kipimo katika eneo la kulipa la kawaida la duka. Ikiwa utalipia kipimo katika eneo la kawaida la kulipa, basi utahitaji kuwasilisha fomu ya dai la dawa ilyoagizwa na daktari ili kurejeshewa pesa kwa gharama uliyolipa.

Je, kuna vipimo ambavyo havilipiwi na bima kupitia kwa duka la dawa?

Vifaa vya kupima COVID ambavyo havilipiwi na bima ni pamoja na:

- Vifaa ambavyo ni lazima vitumwe kwenye maabara (vifaa vya kukusanya)
- Vifaa ambavyo havijaandikwa kuwa ni vya "OTC"
- Vifaa vya kupima COVID vilivyopatikana nje ya Marekani

Nilinunua kifaa cha upimaji wa nyumbani wa COVID-19 mwenyewe, nitarejeshewa pesa nilizotumia?

Ndiyo. Ikiwa ulinunua kifaa cha upimaji wa nyumbani wa COVID-19 kinachouzwa bila agizo la daktari (OTC) cha EUA kilichoidhinishwa na FDA katika eneo lolote ambalo sio sehemu ya maduka ya dawa ya mtandao wetu (kama vile, Amazon, duka la mboga na matunda, duka la dawa, nk.), utarejeshewa pesa ulizotumia kwa gharama ya vifaa vya kupima (hadi \$12 kwa kila kifaa cha kupima) ifuatavyo:

- Ununuzi wa kifaa cha upimaji wa nyumbani ambacho kiko katika orodha ya EUA kilichoidhinishwa na FDA.
- Orodha ya EUA iliyoidhinishwa na FDA inaweza kupatikana katika tovuti yetu katika <https://www.trilliumohp.com/coronavirus-disease--covid-19-.html>, au wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama.
- Vipimo vinavyopatikana bila agizo la daktari vitajumuisha "OTC" (kwa vifaa vya upimaji wa nyumbani vinavyouzwa bila agizo la daktari) katika safu wima ya Sifa.
- Jaza na uwasilishe fomu tofauti ya Dai la Kurejeshewa Pesa Ulizotumia Katika Agizo la Dawa Lililotolewa na Daktari (Prescription Claim Reimbursement) kwa kila mwanachama:
 - Kwa maelekezo kamili ya jinsi ya kuwasilisha dai, tembelea tovuti yetu katika <https://www.trilliumohp.com/coronavirus-disease--covid-19-.html> au wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama.

Ikiwa ulinunua kifaa cha kupima kilichoidhinishwa na FDA/EUA kilichoagizwa na daktari kabla ya Januari 15, 2022, Trillium Community Health Plan itakurejeshea pesa ulizotumia baada ya fomu ya dai kuwasilishwa kulingana na kiasi ulicholipa.

Je, Trillium Community Health Plan itaweka kikomo kwa idadi ya vipimo ambavyo mwanachama anaweza kupokea bila malipo?

Ndiyo. Trillium Community Health Plan italipia hadi vifaa 8 vya upimaji wa nyumbani wa COVID-19 vya EUA, ambavyo ni vya OTC vilivyoidhinishwa na FDA vinavyouzwa bila agizo la daktari kwa kila mwanachama aliye na bima kwa kipindi cha siku 30 bila agizo la PCP au idhini ya awali. Vipimo visivyo na kikomo vitalipiwa na bima kwa agizo kutoka kwa mto huduma wa afya

aliye na leseni. Hili linafuata mwongozo wa shirikisho uliotolewa mnamo Januari 10, 2022.

Nitawasiliana na nani ikiwa nina maswali yoyote?

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kulipiwa kwa vifaa vya upimaji wa nyumbani wa COVID-19 au kuwasilisha dai la kurejeshewa pesa ulizotumia, pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kupitia 1-877-600-5472; TTY: 711.

HUDUMA ZA MATIBABU YA DHARURA NA MATIBABU YA HARAKA

Je, dharura ya matibabu ni nini?

Dharura ni jeraha baya au ugonjwa unaotokea ghafla, ikiwa ni pamoja na maumivu makali ambayo unafikiri yanaweza kusababisha kifo au madhara mabaya ya kimwili ikiwa hutapokea usaidizi mara moja. Hii ni pamoja na mtoto wako ambaye hajazaliwa ikiwa wewe ni mjamzito. Matibabu ya Dharura na ya Haraka hulipiwa na bima wakati wote, saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Unaweza kuenda kwa hospitali yoyote, au mazingira mengine, mahali popote ndani ya Marekani kwa dharura.

Ikiwa unafikiri una dharura halisi, pigia simu kwa 911 au uende kwa Chumba cha Dharura (Emergency Room au ER kwa ufupi) katika hospitali iliyo karibu zaidi. Huhitaji ruhusa ili kutiwiwa katika dharura.

DHARURA INAWEZA KUWA:

- maumivu ya kifua;
- kutatizika kupumua;
- usumishaji;
- kutokwa na damu bila kukoma;
- mifupa iliyovunjika; au,
- dharura ya afya ya akili.

Huduma za gari la wagonjwa

Huduma za gari la wagonjwa hulipiwa ikiwa kuna dharura.

Je, nitapataje matibabu baada ya dharura?

Matibabu ya dharura hulipiwa na bima hadi hali yako itakapokuwa thabiti. Pigia PCP wako simu kwa matibabu ya ufuatiliaji. Matibabu ya ufuatiliaji yanayotolewa baada ya hali yako kuwa thabiti hulipiwa na bima lakini hayachukuliwi kuwa dharura.

Matibabu yanayotolewa baada ya hali ya mgonjwa kuwa thabiti ni matibabu unayopokea baada ya dharura na baada ya hali yako kuwa thabiti. Ikiwa utapokea matibabu ya dharura katika hospitali ambayo sio sehemu ya mtandao wetu na unahitaji matibabu baada ya hali yako kuwa thabiti:

- Ni lazima urudi kwa hospitali ya ndani ya mtandao ili matibabu yako yalipiwe na bima, au
- Ni lazima upate idhini ya awali ili matibabu yako yalipiwe na bima.

Je, nitapataje matibabu ya haraka?

Mtu ataweza kukusaidia mchana na usiku, hata katika wikendi na likizo. Ikiwa huwezi kuwasiliana na ofisi ya PCP wako kuhusu tatizo linalohitaji kushughulikiwa haraka au hawawezi kukuona haraka inavyohitajika, unaweza kuenda kwa matibabu ya haraka bila miadi. Matatizo yanayohitaji kushughulikiwa haraka ni mambo kama

maambukizi makali, kutenguka na maumivu makali. Ikiwa unahitaji mkalimani, tafadhalii julisha kliniki.

Hata kama hujamwona PCP wako bado, mpigie simu kwanza ikiwa unafikiri tatizo lako la afya linahitaji kushughulikiwa haraka. Jina la PCP wako liko katika kadi yako ya Kitambulisho cha Trillium. Unaweza kutafuta Watoa Huduma wa Matibabu ya Haraka katika:

<https://providersearch.trilliumhealthplan.com/>

Maeneo ya Matibabu ya Haraka

AFC Urgent Care

397 Warner Milne Road, Oregon City, OR 97045
503-305-6262

Eagleton Providers PC

17437 Boones Ferry Road, Suite 100
Lake Oswego, OR 97035
413-887-6030

Urgent Care Oregon, LLC

861 W Main Street, Molalla, OR 97038
503-873-8686

Uptown Providers PC

7033 NE Sandy Boulevard, Portland, OR 97213
503-306-6262

Uptown Providers PC

25 NW 23rd Place, Suite 11, Portland, OR 97210
503-766-2215

Uptown Providers PC

14284 SW Allen Boulevard, Beaverton, OR 97005
503-305-6262

Itakuwaje ikiwa siko katika makazi yangu ya kawaida au nikiwa nje jimbo na nihitaji matibabu?

Japo Trillium hutoa bima kwa wanachama mahali popote ndani ya Marekani, wanachama wanapaswa kujua kuhusu kinachoweza kufanya ikiwa wanasaferi nje ya Oregon na wapate dharura. Hata ingawa Trillium imeidhinisha ziara ya chumba cha dharura katika jimbo lingine, hili halimaanishi kwamba watoa huduma wote wanaotoa matibabu wakati wa dharura wangependa kutoza Trillium bili. Hili linamaanisha kwamba unaweza kupokea bili kwa huduma hizo. Usipuuze bili kutoka kwa watu waliokutibu

hospitalini. Ikiwa utapata bili zingine, shirika la matibabu yanayoratibiwa (CCO) litakusaidia kusuluuhisha suala hilo.

DHARURA INAWEZA KUWA:

- maumivu ya kifua;
- kutatizika kupumua;
- usumishaji;
- kutokwa na damu bila kukoma;
- mifupa iliyovunjika; au,
- dharura ya afya ya akili.

Tafadhalii usitumie chumba cha dharura kwa vitu ambavyo vinawea kutibiwa katika ofisi ya matibabu ya haraka. Matatizo yanayohitaji kushughulikiwa haraka ni mambo kama maambukizi makali, kutenguka na maumivu makali.

HATUA ZA KUCHUKUA IKIWA INAWEZEKANA WAKATI WA ZIARA YA NJE YA JIMBO YA CHUMBA CHA DHARURA:

- Hakikisha kwamba una kadi ya Kitambulisho cha Trillium unaposafiri nje ya jimbo;
- Toa kadi yako haraka uwezavyo na uulize ikiwa wako tayari kutoza Trillium (Medicaid) bili;
- Wasiliana na Trillium na ujadili hali hiyo na kuomba ushauri kuhusu cha kufanya;
- Usitie hati zozote saini hadi utakapoja kwamba mto huduma yuko tayari kutoza Trillium (Medicaid) bili;
- Ikiwa inawezekana, acha Trillium izungumze na ofisi ya mto huduma wakati uko huko;

Wakati wa dharura, hatua zilizo hapa juu haziwezekani kila wakati. Hata hivyo, kuijandaa na kujua hatua zinazohitaji kuchukuliwa wakati wa dharura kunaweza kusuluuhisha masuala ya bili wakati ambapo bado uko katika ofisi ya mto huduma katika jimbo hilo. Kuchukua hatua hizi kunaweza kuzuia msongo wa ziada wa kupokea bili kwa huduma ambazo Trillium inaweza kulipia, lakini mto huduma akatae kutoza shirika la matibabu yanayoratibiwa (CCO) bili.

Je, nitafanya nini ikiwa nitapokea bili?

Tafadhalii usipuuze bili za matibabu - tupigie simu mara moja. Watoa huduma wengine hutuma bili ambazo hazijalipwa kwa mawakala wa kukusanya madeni na hata wanaweza kuwasilisha mashtaka mahakamani ili

kulipwa. Inakuwa vigumu zaidi kutatua tatizo hilo pindi hilo linapofanyika.

Pindi tu unapopata bili kwa huduma uliyopokea ulipokuwa unatumia OHP unapaswa:

- Kupigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha Trillium simu mara moja na kusema kwamba mtoa huduma anakutoza bili kwa huduma ya OHP. Tutakusaidia kulipa bili hiyo. Usisubiri hadi upate bili zaidi.
- Ikiwa inafaa, unaweza kukata rufaa kwa kutumia Trillium barua inayosema kwamba hukubaliani na bili hiyo kwa sababu ulikuwa unatumia OHP wakati ambapo ulipokea huduma. Hifadhi nakala ya barua hiyo kwa rekodi zako.
- Fuatilia ili kuhakikisha kwamba tulilipa bili hiyo.
- Ikiwa utapokea hati za mahakama, tupigie simu mara moja. Pia unaweza kupiga simu kwa wakili au

Nambari ya Mafao ya Umma kuitia 800-520-5292 kwa ushauri wa kisheria na usaidizi. Kuna sheria za watumiaji wa huduma ambazo zinaweza kukusaidia unapotozwa bili kimakosa huku ukitumia OHP. Kuna sheria za watumiaji wa huduma ambazo zinaweza kukusaidia unapotozwa bili kimakosa huku ukitumia OHP.

Ikiwa kwa sababu fulani Trillium itakosa kulipia huduma zako, unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo, au katuomba tufanye ukaguzi. Tazama sehemu ya "Malalamiko (Manung'uniko) na Rufaa" kwa maelezo zaidi.

OHP hulipia matibabu ya dharura na ya haraka popote ndani ya Marekani, lakini sio nje ya Marekani. Hiyo inamaanisha kwamba OHP haitalipia matibabu utakayopokea ukiwa Meksiko au Kanada.

MAFAO NA HUDUMA ZAKO ZA MENO

Je, huduma za meno ni zipi?

Huduma za meno ni sehemu ya mafao yako. Kupata uchunguzi wa mara kwa mara wa meno kwa matibabu ya kuzuia magonjwa ni muhimu kwa afya yako ya jumla na kunaweza kusaidia kuzuia ugonjwa wa meno. Ikiwa unahitaji usaidizi wa huduma zako za meno, pigia Trillium simu. Tuko hapa ili kukusaidia upate matibabu unayohitaji.

Wanachama wa Trillium wanaweza kuchagua kutoka kwa wowote kati ya mipango ifuatayo ya matibabu ya meno:

- **Advantage Dental Services** au
- **Capitol Dental Care** au
- **Oregon Dental Service.**

Nina mpango upi wa matibabu ya meno?

Utapata mpango wako uliopewa wa matibabu ya meno au Shirika la Matibabu ya Meno (Dental Care Organization au DCO kwa ufupi) kwenye Kadi yako ya Kitambulisho cha Mwanachama wa Trillium, ambayo utapokea kwa barua ya posta



Medical-Dental-Behavioral Health

Name: <John Smith>

Oregon Health Plan#: <123456789101112>

PCP Start Date: <12/05/2016>

Doctor (PCP): <Dr. Jane Doe>

RX: Envolve Rx

RXBIN: 004336

RXPCN: MCAIDADV

RXGRP: RX5481

DCO: <DCO Name>

DCO Phone: <(555) 555-1234>

Mental Health Crisis Hotline:

Multnomah Co.: 503-988-4888 | 800-716-9769

Washington Co.: 503-291-9111 | Clackamas Co.: 503-655-8585

Tafadhalii onyesha Kadi yako ya Kitambulisho cha Mwanachama wa Trillium na Kitambulisho cha Afya cha Oregon kila mara unapoenda kwa daktari wa meno. Ikiwa utapoteza Kadi yako ya Kitambulisho cha Mwanachama, tafadhalii omba mpya kwa kupiga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuitia 1-877-600-5472, TTY 711.

Je, nitachaguaje mpango wa meno?

Ikiwa hujapewa mpango wa matibabu ya meno au ungependa kubadilisha mpango wako wa matibabu ya meno, tafadhalii wasiliana na kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuitia 1-877-600-5472, TTY 711.

Je, nitatumiaje mafao yangu ya meno?

Unapopewa mpango wa matibabu ya meno, unahitaji kuchagua kliniki au ofisi ya matibabu ya meno kama Daktari wako wa Msingi wa Meno (Primary Care Dentist au PCD kwa ufupi). PCD wako atashirikiana nawe ili kushughulikia mahitaji yako ya meno. Pigia PCD wako simu kabla ya kutafuta matibabu ya meno.

Je, Nitachagua Daktari wa Msingi wa Meno Vipi?

Unaweza kuchagua Daktari wa Msingi wa Meno (Primary Care Dentist au PCD kwa ufupi) kutoka kwa kipengele cha kutafuta daktari wa meno cha Trillium Find a Dentist kwenye tovuti yetu. <https://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/benefit-information.html.html>

Au, unaweza kupiga simu kwa ofisi ya PCD wako na watasaidia kupanga miadi yako ya kwanza na PCD.

Advantage Dental Services

Huduma kwa Wateja
Nambari isiyotozwa ada 1-866-268-9631 TTY 711

Capitol Dental Care

1-503-585-5205 au bila kutozwa ada
1-800-525-6800
TTY 1-800-735-2900

Oregon Dental Service

1-503-243-2987 au bila kutozwa ada
1-800-342-0526
TTY 1-503-243-3958 au 1-800-466-6313

Je, nitapangaje miadi na Dakatari wangu wa Msingi wa Meno (PCD)?

- Mpigie PCD wako simu wakati wa saa za kazi. Unaweza kupata nambari ya simu katika sajili ya watoa huduma ya mpango wako wa matibabu ya meno au kwa kupiga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama.
- Iambie ofisi hiyo kwamba wewe ni mwanachama wa Trillium na mbona unataka kuona daktari wa meno.
- Kumbuka kupeleka Kadi yako ya Kitambulisho cha Mwanachama wa Trillium na Kitambulisho cha Afya cha Oregon kwa miadi hiyo.
- Ikiwa unahitaji lugha ya ishara au mkalimani katika miadi yako, hakikisha unawaambia wafanyakazi wa kliniki wakati utakapopanga miadi hiyo.

Ili kuratibu matibabu yako ya meno, Daktari wako wa Msingi wa Meno:

- Atahifadhi rekodi zako za matibabu ya meno katika eneo moja ili kukupatia huduma bora zaidi;
- Atatoa ufkiaji kwa matibabu ya haraka na ya dharura ya meno kwa saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki;
- Atakuwa mtu wa kwanza unayewasiliana naye unapohitaji matibabu ya meno; na
- Atapanga matibabu bobezi ya meno, ikiwa unayahitaji.

Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?

Ikiwa unahitaji usaizidi wa kufika katika miadi zako, tafadhalii pigia MTM simu bila kutozwa ada kwa 877-583-1552 (TTY: 711). Tunaweza kusaidia ikiwa huna njia ya kufika kwa daktari, daktari wa meno au mshauri wako. Unaweza kupata usaizidi wa kulipia usafiri.

Je, nitabadilishaje Daktari wangu wa Msingi wa Meno?

Unaweza kubadilisha PCD wako mara mbili kila mwaka. Ili kuchagua PCD mpya, tumia sajili ya watoa huduma kutoka kwa mpango wako wa matibabu ya meno.

Itakuwaje ikiwa ninafikiri ninahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine?

Ikiwa unafikiri unahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine, panga miadi na PCD wako kwanza. PCD wako ataamua ni huduma na vipimo vipi ambavyo unaweza kuhitaji. Ikiwa unafikiri unahitaji kuona mtaalamu au mtoe huduma mwingine, PCD wako atakupea rufaa. Rufaa hutolewa kwa kutegemea kesi binafsi wakati ambapo PCD wako anahisi kwamba zinahitajika. Mpango wako wa matibabu ya meno ni lazima uidhinishe rufaa kwanza kabla ya kuenda kwa miadi na mtaalamu au mtoe huduma mwingine.

Muhimu: Kuenda kwa mtaalamu bila rufaa kutoka kwa PCD wako kunaweza kusababisha kutolipwa kwa bili yako. Hili linaweza kumaanisha kwamba ikiwa utatia saini kwenye ondoleo, utalazimika kulipa bili hiyo

JE, NINA MAFAO YAPI YA MENO?

Muhtasari wa Mafao na Huduma

	MAFAO	WANAWAKE WAJAWAZITO NA WANACHAMA WALIO NA UMRI WA CHINI YA MIAKA 21	WATU WAZIMA WENGINE WOTE
HUDUMA ZA DHARURA:	Huduma za Dharura za Kufanya Hali ya Mgonjwa Kuwa Thabiti (ndani au nje ya eneo lako la huduma) Mifano: <ul style="list-style-type: none"> Maumivu makali mno au maambukizi Kutokwa na damu au kuvimba Majeraha ya meno au ufizi 	X	X
HUDUMA ZA KUZUIA MAGONJWA	Uchunguzi	X	X
	Kusafisha	X	X
	Matibabu ya Floraidi	X	X
	Vifaa vya kufunga kabisa	X	Hailipowi
	Vijazo	X	X
	Meno Kiasi ya Bandia	X	Imewekewa kikomo
	Meno Kamili ya Bandia	Imewekewa kikomo	Imewekewa kikomo
	Sehemu Inayoonekana ya Meno	Imewekewa kikomo	Hailipowi
UPASUAJI WA MDOMO NA MAJERAHA YA NDANI YA MENO			
	Kuondolewa Meno	X	X
	Matibabu ya Mizizi ya Meno	X	Imewekewa kikomo

*Mafao yanaweza kutegemea masharti ya idhini ya awali na vikwazo vya idadi ya nyakati za matumizi.

HUDUMA ZA MATIBABU YA DHARURA NA MATIBABU YA HARAKA YA MENO

Je, dharura ya meno ni nini?

Matibabu ya dharura ya meno yanapatikana kwa saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Dharura ni tatizo baya linalohitaji matibabu mara moja. Linaweza kuwa jeraha au ugonjwa mbaya wa ghafla. Baadhi ya mifano ya hali za dharura ni:

- Maambukizi mabaya;
- Uvimbe mbaya ulio na usaha (uvimbe ulio na usaha ni lengelenge kwenye tishu yako ya ufizi);
- Maumivu makali ya meno (maumivu ambayo hayakomi unapotumia dawa inayouzwa bila agizo la daktari ya kupunguza uchungu); na,
- Jino ambalo limeng'ooka.

Piga simu kwa 911 ikiwa unaamini una dharura.

Piga simu kwa 911 ikiwa unahitaji huduma za gari la wagonjwa, ambazo hulipiwa na bima ikiwa kuna dharura.

Pia unaweza kupokea huduma za matibabu baada ya hali yako kuwa thabiti ili kuboresha hali yako. Kwa maelezo zaidi kuhusu hospitali zilizo na huduma za dharura na huduma za matibabu ya baada ya hali ya mgonjwa kuwa thabiti, tazama "Je, nitapata daktari au mtoa huduma vipi?"

Je, huduma ya matibabu ya haraka ya meno ni gani?

Matibabu ya haraka ya meno ni matibabu ya meno yanayohitaji matibabu ya upesi lakini yasiyo ya mara moja. Baadhi ya mifano ya hali zinazohitaji kushughulikiwa haraka ni:

- Maumivu ya meno;
- Fizi zilizovimba; na,
- Vijalizio vya vijishimo vya meno vilivyopotea.

Baadhi ya huduma za meno zinaweza kuhitaji idhini ya awali kutoka kwa mpango wako wa matibabu ya meno, lakini huduma za meno za dharura au za haraka hazihitaji idhini ya awali.

Itakuwaje ikiwa siko katika makazi yangu ya kawaida na nipate dharura au kuhitaji matibabu ya haraka ya meno?

Ikiwa unasafiri nje ya eneo la huduma la Trillium na upate dharura, jaribu kuwasiliana na PCD wako kwanza (maelekezo sawa na yaliyo hapa huu). Unaweza kutafuta matibabu katika hospitali yoyote ndani ya Marekani kwa matibabu ya dharura. Ikiwa ni lazima upokee matibabu ya dharura ya meno nje ya eneo hilo, mwambie daktari wa meno atumie mpango wako wa matibabu ya meno bili iliyo na bidhaa zilizotumika na maelezo ya chati yanayofafanua dharura hiyo ya meno

Je, nitapataje matibabu baada ya dharura?

Baada ya kuona daktari wa meno kwa dharura ya meno, tafadhalii pigia PCD wako simu ili kupanga matibabu zaidi ikiwa yanahitajika.

MAFAO YA AFYA YA AKILI NA URAIBU WAKEMIKALI

Je, huduma za afya ya akili ni zipy?

Huduma za afya ya akili zinapatikana kwa mtu ye yeyote anayehitaji usaidizi kuhusu mfadhaiko, wasiwasi, matatizo ya kifamilia, mienendo migumu, au matatizo mengine ya afya ya akili yanayofanya iwe vigumu kuishi maisha unayotaka. OHP hulipia huduma nyingi zinazoweza kukusaidia.

Huduma za watoto na watu wazima zinaweza kujumuisha tiba ya ana kwa ana, tiba ya familia, tiba ya kikundi, usimamizi wa dawa, usimamizi wa kesi au kujenga ustadi. Unaweza kukutana na tabibu ambaye anaweza kupendekeza ni huduma zipy zinazoweza kukusaidia. Daima tuko tayari kuzungumza nawe ili kukusaidia kupata usaidizi unaohitaji.

Tunaweza kutoa huduma za usimamizi wa kesi kwako au kwa mpwendwa wako anayetafuta matibabu.

Muhimu: Huhitaji rufaa ili kupata huduma za afya ya akili kutoka kwa mto huduma wa mtandao wetu. Tafadhali tazama Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium kwa orodha ya watoa huduma wa mtandao wetu.

Huduma za afya ya akili za watu wazima

Watu wazima wanaweza kuchagua huduma anuwai zinazoweza kusaidia kwa matatizo ya afya ya akili kutoa kwa watoa huduma wetu wengi. Mtindo wa Matibabu Thabiti ya Jamii (Assertive Community Care) au ACT wa matibabu huwasaidia wale ambao wamelazwa hospitalini kwa ugonjwa mbaya wa akili na walio katika hatari zaidi ya kudhoofika kwa afya na mgogoro.

Timu za ACT zimejitolea kwa dhati kuwaweka watu katika jamii zao ambamo wanaweza kuimarisha ubora wa maisha yao kuitia kwa timu anuwai ya wataalamu wakarimu, ufikiaji wa nafasi nzuri za ajira na usimamizi wa kesi.

Huduma za afya ya akili za watoto

Watoto walio na changamoto za afya ya akili huhudumiwa kwa njia mbalimbali. Tiba zisizohusisha kulazwa kwa wagonjwa katika mawakala, nyumbani na shulenii husaidia kufanya tiba kuwa rahisi kumfikia kijana na familia yake.

Wakati mwngine watoto/vijana huwa na changamoto kali za afya ya akili na hujipata wakihangaika ili kufanikiwa nyumbani, shulenii na mazingira mengine. Msururu wa huduma na usaidizi unapatikana kwa mtoto/kijana na familia yake kulingana na mahitaji yake mahususi. Huduma hizi zinaweza kuwa ni pamoja na huduma pana zisizohusisha kulazwa kwa mgonjwa, mpango wa Huduma za Uangalizi Makini Zisizohusisha Kulazwa kwa Mgonjwa na Usaidizi, mpango wa Uangalizi Makini wa Mtu Binafsi, au Uratibu wa Uangalizi Makini. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kubainishaa ni huduma zipy zinakufaa zaidi, tupigie simu na tunaweza kukusaidia.

JE, NITATUMIAJE MAFAO YANGU YA AFYA YA AKILI NA URAIBU WA KEMIKALI?

Je, nitapataje matibabu ya uraibu wa kemikali (pombe na dawa za kulevyo)?

Matatizo ya pombe na dawa za kulevyo ni magumu kwa mtu na familia nzima. Ikiwa unafikiri una tatizo, omba usaidizi. Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium inaorodhesha watoa huduma wa matibabu ya uraibu wa kemikali unaoweza kupigia simu. Pia unaweza kupigia Trillium simu kwa usaidizi.

Ikiwa una mahitaji ya matibabu ya afya ya akili, unapaswa kuratibu miadi na mtoa huduma wa afya ya akili mara moja.

Ikiwa unahitaji huduma za afya ya akili mara moja, unaweza kupiga simu kwa mtoa huduma yeoyote aliyerodheshwa kwenye Sajili wa Watoa Huduma wa Trillium, au upigie Trillium simu.

Je, nitapataje mtoa huduma wa afya ya akili?

Baadhi ya watoa huduma wa Trillium hawakubali wagonjwa wapya. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kutafuta mtoa huduma anayekubali wagonjwa wapya au mtoa huduma anayezungumza lugha nyingine kando na Kiingereza, pigia Trillium simu. Kwa matibabu ya hospitalini ya mara kwa mara, ni sharti uchague hospitali iliyoorodheshwa katika Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium.

Ikiwa una intaneti, unaweza kutafuta mtoa huduma au kuchapisha sajili ya watoa huduma katika:
<http://providersearch.trilliumhealthplan.com>.

PIGIA TRILLIUM SIMU IKIWA:

- Unahitaji usaidizi wa kutafuta mtoa huduma wa afya ya akili au unahitaji mtoa huduma anayezungumza lugha nyingine kando na Kiingereza.
- Unataka kuona mtoa huduma wa afya ya akili ambaye hayupo katika Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium. Unahitaji kupata idhini ya awali kutoka kwa Trillium kwanza. Aina hii ya idhini ni ya kesi maalum tu.
- Unahitaji kubadilisha mtoa huduma wako wa afya ya akili.
- Unahitaji usaidizi wa kuratibu huduma za afya ya akili ambazo hazilipiwi na bima.

Itakuwaje ikiwa ninahitaji usaidizi wa kuchagua mtoa huduma wa afya ya akili?

Wanachama wa Trillium huchagua watoa huduma wa afya ya akili wanaowaona. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuchagua mtoa huduma wa afya ya akili, pigia Trillium simu. Ikiwa umeona mtoa huduma wa afya ya akili ambaye hajaorodheshwa kwenye Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium au unataka kubadilisha ili utumie mtoa huduma tofauti wa afya ya akili, pigia Trillium simu.

Je, nitapangaje miadi na mto huduma wangu wa afya ya akili?

Ili kuanza, unaweza kupiga simu kwa mto huduma ye yote aliyeorodheshwa katika Sajili ya Watoa Huduma wa Trillium, au upigie Trillium simu kwa usaidizi wa kuchagua mto huduma. Mara baada ya kuchagua mto huduma wa afya ya akili, unaweza kupanga miadi ili kumuona mara moja. Ikiwa huwezi kuhudhuria miadi, mpigie mto huduma wako wa afya ya akili simu haraka uwezavyo. Ikiwa utakosa kuhudhuria miadi bila kumjulisha mto huduma wako wa afya ya akili sababu, anaweza kukuomba uchague mto huduma mpya wa afya ya akili.

Huduma za Afya ya Akili Zisizolipiwa na Bima

Kuna baadhi ya huduma za afya ya akili ambazo Trillium Community Health Plan hulipii, lakini ambazo OHP italipia. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuratibu huduma hizi, kama vile matibabu ya muda mrefu ya matatizo ya kiakili, tafadhali piga simu kwa kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama. Omba kuzungumza na mratibu wa matibabu.

BAADHI YA MIFANO YA HUDUMA ZINAZOLIPIWA NA OHP LAKINI ZISIZOTOLEWA NA TRILLIUM NI:

- Baadhi ya dawa za magonjwa fulani ya akili
- Kurejeshewa pesa kwa gharama ulizolipa katika kituo cha matibabu ya kikundi ya nyumbani kwa wanachama walio na umri wa chini ya miaka 21
- Matibabu ya muda mrefu ya magonjwa ya akili kwa wanachama wenye umri wa miaka 18 na zaidi

- Utunzaji binafsi katika makazi ya ulezi ya watu wazima kwa wanachama walio na umri wa miaka 18 na zaidi

Kwa maelezo zaidi au orodha kamili, pigia kitengo cha Trillium cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472.

Je, nitapataje dawa zangu zinazoagizwa na daktari?

Trillium hulipia dawa katika maduka mengi ya dawa ndani ya Oregon. Peleka agizo la dawa ulilopewa na daktari katika duka la dawa ambalo ni rahisi zaidi kwako kufika. Ikiwa unahitaji kuchukua dawa nje ya Oregon, duka la dawa na daktari aliyeziagiza ni lazima awe amesajiliwa na Jimbo la Oregon. Ikiwa ni dharura, pigia Trillium simu ili kuomba ondoleo la masharti ya kawaida. Trillium itakubali kuchukuliwa kwa dawa katika eneo lisilo la kuchukua dawa katika hali fulani tu. Ikiwa utalipia dawa zako, unaweza kuwasilisha ombi la kurejeshewa pesa ulizotumia. Trillium itaweza kukurejeshea pesa ulizotumia katika hali fulani tu.

Pigia daktari wako au Trillium simu kwa usaidizi wa dawa zisizo kwenye orodha rasmi ya dawa zinazoweza kuagizwa au zinazouzwa bila agizo la daktari.

Hutulipii dawa zote zinazoagizwa na daktari. **Dawa nyingi ambazo watu hutumia kwa magonjwa ya akili hulipiwa moja kwa moja na Mamlaka ya Afya ya Oregon (OHA). Tafadhali mwonyeshe mfamasi wako kadi zako za Kitambulisho cha Afya cha Oregon na Kitambulisho cha Trillium. Duka hilo la dawa litajua mahali pa kutuma bili.**

HUDUMA ZA DHARURA NA MGOGORO WA AFYA YA AKILI

Je, dharura ya afya ya akili ni nini?

Dharura ya afya ya akili ni kuhisi huna udhibiti au kufanya mambo bila udhibiti, au hali ambayo inaweza kukudhuru wewe au mtu mwingine. Pata usaidizi mara moja. Usisubiri hadi kutakapokuwa na hatari halisi. Piga simu kwa Nambari ya Migogoro (Crisis Line), piga simu kwa 911, au uende kwenye Chumba cha Darura. Huduma za gari la wagonjwa hulipiwa na bima ikiwa kuna dharura. Unaweza kufikia huduma za gari la wagonjwa kwa kupiga simu kwa 911.

- Ikiwa unaishi katika Kaunti ya Clackamas, unaweza kupiga simu kwa nambari ya Kaunti ya migogoro 24-7 kuititia 503-655-8585.
- Ikiwa unaishi katika Kaunti ya Multnomah, unaweza kupiga simu kwa nambari ya Kaunti ya migogoro 24-7 kuititia 503-988-4888.
- Ikiwa unaishi katika Kaunti ya Washington, unaweza kupiga simu kwa nambari ya Kaunti ya migogoro 24-7 kuititia 503-291-9111.
- Piga simu kwa 911 ikiwa wakati wowote katika dharura hiyo utahisi kwamba hali yako sio salama. Polisi watakuja kwa anwani yako ili kukusaidia na kuwasiliana na mpango wa karibu zaidi wa migogoro.

Ikiwa mtu aliye na mgogoro ni kijana, aliye na umri wa chini ya miaka 18, unaweza kupiga simu kwa Nambari ya Migogoro ya Vijana (Youth Crisis Line) kuititia 541-689-3111, TTY 711, kupiga simu kwa 911, au kuenda kwa Chumba cha Dharura. Huduma tampa za migogoro zinapatikana kwa saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki kutoka kwa Mtaalamu Aliyehitimu wa Afya ya Akili (Qualified Mental Health Professional au QMHP kwa ufupi). Jibu la matibabu ya ana kwa ana kutoka kwa QMHP litatolewa ikiwa litaonyeshwa kiafya kulingana na simu ya dharura.

Huduma tampa za migogoro na nambari ya simu iliyotengwa ya migogoro inakusudiwa kukuza uthabiti katika mazingira ya jamii badala ya kukamatwa, kuwasilishwa katika Idara ya Dharura, au kulazwa katika

kituo cha utunzaji makini. Ikiwa unapokea Matibabu ya Nyumbani ya Uangalizi Makini ya Afya ya Akili, huduma za kushughulikia migogoro zinapatikana kwa saa 24 kwa siku. Dharura ni jeraha baya au ugonjwa unaotokea ghafla, ikiwa ni pamoja na maumivu makali ambayo unafikiri yanaweza kusababisha kifo au madhara mabaya ya kimwili ikiwa hutapokea usaidizi mara moja. Hii ni pamoja na mtoto wako ambaye hajazaliwa ikiwa wewe ni mjamzito. Matibabu ya dharura hulipiwa na bima kwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Unaweza kuenda kwa hospitali yoyote, mahali popote kwa dharura. Kwa maelezo zaidi kuhusu mahali pa kupata huduma za dharura na huduma za matibabu ya baada ya hali ya mgonjwa kuwa thabiti, tazama “Je, nitapata daktari au mtoa huduma vipi?”

Itakuwaje ikiwa siko katika makazi yangu ya kawaida na nipaye dharura?

Ikiwa una dharura ya afya ya akili na huwezi kurudi kwa Kaunti za Clackamas, Multnomah au Washington kwa matibabu, unaweza kuenda kwa chumba cha dharura cha hospitali iliyo karibu zaidi. Ziara yako ya chumba cha dharura italipiwa na bima mradi uko Marekani. Usitumie chumba cha dharura kwa matibabu yasiyo ya dharura.

Je, nitapataje matibabu baada ya dharura?

Matibabu ya dharura hulipiwa na bima hadi hali yako itakapokuwa thabiti. Pigia PCP au mtoa huduma wako wa afya ya akili simu kwa matibabu ya ufuutiliaji. Matibabu ya ufuutiliaji yanayotolewa baada ya hali yako kuwa thabiti hulipiwa na bima lakini hayachukuliwi kuwa dharura.

Je, ninaweza kupokea usafiri hadi kwa miadi yangu?

Ikiwa unahitaji usaidizi wa kufika katika miadi zako, tafadhalii pigia MTM simu bila kutozwa ada kuititia 541-682-5566 au 877 kwa 711. Tunaweza kusaidia

ikiwa huna njia ya kufika kwa daktari, daktari wa meno au mshauri wako. Unaweza kupata usaidizi wa kulipia usafiri.

MALALAMIKO (MANUNG'UNIKO) NA RUFAA

Je, nitawasilishaje lalamiko au nung'uniko?

Ikiwa hujaridhishwa na Trillium, huduma zako za afya, au mtoe huduma wako, unaweza kulalamika au kuwasilisha nung'uniko wakati wowote kwa suala lolote isipokuwa kukataliwa. Tutajaribu kufanya hali kuwa bora. Piga tu simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472 ,TTY: 711, au ututumie barua kwa anwani hii: Trillium Community Health Plan, 555 International Way, Building B, Springfield, Oregon 97477.

Pia unaweza kupiga simu kwa Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Oregon Health Plan kuititia 1-800-273-0557 ili kuwasilisha lalamiko au kuwasilisha nung'uniko. Mtoe huduma wako au mtu mwagine anaweza kukuwasilishia nung'uniko. Anahitaji kuwa na idhini yako ilioandikwa ili kufanya hivyo.

Ni lazima tulisuluhihe au kupiga simu au kukuandikia barua ndani ya siku 5 za kazi kuanzia tarehe tuliyopokea lalamiko.

Ikiwa hatuwezi kulisuluhiha ndani ya siku 5 za kazi, tutakutumia barua ndani ya siku 5 za kazi ili kueleza sababu. Tunaweza kuchukua hadi siku 30 ili kushughulikia lalamiko lako. Hatutamwambia yejote kuhusu lalamiko lako ila ukituomba tufanye hivyo. Utaarifiwa kwa lugha unayopendelea ikiwa Trillium itachukua muda zaidi ili kusuluhiha nung'uniko.

Kama kumbusho, Trillium na mtoe huduma wako hawawezi kukuchukulia hatua kwa kuwasilisha lalamiko, kushiriki katika uchunguzi, au kukataa kukubali jambo ambalo unaamini ni kinyume cha sheria. Trillium haiwezi kukuomba uondoe nung'uniko, rufaa au usikilizaji wa kesi ambaa umewasilisha.

Ikiwa huduma itakaliwa – nitaombaje rufaa?

Ikiwa huduma itakataliwa, kupunguzwa, au kukomeshwa, utapokea Taarifa ya Uamuzi Hasi wa Mafao (Notice of

Adverse Benefit Determination au NOABD kwa ufupi). Pia tutamwarifu mtoe huduma wako. Barua hiyo itaeleza jinsi ya kukata rufaa (kutuomba tubadilishe uamuzi wetu). Una haki ya kuomba kuubadilisha kuititia kwa rufaa au usikilizaji wa haki wa kesi wa jimbo. Unaweza kuomba rufaa kwa kutamka au maandishi kabla ya siku 60 kuanzia tarehe ilio kwenye barua ya Taarifa ya Uamuzi Hasi wa Mafao.

Ikiwa utanyimwa huduma au hukupokea taarifa ilioandikwa ya kukataliwa au mtoe huduma wako wa huduma za afya akikwambia kwamba utahitaji kulinia huduma ambayo hailipiwi na bima, unaweza kuomba kuititia taarifa ya kukataliwa. Taarifa ya kukataliwa itaonyesha kwamba huduma hiyo hailipiwi na bima. Baada ya kupokea kukataliwa huko, unaweza kuomba rufaa kwa Trillium.

Je, mtoe huduma wangu anaweza kuniombea rufaa?

Ikiwa umenyimwa huduma, watoa huduma wako wanaruhusiwa kuwasilisha rufaa kwa niaba yako. Tutahitaji kuititia idhini yako ilioandikwa au ya kutamka ili kufanya hivyo.

Jinsi ya Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi

Katika rufaa, mtaalamu tofauti wa huduma za afya katika Trillium atakagua kesi yako. Tuombe rufaa kwa:

- Kupigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472 ,TTY: 711; na kuomba rufaa kwa kutamka;
- Kutuandikia barua; au,
- Kujaza fomu nambari 3302 ya OHP ya Ombi la Rufaa na Usikilizaji wa Kesi. Ulitumiwa fomu hii pamoja na barua ya Taarifa ya Hatua. Pia unaweza kutupigia simu uombe fomu hii.

Ikiwa unahitaji usaidizi kuhusu hili, piga simu na tunaweza kujaza fomu ya rufaa ili uitie saini. Unaweza kuomba mtu kama rafiki au meneja wa kesi akusaidie. Pia unaweza kupiga simu kwa Nambari ya Mafao ya Umma kuititia 1-800-520-5292 kwa ushauri wa kisheria na usaidizi.

Utapata **Taarifa ya Utatuzi wa Rufaa (Notice of Appeal Resolution au NOAR kwa ufupi)** kutoka kwetu ndani ya siku 16 inayokujulisha ikiwa mkaguzi anakubaliana au kutokubaliana na uamuzi wetu. Ikiwa tunahitaji muda zaidi wa kufanya ukaguzi, tutakutumia barua inayoeleza mbona tunahitaji hadi siku 14 zaidi. Pia unaweza kuomba muda zaidi (hadi siku 14). Endapo Trillium itakosa kufuata masharti ya taarifa na wakati kwa mchakato wa kawaida au ulioongezwa muda wa rufaa, unachukuliwa kuwa umemaliza mchakato wa rufaa na unaweza kuanzisha Usikilizaji wa Haki wa Kesi wa Jimbo. Trillium itaomba muda zaidi katika mchakato wa nung'unico au rufaa ikiwa kufanya hivyo kunamfaa mwanachama tu.

Huku ukisubiri rufaa yako, unaweza kuendelea kupata huduma ambayo tayari ilikuwa imeanza kabla ya uamuzi wetu asili wa kuikomesha. Ni sharti utuombe kuendeleza huduma hiyo ndani ya siku 10 baada ya kupokea Taarifa ya Hatua ambayo iliomesha. Ikiwa utaendeleza huduma na mkaguzi akubaliane na uamuzi asili, unaweza kulazimika kulipia gharama ya huduma ulizopokea baada ya siku ya kuanza kwa matumizi iliyo katika Taarifa asili ya Hatua.

Ikiwa unahitaji usaidizi wa fomu za rufaa, piga simu kwa Trillium, kitengo cha Huduma kwa Wanachama cha OHP, au wasiliana na:

Legal Aid Services in Oregon,
Portland Regional Office
520 SW Sixth Avenue, Suite 700
Portland, OR 97204
503-224-4086 au 1-800-228-6958 (bila kutozwa ada)

Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji rufaa ya haraka (iliyoharakishwa)?

Ikiwa wewe na mtoya huduma wako mnaamini kwamba una tatizo la afya linalohitaji kushughulikiwa haraka ambalo haliwezi kusubiri rufaa ya kawaida, tuambie kwamba unahitaji rufaa ya haraka (iliyoharakishwa). Tunapendekeza ujumuushe taarifa kutoka kwa mtoya huduma wako au umwambie atupigie simu na kueleza mbona hali hiyo inahitaji kushughulikiwa haraka.

Tutakupigia simu na kukuandikia ndani ya siku moja ya kazi ili kukujuishwa kwamba tumepokea ombi la rufaa iliyoarakishwa. Ikiwa tutakubali kwamba inahitaji kushughulikiwa haraka, tutakupigia simu ili kukupatia uamuzi ndani ya saa 72. Ikiwa tunahitaji muda zaidi wa kufanya ukaguzi, tutakutumia barua inayoeleza mbona

tunahitaji hadi siku 14 zaidi. Pia unaweza kuomba kuongezwa kwa muda kwa hadi siku 14. Ndani ya siku 32 za kazi, Trillium itakutumia barua iliyoandikwa inayoeleza uamuzi na kukanifua au mtoya huduma wako kwa simu ikiwa ombi la haraka la rufaa limekataliwa.

Ikiwa rufaa yangu itakataliwa, nitapataje kikao cha watawala cha usikilizaji wa kesi?

Baada ya rufaa, unaweza kuomba usikilizaji wa haki wa kesi wa jimbo kwa Jaji wa Sheria ya Utawala wa Oregon (Oregon Administrative Law Judge). Utakuwa na siku 120 kuanzia tarehe iliyo kwenye Taarifa yako ya Utatuzi wa Rufaa (Notice of Appeal Resolution au NOAR kwa ufupi) ili kuomba usikilizaji wa kesi wa jimbo. Barua yako ya NOAR itakuwa na fomu unayoweza kutuma. Pia unaweza kutuomba tukutumie fomu ya Ombi la Rufaa na Usikilizaji wa Kesi, au upige simu kwa kitengo cha OHP cha Huduma kwa Wateja kupitia 800-273-0557, TTY 711, na uombe fomu nambari 3302.

Wakati wa kusikizwa kwa kesi, unaweza kumwambia jaji ni kwa nini hukubaliani na uamuzi wetu na mbona huduma hiyo inafaa kulipiwa na bima. Huhitaji wakili lakini unaweza kuandamana na wakili au mtu mwengine kama daktari. Ikiwa utaajiri wakili, ni sharti ulipe ada yake. Unaweza kuuliza Nambari ya Mafao ya Umma (mpango wa Huduma za Msaada wa Kisheria za Oregon na Kituo cha Sheria cha Oregon) kupitia **1-800-520-5292**, TTY 711, kwa ushauri na uwakilishaji unaowezekana. Maelezo kuhusu msaada wa kisheria wa bila malipo yanaweza kupatikana katika www.oregonlawhelp.org.

Usikilizaji wa kesi mara nyingi huchukua zaidi ya siku 30 kutayarisha. Huku ukisubiri kusikizwa kwa kesi, unaweza kuendelea kupokea huduma ambayo tayari ilikuwa imeanza kabla ya uamuzi wetu asili wa kuikomesha. Ni sharti utuombe kuendeleza huduma hiyo kabla ya siku 10 kukamilika baada ya tarehe ya NOAR. Ikiwa utaendeleza huduma hiyo na jaji akubaliane na uamuzi asili, unaweza kulazimika kulipia gharama ya huduma ulizopokea baada ya siku ya kuanza kwa matumizi iliyo katika NOAR asili.

Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji usikilizaji wa haraka (ulioharakishwa) wa kesi?

Ikiwa wewe na mtoe huduma wako mnaamini kwamba una tatizo la afya linalohitaji kushughulikiwa haraka ambalo haliwezi kusubiri usikilizaji wa kawaida wa kesi, sema kwamba unahitaji usikilizaji wa haraka (ulioharakishwa) wa kesi na kutuma fomu ya Ombi la Rufaa na Usikilizaji wa Kesi kwa faksi kwa Kitengo cha OHP cha Usikilizaji wa Kesi. Tunapendekeza ujumuise taarifa kutoka kwa mtoe huduma wako inayoeleza mbona hali hiyo inahitaji kushughulikiwa haraka. Unapaswa kupata uamuzi ndani ya siku 3 za kazi. Nambari ya faksi ya Kitengo cha Usikilizaji wa Kesi ni 1-503-945-6035.

Ikiwa ombi lako la usikilizaji wa haraka wa kesi litakataliwa, tutafanya juhudzi zinazofaa ili kumpatia mwanachama na mtoe huduma aliyetua ombi hilo taarifa ya haraka ya kutamkwa ya kukataliwa na kufuatilia kwa taarifa iliyoandikwa ndani ya siku mbili.

Je, huduma zangu zitasitishwa?

Ikiwa unapokea huduma za OHP na unataka huduma hizo ziendelee hadi usikilizaji wako wa kesi utakaposuluhishwa, unaweza kuomba uendelezaji wa mafao ndani ya siku 10 za kazi baada ya kupoakea barua ya Taarifa ya Hatua. Ikiwa uamuzi kutoka kwa usikilizaji wa kesi hautakuunga mkono, unaweza kulazimika kulipia huduma zilizoendelezwa ulizopokea huku ukisubiri uamuzi. Maelezo yote ya mwanachama yaliyotumiwa wakati wa mchakato wa Lalamiko, Rufaa na Usikilizaji wa Kesi wa Watawala huhifadhiwa kwa usalama kwa ajili yako. Unaweza kupiga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472 au TTY kuititia 711.

Je, nitafanya nini ikiwa nitapokea bili?

Hata kama huitajiki kulipa, tafadhali USIPUUZE BILI ZA MATIBABU - tupigie simu mara moja. Watoa huduma wengine hutuma bili ambazo hazijalipwa kwa mawakala wa kukusanya madeni na hata kuwasilisha mashtaka mahakamani ili kulipwa. Inakuwa vigumu zaidi kutatua tatizo hilo pindi hilo linapofanyika.

PINDI TU UNAPOATA BILI KWA HUDUMA ULIYOPKEA ULIPOKUWA UNATUMIA OHP UNAPASWA:

1. Kupigia mtoe huduma simu, umwambie kwamba ulikuwa unatumia OHP na umwombe atoze Trillium bili.

2. Kupigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia 1-877-600-5472 au TTY kuititia 711 mara moja na kusema kwamba mtoe huduma anakutoza bili kwa huduma ya OHP. Tutakusaidia kulipa bili hiyo. Usisubiri hadi upate bili zaidi.
3. Unaweza kukata rufaa kwa kumtumia mtoe huduma barua inayosema kwamba hukubaliani na bili hiyo kwa sababu ulikuwa unatumia OHP wakati ambapo ulipokea huduma. Hifadhi nakala ya barua hiyo kwa rekodi zako.
4. Fuatilia ili kuhakikisha kwamba tulilipa bili hiyo.
5. Ikiwa utapokea hati za mahakama zinazohusiana na bili hiyo, tupigie simu mara moja. Pia unaweza kupiga simu kwa wakili au Nambari ya Mafao ya Umma kuititia 1-800-520-5292 kwa ushauri wa kisheria na usaidizi. Kuna sheria za watumiaji wa huduma ambazo zinaweza kukusaidia unapotozwu bili kimakosa huku ukitumia OHP.

Ikiwa utapata bili ya huduma za afya na huna uhakika ikiwa unafaa kulipa, pigia kitengo cha Huduma kwa Wanachama simu kuititia **1-877-600-5472** au TTY kuititia 711 mara moja.

Wakati mwingine, mtoe huduma wako hukosa kujaza hati inavyofaa na kukosa kulipwa kwa sababu hiyo. Hilo halimaanishi kwamba unapaswa kulipa. Ikiwa tayari umepokea huduma hiyo na tukatae kumlipa mtoe huduma wako, mtoe huduma wako hawezu kukutoza bili. Unaweza kupoakea taarifa kutoka kwetu inayosema kwamba hatutalipia huduma hiyo. Taarifa hiyo haimaanishi kwamba unapaswa kulipa. Mtoe huduma anapaswa kufuta malipo hayo. Ikiwa sisi au mtoe huduma wako atakwambia kwamba huduma hiyo hailipwi na OHP, bado una haki ya kopinga uamuzi huo kwa kuomba rufaa au usikilizaji wa kesi.

Wajibu wa malipo

Wanachama wa Trillium hawapaswi kulazimika kulipia huduma za afya. Hakuna mtoe huduma wa kandarasi au wakala, mdhamini au mwakilishi wa kisheria wa mtoe huduma wa kandarasi anayeweza:

- kutoza mwanachama bili
- kutuma bili ya mwanachama kwa wakala wa kukusanya madeni
- kudumisha kesi ya haki za binadamu dhidi ya mwanachama ili kukusanya kiasi chochote kinachostahili kulipwa na Trillium ambacho

mwanachama hawajibikii kwa mto huduma wa kandarasi

Ikiwa utapokea bili, piga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama

Wanachama wa OHP hawalipii huduma zinazolipiwa na bima. Mto huduma wako wa afya anaweza kukutumia bili ikiwa tu yafuatayo ni kweli:

- **Huduma ya matibabu ni kitu ambacho mpango wako wa OHP haulipii;**

- Kabla ya kupokea huduma, ultia saini Mkataba halali wa Kulipa, fomu ya OHP nambari 3165 - Mkataba wa Mteja wa OHP wa Kulipia Huduma za Afya (pia huitwa ondoleo);
- Fomu hiyo ilionyesha gharama iliyokadiriwa ya huduma;
- Fomu hiyo ilisema kwamba OHP hailipii huduma hiyo; na,
- Fomu hiyo ilisema kwamba unakubali kulipa bili hiyo mwenyewe.

- **Huduma za famasia ni kitu ambacho mpango wako wa OHP haulipii;**

- Kabla ya kupokea dawa, utaombwa kutia saini Mkataba halali wa Kulipa, fomu ya OHP nambari 3166 - Mkataba wa Mteja wa OHP wa Kulipia Huduma za Famasia (pia huitwa ondoleo);
- Fomu hiyo itaonyesha gharama ya dawa;
- Fomu hiyo itasema kwamba OHP hailipii huduma hiyo; na, Fomu hiyo itasema kwamba unakubali kulipa bili hiyo mwenyewe.

Je, ni wakati upi ambapo nitalazimika kulipia huduma za afya zilizo katika OHP?

- Unaweza kulazimika kulipia huduma ambazo hulipiwa na OHP ikiwa utoana mto huduma ambayo hakubali OHP au ambaye sio sehemu ya

mtandao wetu wa watoa huduma. Kabla ya kupata matibabu au kuenda kwa duka la dawa, hakikisha kwamba liko katika mtandao wetu wa watoa huduma.

- Utalazimika kulipia huduma ikiwa hukuwa unastahiki kwa OHP ulipopokea huduma hiyo.
- Wewe, au mwakilishi anayewajibika kifedha, atalazimika kulipia huduma zisizolipiwa na OHP:
 - Ikiwa utatia saini mkataba wenye maelezo ya kina ili kulipia huduma kabla ya kuipokea.
 - Mkataba huo una orodha ya huduma zote na kiasi cha pesa zinachogharimu.
 - Hii ni pamoja na huduma zilizokataliwa chini ya idhini ya awali.
- Mkataba wa Kulipa ni halali ikiwa tu huduma hiyo imeratibiwa ndani ya siku 30 baada yako au mwakilishi wako kutia saini.
- Kutozwa salio la bili, ambayo ni mbinu ya kutoza ada kwa salio kati ya kiasi ambacho mto huduma hutoza na kiasi ambacho bima yako hulipa, hakutatumiwa wakati wowote.

Nilikuwa hospitalini na mpango wangu ulilipa hilo, lakini sasa ninapata bili kutoka kwa watoa huduma wengine. Ninaweza kufanya nini?

Unapoenda hospitalini au kwa chumba cha dharura, unaweza kutiwi na mto huduma ambaye sio mfanyakazi wa hospitali hiyo. Kwa mfano, madaktari wa chumba cha dharura wanaweza kuwa na kliniki binafsi na watoe huduma katika chumba cha dharura. Wanaweza kukutumia bili tofauti. Ikiwa utafanyiwa upasuaji hospitalini, kutakuwa na bili tofauti ya hospitali, daktari wa upasuaji, na labda hata maabara, mwanaradiolojia, na mtaalamu wa unusukaputi. Kwa kuwa tu Trillium ililipa bili ya hospitali haimaanishi kuwa Trillium ililipa watoa huduma wengine. Usipuuze bili kutoka kwa watu waliokutibu hospitalini. Ikiwa utapokea bili zingine, mpigie kila mto huduma simu na umwombe atoze Trillium bili. Unapaswa kufuata hatua 1-5 kwenye sehemu ya “Ninapaswa kufanya nini ikiwa nitapokea bili?”.

JE, NITATOA MAAMUZI YANGU YA MWISHO WA MAISHA VIPI?

Maamuzi ya mwisho wa maisha na Maagizo ya Mapema (Hati za Kisheria za Maelekezo Kuhusu Matibabu)

Agizo la Mapema ni fomu ya kisheria ambayo hukuruhusu:

1. Kushiriki maadili, imani, malengo na matakwa yako ya huduma za afya ikiwa huwezi kuyaeleza mwenyewe.
2. Kutaja mtu wa kufanya maamuzi yako ya huduma za afya ikiwa huwezi kuyafanya mwenyewe. Mtu huyu huitwa mwakilishi wako wa huduma za afya na ni lazima akubali kufanya jukumu hili.

Baadhi ya watoa huduma wanaweza kutofuta Maagizo ya Mapema. Waulize watoa huduma wako ikiwa watafuata yako. Watu wazima walio na umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kufanya maamuzi kuhusu matibabu yao, ikiwa ni pamoja na kukataa matibabu. Inaweza kufanyika kwamba siku fulani unaweza kuwa mgonjwa sana au kuumia vibaya hadi ukose uwezo wa kuwaambia watoa huduma wako ikiwa unataka matibabu fulani au la. Ikiwa una Agizo la Mapema lililoandikwa, pia linaloitwa Hati ya Kisheria ya Maelekezo Kuhusu Matibabu, watoa huduma wako wanaweza kufuata maagizo yako. Ikiwa huna Agizo la Mapema, watoa huduma wako wanaweza kuuliza familia yako cha kufanya. Ikiwa familia yako haiwezi kufanya uamuzi au itakosa kufanya uamuzi, watoa huduma wako watakupatia matibabu ya kawaida ya tatizo lako la afya.

Ikiwa hutaki aina fulani za matibabu kama mashine ya kupumua au mrija wa kulishwa, unaweza kuandika hilo katika Agizo la Mapema. Hukuruhusu kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako kabla ya kuhitaji aina hiyo ya matibabu - endapo huwezi kuyaelekeza mwenyewe, kama vile wakati ambapo uko katika hali ya kuzimia. Ikiwa una fahamu na uko macho, watoa huduma wako daima watasikiliza unachotaka.

Unaweza kupata fomu ya Agizo la Mapema katika hospitali nyingi na kwa watoa huduma wengi. Pia unaweza kupata moja mtandaoni katika <https://www.oregon.gov/oha/PH/ABOUT/Pages/AdvanceDirectiveAdoptionCommittee.aspx>

Ikiwa utaandika Agizo la Mapema, hakikisha umezungumza na watoa huduma wako na familia yako kulihusu na uwapatie nakala. Wanawea tu kufuata maagizo yako ikiwa wanayo. Ikiwa utabadilisha msimamo, unaweza kubatilisha Agizo lako la Mapema wakati wowote. Ili kubatilisha Agizo lako la Mapema, omba kurudishiwa nakala na uzirarue, au uandike LIMEBATILISHWA kwa herufi kubwa, utie saini na kuziandika tarehe. Kwa maswali au maelezo zaidi, wasiliana na kitengo cha Oregon cha Maamuzi ya Afya (Oregon Health Decisions) kupitia 1-503-692-0894, bila kutozwa ada kupitia 1-800-422-4805, au TTY kupitia 711.

Trillium haifanyi maamuzi ya kulipia matibabu kwa kuzingatia maadili au imani za kidini. Huenda ukawa na ombi ambalo daktari au hospitali fulani haiwezi kufuata kwa sababu ya imani zao za kimaadili au za kidini. Ikiwa hilo litafanyika, daktari au hospitali hiyo inapaswa kukwambia ili uweze kuamua ikiwa unataka daktari au hospitali tofauti ikuhudumie.

Ikiwa unafikiri Trillium haikufuata masharti ya agizo la mapema (inayomaanisha kile ambacho mpango unapaswa kuwalishwa wanachama katika muktadha wa Maagizo ya Mapema), unaweza kuwasilisha lalamiko kwa OHA <https://www.oregon.gov/oha/ph/providerpartnerresources/healthcareprovidersfacilities/healthcarehealthcareregulationqualityimprovement/pages/complaint.aspx> OHA: 1-800-699-9075

PIA UNAWEZA KUTUMA LALAMIKO LAKO KWA:

Health Care Regulation and Quality Improvement

800 NE Oregon St, #465, Portland, OR 97232

Barua pepe: Mailbox.hclc@state.or.us

Faksi: 971-673-0556

Simu: 971-673-0540; TTY: 711

Pia unaweza kuwasilisha lalamiko kwa Trillium. Unaweza kupiga simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama kuititia 1-877-600-5472, TTY: 711 au ututumie barua kwa anwani yetu katika: 555 International Way, Building B, Springfield, Oregon 97477.

Tamko la matibabu ya afya ya akili

Oregon ina fomu ya kuandika matakwa yako ya matibabu ya afya ya akili ikiwa una mgogoro wa afya ya akili, au ikiwa kwa sababu fulani huwezi kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako ya afya ya akili. Fomu hiyo inaitwa Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili. Unaweza kuijaza wakati ambapo unaweza kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako. Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili hutwambia aina ya matibabu unayotaka endapo utakosa uwezo wa kufanya matakwa yako kujulikana. Ni mahakama au madaktari wawili tu wanaweza kuamua ikiwa huna uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako ya afya ya akili.

Fomu hii hukuruhusu kufanya maamuzi kuhusu aina za matibabu unayotaka na usiyotaka. Inaweza kutumiwa kutaja mtu mzima wa kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako. Mtu utakayemtaja ni sharti akubali kuzungumza kwa niaba yako na kufuata matakwa yako. Ikiwa matakwa yako hayajaandikwa, mtu huyu ataamua unachotaka.

Fomu ya tamko hutumika kwa miaka mitatu (3) pekee. Ikiwa utakosa uwezo wa kufanya maamuzi ndani ya miaka hiyo mitatu (3), tamko lako litasalia kuwa halali hadi wakati ambapo unaweza kufanya maamuzi tena. Unaweza kubadilisha au kubatilisha tamko lako wakati ambapo unaweza kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako. Ni lazima umpatie Daktari wako wa Matibabu ya Msingi na mtu utakayemtaja wa kufanya maamuzi kwa niaba yako fomu yako.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili, nenda kwenye tovuti ya Jimbo la Oregon katika: <http://cms.oregon.gov/oha/amh/forms/declaration.pdf>. Ikiwa mto huduma wako atakosa kufuata matakwa yako yaliyo kwenye Tamko lako la Matibabu ya Afya ya Akili, unaweza kulalamika. Fomu ya hili inapatikana katika <https://www.oregon.gov/oha/PH/PROVIDERPARTNERRESOURCES/HEALTHCAREPROVIDERSFACILITIES/HEALTHCAREHEALTHCAREREREGULATIONQUALITYIMPROVEMENT/Pages/complaint.aspx>

TUMA LALAMIKO LAKO KWA:

Health Care Regulation and Quality Improvement
800 NE Oregon St, #465
Portland, OR 97232

Barua pepe: Mailbox.hcls@state.or.us
Faksi: 971-673-0556
Simu: 971-673-0540; TTY: 711

JE, MAELEZO YANGU YA KIBINAFSI NI YA FARAGHA?

Rekodi zako ni za faragha

Maelezo yote ya mgonjwa ni ya faragha. Hii ni pamoja na chochote kilicho kwenye rekodi yako ya matibabu na chochote unachotupatia, daktari wako au wafanyakazi wake wa kliniki. Hatushiriki maelezo haya bila idhini yako isipokuwa katika dharura, au wakati ambapo inaruhusiwa na kanuni za jimbo au za taifa.

Katika dharura, ni maelezo yanayohitajika ili kukusaidia pekee yanayoshirikiwa. Wafanyakazi wa jimbo au wa taifa wanaweza kukagua rekodi zako ili kuona ikiwa tulikupatia matibabu bora zaidi ambayo tungeweza. Daktari au kliniki yako inaweza kukuomba orodha ya kila mtu ambaye tumempatia rekodi zako.

maelezo yako katika ziara yako ya kwanza au baadaye. Fomu hiyo itaeleza ni maelezo yapi yatakayoshirikiwa, atakayepokea maelezo hayo na mbona anayahitaji. Fomu hiyo pia ina tarehe inayoonyesha kushirikiwa kutakapokoma.

Huwa tunashiriki rekodi zako kwa sababu za matibabu, upasuaji na malipo pekee. Unaweza kuweka kikomo kwa anayeona rekodi zako. Ikiwa kuna mtu ambaye hutaki aone rekodi zako, tafadhali tuambie kwa maandishi. Unaweza kutuomba orodha ya kila mtu ambaye tumempatia rekodi zako.

Sheria inayoitwa Sheria ya Kubebeba na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (Health Insurance Portability and Accountability Act au HIPAA kwa ufupi) hulinda rekodi zako za matibabu na kuzifanya kuwa za faragha. Hili pia huitwa usiri. Tuna hati inayoitwa Taarifa ya Utendaji wa Faragha (Notice of Privacy Practices) inayoeleza kwa kina jinsi tunavyotumia maelezo binafsi ya wanachama wetu. Tutakutumia ukiomba. Piga tu simu kwa kitengo cha Huduma kwa Wanachama na uombe Taarifa ya Utendaji wa Faragha.

Nitakaguaje, kusahihisha, au kuweka kikomo kwa kushirikiwa kwa Maelezo yangu ya Afya Yanayolindwa(Protected Health Information au PHI kwa ufupi)?

UNAWEZA KUWASILIANA NA TRILLIUM ILI:

- Kuomba kutazama au kunakili rekodi zako.
- Kuomba kuweka kikomo kwa jinsi ambavyo maelezo kukuhusu hutumiwa au kushirikiwa.
- Kuomba kubatilisha idhini yako.
- Kuomba kusahihisha au kubadilisha rekodi zako.
- Kuomba orodha ya nyakati ambazo Trillium ilishiriki maelezo kukuhusu.

Unaweza kuwa na nakala ya rekodi zako za matibabu. Mto huduma wako ana idadi kubwa ya rekodi zako za matibabu, kwa hivyo unaweza kumuomba nakala. Anaweza kutoza ada inayokubalika kwa nakala. Unaweza kutuomba nakala ya rekodi tulizonazo. Tunaweza kukutoza ada inayokubalika kwa nakala hizo.

Unaweza kuwa na nakala ya rekodi zako za afya ya akili isipokuwa mto huduma wako akifikiri hili linaweza kusababisha matatizo makubwa.

Trillium inaweza kukataa ombi lako la kutazama, kunakili au kubadilisha rekodi zako ikiwa mto huduma wako atasema kwamba hufai kuziona. Ikiwa ombi lako litakataliwa, utapokea barua inayokwambia mbona ombi hilo lilikataliwa na jinsi unavyoweza kuomba ukaguzi wa kukataliwa huko.

Pia utapokea maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha lalamiko kwa Trillium au Idara ya Marekani ya Huduma za Afya na Binadamu, Ofisi ya Haki za Raia.

Je, nitawasilishaje lalamiko kuhusu faragha au kuripoti tatizo la faragha?

Unaweza kuwasiliana na Trillium au Idara ya Marekani ya Huduma za Afya na Binadamu, Ofisi ya Haki za Raia, ikiwa unataka kuwasilisha lalamiko kuhusu faragha au kuripoti tatizo kuhusu jinsi ambavyo Trillium imetumia au kushiriki maelezo kukuhusu. Mafao yako hayataathiriwa na malalamiko yoyote unayotoa. Trillium haiwezi kulipiza kisasi dhidi yako kwa kuwasilisha lalamiko, kushiriki katika uchunguzi, au kukataa kukubali jambo ambalo unaamini ni kinyume cha sheria.

UNAWEZA KUWASILISHA LALAMIKO KUHUSU FARAGHA KWA BARUA YA POSTA:

Office for Civil Rights
Department of Health and Human Services
2201 Sixth Avenue
Mail Stop RX-11 Seattle, WA 98121

Kwa simu: 1-206-615-2290
Nambari isiyotozwa ada: 1-800-368-1019
TTY: 1-800-537-7697
Au, kwa faksi: 1-206-615-2297

TAARIFA YA UTENDAJI WA FARAGHA

Wafanyakazi wa Trillium ni sharti wakusanye maelezo kukuhusu ili kutoa huduma za afya. Tunajua kwamba maelezo tunayokusanya kukuhusu na afya yako ni ya faragha. Tunatakiwa kulinda maelezo haya na sheria ya taifa na jimbo. Tunaita maelezo haya Maelezo ya Afya Yanayolindwa (Protected Health Information au PHI kwa ufupi).

Taarifa ya Utendaji wa Faragha hukwambia jinsi Trillium inaweza kutumia au kushiriki maelezo kukuhusu. Sio hali zote zitaelezwa. Tunatakiwa kukupatia taarifa ya utendaji wetu wa faragha kwa maelezo tunayokusanya na kuhifadhi kukuhusu. Tunatakiwa kufuata masharti ya taarifa inayotumika kwa sasa.

Katika siku zijazo, Trillium inaweza kubadilisha Taarifa yake ya Utendaji wa Faragha. Mabadiliko yoyote yatumika kwa maelezo ambayo Trillium inayo tayari, pamoja na maelezo ambayo Trillium itapokea katika siku zijazo. Nakala ya taarifa mpya itatolewa na Trillium kama inavyohitajika kisheria.

Unaweza kuomba nakala ya Taarifa ya sasa au Utendaji wa Faragha wakati wowote unapotembelea au kuwasiliana na Trillium. Pia unaweza kuipata mtandaoni katika <http://www.trilliumohp.com>.

Jinsi ambavyo Trillium inaweza kutumia na kushiriki maelezo bila idhini yako kwa ajili ya matibabu

Tunaweza kutumia au kushiriki maelezo na watoa huduma wa matibabu ambao wanahusika katika matibabu yako. Kwa mfano, maelezo yanaweza kushirikiwa ili kubuni na kutekeleza mpango wa matibabu yako.

Kwa malipo

Tunaweza kutumia au kushiriki maelezo ili kupata malipo au kulipia huduma za afya unazopokea. Kwa mfano, tunaweza kutoa maelezo ya afya yanayolindwa (PHI) ili kuitoza OHP bili kwa huduma za afya ulizopewa.

Kwa uendeshaji wa shughuli za huduma za afya

Tunaweza kutumia au kushiriki maelezo ili kudhibiti mipango na shughuli zetu. Kwa mfano, tunaweza kutumia maelezo ya afya yanayolindwa (PHI) ili kukagua ubora wa huduma unazopokea.

Kwa matibabu ya afya ya akili

Tunaweza kushiriki au kubadilishana maelezo fulani na mipango mingine ya matibabu yanayodhibitiwa ya OHP kwa madhumuni ya shughuli za matibabu.

Kwa shughuli za afya ya umma

Trillium ni kontrakta wa OHA, wakala wa afya ya umma anayehifadhi na kusasisha rekodi za matukio ya maisha, kama vile kuzaliwa kwa watoto na vifo, na kufuatilia baadhi ya magonjwa.

Kwa shughuli za usimamizi wa afya

Trillium inaweza kutumia au kushiriki maelezo ili kukagua au kupeleleza watoa huduma wa afya.

Kama inavyotakiwa na sheria na kwa utekelezaji wa sheria.

Trillium itatumia na kushiriki maelezo wakati ambapo inatakiwa au kuruhusiwa na sheria za taifa au jimbo, au kwa agizo la mahakama.

Kwa ripoti na upelelezi wa dhuluma

Trillium inatakiwa na sheria kupokea na kupeleleza ripoti za dhuluma.

Kwa mipango ya serikali

Trillium inaweza kutumia na kushiriki maelezo kwa mafao ya umma chini ya mipango mingine ya serikali. Kwa mfano, Trillium inaweza kushiriki maelezo kwa ajili ya kubaini mafao ya Mapato ya Ziada ya Usalama (Supplemental Security Income au SSI kwa ufupi).

Ili kuepuka madhara

Trillium inaweza kushiriki maelezo ya afya yanayolindwa (PHI) na watekelezaji wa sheria ili kuepuka tishio bayla la afya na usalama wa mtu au umma.

Kwa utafiti

Trillium inaweza kutumia maelezo kwa utafiti na kubuni ripoti. Ripoti hizi haziwatambui watu mahususi.

Kufichua maelezo kwa wanafamilia, marafiki na wengine ambao wanahusika katika matibabu yako

Trillium inaweza kushiriki maelezo na watu wa familia yako au watu wengine ambao wanahusika katika matibabu yako. Una haki ya kupinga kushirikiwa kwa maelezo haya.

Matumizi mengine na kufichuliwa kwa maelezo huhitaji idhini yako iliyoandikwa

Kwa hali zingine, Trillium itaomba idhini yako iliyoandikwa kabla ya kutumia au kufichua maelezo. Unaweza kubatilisha idhini hii wakati wowote kwa maandishi. Trillium OHP haiwezi kubatilisha matumizi au ufhuzi wowote wa maelezo ambao umefanywa tayari kwa idhini yako.

Sheria zingine hulinda maelezo ya afya yanayolindwa (PHI)

Mipango mingi ya Trillium ina sheria zingine za matumizi na ufhuzi wa maelezo kukuhusu. Kwa mfano, ni sharti utoe idhini iliyoandikwa ili Trillium itumie na kushiriki rekodi zako za matibabu ya uraibu wa kemikali.

Je, haki zangu za faragha za maelezo ya afya yanayolindwa (PHI) ni zipi?

Una haki zifuatazo kuhusu maelezo ya afya ambayo Trillium huhifadhi kukuhusu.

Haki ya kuona na kupata nakala za rekodi zako za matibabu

Katika hali nyingi, una haki ya kutazama au kupata nakala za rekodi zako za matibabu. Ni lazima utoe ombi kwa maandishi. Unaweza kutozwa ada kwa gharama ya kutengeneza nakala za rekodi zako. Ikiwa unataka kupata nakala za rekodi zako, pigia Trillium simu.

Haki ya kuomba kusahihishwa au kusasishwa

kwa rekodi zako Unaweza kuomba Trillium ibadilishe au kuongeza maelezo yanayokosekana kwenye rekodi

zako ikiwa unafikiri kuna kosa. Ni lazima utoe ombi kwa maandishi na utoe sababu ya ombi lako.

Haki ya kupata orodha ya kufichuliwa kwa maelezo

Una haki ya kuomba Trillium nakala ya watu ambao wamewapatio rekodi zako ndani ya miaka sita iliopita. Ni lazima utoe ombi kwa maandishi. Orodha hii haitajumuisha nyakati ambazo maelezo yalishirikiwa kwa shughuli za matibabu, malipo au huduma za afya. Orodha hii haitajumuisha maelezo yaliyotolewa kwako au familia yako moja kwa moja, au maelezo ambayo yalitumwa kwa idhini yako.

Haki ya kuomba kuweka vikomo kwa matumizi na kufichuliwa kwa maelezo ya afya yanayolindwa (PHI)

Una haki ya kutuomba kuweka kikomo kwa jinsi ambavyo maelezo ya afya yanayolindwa (PHI) kukuhusu yanatumiwa au kushirikiwa. Ni lazima utoe ombi hilo kwa maandishi na uiambie Trillium ni maelezo yapi unayotaka kuwekeea kikomo na unataka vikomo hivyo vitumiwe kwa nani. Unaweza kuomba kizuizi(vizuizi) hicho(hivyo) kukomeshwa kwa maandishi au kwa kutamka.

JE, NITARIPOTI ULAGHAI, MATUMIZI MABAYA AU UFUJAJI UNAOSHUKIWA VIPI?

Tumejitolea kwa dhati kuzuia Ulaghai, Matumizi Mabaya na Ufujaji kwa kufuata Sheria zote Zinazohusika, ikiwa ni pamoja na, bila kikomo kwa Sheria ya Jimbo ya Madai ya Uongo (State's False Claims Act) na Sheria ya Madai ya Uongo (False Claims Act) ya shirikisho.

MIFANO YA ULAGHAI WA MTOA HUDUMA NI PAMOJA NA:

- Watoa huduma kutoza bili kwa huduma ambazo hazikufanyika au kutoza bili kwa bidhaa ambazo hazikutolewa kwa mwanachama

MIFANO YA MATUMIZI MABAYA YA MTOA HUDUMA NI PAMOJA NA:

- Watoa huduma kuagiza vipimo vyta kutambua magonjwa ambavyo havifai
- Kuagiza dawa zaidi kuliko zinazohitajika katika kutibu ugonjwa mahususi

Haki ya kuondoa ruhusa

Ikiwa utaombwa kutia saini idhini ya kutumia au kushiriki maelezo, unaweza kubatilisha idhini hiyo wakati wowote. Ni lazima utoe ombi kwa maandishi. Hili halitaathiri maelezo ambayo yameshirikiwa tayari.

Haki ya kuchagua jinsi tunavyowasiliana nawe

Una haki ya kuomba Trillium ishiriki maelezo nawe kwa njia fulani au katika eneo fulani. Kwa mfano, unaweza kuomba Trillium itume maelezo kwa anwani yako ya kazi badala ya anwani yako ya nyumbani. Ni lazima utoe ombi hili kwa maandishi. Huhitaji kueleza msingi wa ombi lako.

Haki ya kuwasilisha lalamiko

Una haki ya kuwasilisha lalamiko ikiwa hukubaliani na jinsi ambavyo Trillium imetumia au kushiriki maelezo kukuhusu.

Haki ya kupata nakala ya karatasi ya taarifa hii

Una haki ya kuomba nakala ya karatasi ya haki yako wakati wowote.

MIFANO YA UFUJAJI WA MTOA HUDUMA NI PAMOJA NA:

- Maduka ya dawa bila kukusudia kutoza bili kwa dawa za majina ya chapa wakati dawa za jenasi zinapatikana
- Watoa huduma bila kukusudia kutoza bili kwa huduma zisizohitajika za matibabu

MIFANO YA ULAGHAI WA MWANACHAMA NI PAMOJA NA:

- Mtu mwengine kando na mwanachama kutumia kadi ya kitambulisho cha mwanachama ili kupata huduma au bidhaa za matibabu

MIFANO YA MATUMIZI MABAYA YA MWANACHAMA NI PAMOJA NA:

- Kutochukua dawa kutoka kwa Duka la Dawa

MIFANO YA UFUJAJI WA MWANACHAMA NI PAMOJA NA:

- Kupata huduma zisizohitajika za matibabu

KUUNGANISHA HUDUMA ZAKO ZA AFYA

Kama mwanachama, una haki ya kuripoti Ulaghai, Matumizi Mabaya na Ufujaji bila utambulisho wako kujulikana na kulindwa chini ya sheria zinazohusika za Mtu Anayefichua Taarifa Kuhusu Shughuli Isiyo Halali (Whistleblower). Trillium itatuma ripoti za ulaghai, matumizi mabaya au ufujaji unaoshukiwa kwa mawakala wanaofaa. Nambari ya simu iliyotengwa inapatikana ya kutuambia kuhusu ulaghai au ufujaji.

Ikiwa unafikiri makosa, ulaghai, matumizi mabaya au ufujaji umefanyika, ripoti hilo haraka uwezavyo! Kutuambia kutasaidia kuwazuia wanachama wengine kuwa waathiriwa. Kutuambia pia kutasaidia kuokoa mafao yako ya huduma za afya. Ikiwa una mashaka kuhusu maelezo Ufafanuzi wako wa Mafao au umaamini huenda kuna makosa, ulaghai, matumizi mabaya au ufujaji, tafadhalii wasiliana nasi.

Kwa simu

Nambari ya Faragha ya Ulaghai, Matumizi Mabaya na Ufujaji, Bila kutozwa ada 1-866-685-8664

Huduma kwa Wanachama

Bila kutozwa ada 1-877-600-5472 TTY 711

Ana kwa ana

13221 SW 68th Pkwy #200, Tigard, OR 97223

Kwa Barua ya Posta

Trillium Community Health Plan, P.O. Box 11740 Eugene, Oregon 97440-3940

Pia unaweza kuripoti unachoamini kuwa ulaghai, matumizi mabaya na ufujaji kwa:

Ofisi ya Inspeksa Mkuu

Bila kutozwa ada 1-800-HHS-TIPS au 1-800-447-8477, TTY 1-800-377-4950

Mahali pa Kuripoti Kisa cha Ulaghai au Ufujaji wa Mtoa Huduma

Medicaid Fraud Control Unit (MFCU) Oregon Department of Justice

100 SW Market Street, Portland, OR 97201

Simu: 971-673-1880, Faksi: 971-673-1890

OHA Program Integrity Audit Unit (PIAU)

3406 Cherry Ave. NE, Salem, OR 97303-4924

Faksi: 503-378-2577, Nambari iliyotengwa ya simu: 1-888-FRAUD01 (888-372-8301)

Tovuti: <https://www.oregon.gov/oha/FOD/PIAU/Pages/Index.aspx>

Mahali pa Kuripoti Kisa cha Ulaghai au Ufujaji wa Mwanachama

DHS/OHA Fraud Investigation

PO Box 14150, Salem, OR 97309

Nambari iliyotengwa ya simu: 1-888-FRAUD01 (888-372-8301), Faksi: 503-373-1525 Kumbuka: Nambari iliyotengwa ya simu Tovuti: <https://www.oregon.gov/dhs/ABUSE/Pages/fraud-reporting.aspx>

Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson)

Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson) ni afisa wa umma ambaye hufanya kazi kama mpatanishi asiyependelea kati ya watu na mashirika.

Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (ombudsperson) ndani ya Oregon anapatikana katika:

500 Summer St NE Salem, Oregon 97301

Faksi 503-947-2341

Unaweza kuomba usaidizi kwa Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson) wa OHA kwa kupiga simu bila kutozwa ada kwa 1-877-642-0450 (TTY 711).

MACHAGUO MAPYA YA KUDHIBITI REKODI ZAKO ZA KIDIJITALI ZA AFYA

Mnamo Julai 1, 2021, kanuni mpya ya shirikisho inayoitwa Kanuni ya Uwezo wa Kushiriki Maelezo na Ufikiaji wa Mgonjwa (Interoperability and Patient Access Rule CMS 915 F) ilifanya iwe rahisi kwa wanachama kupata rekodi zao za afya wanapozihitaji zaidi. Sasa una ufikiaji kamili kwa rekodi zako za afya kwa simu yako, jambo linalokuruhusu kudhibiti afya yako vyema zaidi na kujua ni rasilimali zippi zinapatikana kwako.

Fikiri:

- Unaenda kwa daktari mpya kwa sababu huhisi vyema na daktari huyo anaweza kupata historia yako ya afya ya miaka mitano iliyopita.
- Unatumia sajili iliyosasishwa ya watoa huduma ili kupata mtoa huduma au mtaalamu.
- Mtoa huduma au mtaalamu huyo anaweza kutumia historia yako ya afya ili kutambua ugonjwa wako na kuhakikisha kwamba unapata matibabu bora zaidi.
- Unaenda kwa kompyuta yako ili kuona ikiwa dai lako limelipwa, limekataliwa au linachakatwa bado.
- Ikiwa unataka, unachukua historia yako ya afya unapobadilisha mipango ya afya.*

Mnamo 2022, wanachama wanaweza kuanza kuomba kuhamishwa kwa rekodi zao za afya wanapobadilisha mipango ya afya.*

KANUNI MPYA INAFANYA IWE RAHISI KUPATA MAELEZO KUHUSU:**

- madai (yaliyolipwa na kukataliwa)
- sehemu mahususi za maelezo yako ya afya
- bima ya dawa za famasia
- watoa huduma wa afya

***Unaweza kupata maelezo ya tarehe za huduma mnamo au baada ya Januari 1, 2016.*

Kwa maelezo zaidi, tembelea akaunti yako ya mtandaoni ya mwanachama.

MANENO YA KUJUA

Hatua: (1) Kukataliwa au idhini yeny kikomo ya huduma iliyoombwa, ikiwa ni pamoja na aina au kiwango cha huduma; (2) Kupunguzwa, kusimamishwa au kukomeshwa kwa huduma iliyodhinishwa hapo awali; (3) Kukataliwa, kikamilifu au kwa sehemu ya malipo ya huduma; (4) Kukosa kutoa huduma kwa wakati unaofaa, kama inavyobainishwa na jimbo; (5) Ukosefu wa CCO wa kuchukua hatua ndani ya kipindi cha muda kilichotolewa katika 438.408(b); au, (6) Kwa mkazi wa eneo la kijiji aliye na CCO moja, kukataliwa kwa ombi la msajiliwa wa Oregon Health Plan la kutumia haki zake chini ya 438.52(b)(ii), ili kupata huduma nje ya mtandao.

Matibabu ya Uangalizi Makini ya Kulazwa kwa Ugonjwa wa Akili:

Matibabu ya Uangalizi Makini ya Kulazwa kwa Ugonjwa wa Akili: Matibabu unayopokea hospitalini. Aina hii ya matibabu ni lazima iidhinishwe.

Agizo la Mapema: Hati inayokuruhusu kueleza matakwa yako kuhusu matibabu mwishoni mwa maisha.

Rufaa: Wakati ambapo unaomba mpango kubadilisha uamuzi usiokubaliana nao kuhusu huduma ambayo daktari wako aliagiza. Unaweza kuandika barua au kujaza fomu ukieleza mbona mpango unapaswa kubadilisha uamuzi wake. Hili linaitwa kuwasilisha rufaa.

Miadi: Ziara na mtoa huduma.

Afya ya Akili: Inajumuisha matibabu ya afya ya akili na ugonjwa unaotokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Mpango wa Matibabu: mpango wa wanachama wanaotumia huduma za Usimamizi wa Kesi, Uratibu wa Matibabu au Uratibu wa Uangalizi Makini wa Wagonjwa. Mpango wa matibabu husaidia kutoa matibabu ya jumla ya mtu. Unaeleza usaidizi, matokeo, shughuli na rasilimali zinazohitajika ili kutimiza malengo binafsi, afya na usalama wa mwanachama. Mpango huo ni shirikishi, umeunganishwa na unazingatia nyanja mbalimbali. Unaweza kuangalia mahitaji ya matibabu, kijamii, kitamaduni, kimaendeleo, kitabia, kielimu, kiroho na kifedha ili kupata matokeo bora ya afya na ustawi.

Usimamizi wa Kesi: Huduma za kukusaidia kupokea matibabu yanayofaa kutoka kwa mawakala wengine.

Mpango wa CHOICE (UCHAGUZI): Mpango wa CHOICE (UCHAGUZI) huwasaidia watu wazima walio na

ugonjwa wa akili kuishi katika mazingira yeny vizuizi vichache zaidi yaliyo na uwajibikaji wa ndani na uratibu wa matibabu, huduma maalum za kijamii na usaidizi wa mpito.

Ushauri: Ushauri unaotolewa kutoka kwa mtoa huduma mmoja kwa mwingine anayehusika katika matibabu yako.

Shirika la Matibabu Yanayoratibiwa (Coordinated Care Organization au CCO kwa ufupi): CCO ni shirika la kijamii linaloundwa na aina zote za watoa huduma wa afya wanaoungana ili kusaidia afya ya watu, familia na jamii.

Sehemu ya gharama unayostahili kulipa: Kiasi cha pesa ambacho ni sharti mtu alipe mwenyewe kwa kila huduma ya afya. Wanachama wa Oregon Health Plan hawalipi sehemu ya gharama kwa huduma. Bima binafsi ya afya na Medicare wakati mwingine huwa na sehemu ya gharama ambayo mwanachama anapaswa kulipa kwa huduma.

Vifaa vya Kudumu vya Afya (Durable Medical Equipment au DME kwa ufupi):

Vifaa vya Kudumu vya Afya (Durable Medical Equipment au DME kwa ufupi): Vifaa kama viti vyaa magurudumu, vifaa vya kutembea na vitanda vya hospitali. Vinaitwa vya kudumu kwa sababu huwepo kwa muda mrefu. Huwa haviishi kama dawa.

Hali ya Matibabu ya Dharura: Ugonjwa au jeraha linalohitaji matibabu mara moja. Hii inaweza kuwa kutokwa na damu kusikokoma, maumivu makali au mifupa iliyovunjika. Inaweza kuwa kitu ambacho kinaweza kufanya sehemu fulani ya mwili wako kuacha kufanya kazi vyema. Tatizo la dharura la afya ya akili ni kujihisi hunu udhibiti, au kuhisi kama kwamba unataka kujiumiza au kumuumiza mtu mwingine.

Usafirishaji (usafiri) wa Dharura: Kutumia gari la wagonjwa au ndege ya wagonjwa (Life Flight) ili kupata matibabu. Wahudumu wa matibabu ya dharura (Emergency medical technicians au EMT kwa ufupi) hutoa matibabu wakati unasafiri kwa gari au ndege.

Chumba cha Dharura na Idara ya Dharura (ER na ED): Chumba cha Dharura (Emergency room) na Idara ya Dharura (Emergency Department), eneo katika hospitali ambapo unaweza kupata huduma ya dharura ya matibabu au afya ya akili.

Huduma za Dharura: Matibabu ambayo huimarisha au kuleta utulivu kwa matatizo mabaya ya ghafla ya afya au ya afya ya akili.

Huduma Ambazo Hazijajumuishwa: Vitu ambavyo mpango wa afya haulipii. Huduma za kuimarisha mwonekano wako, kama upasuaji wa mapambo, na vitu ambavyo hupona vyenyewe kama homa, kwa kawaida havijumuishwi.

Nung'uniko: Lalamiko kuhusu mpango, mto huduma au kliniki. Sheria inasema kwamba mashirika ya matibabu yanayoratibiwa (CCOs) ni lazima yajibu kila lalamiko.

Huduma na Vifaa vya Kusaidia Kurejea kwa Hali ya Kawaida: Huduma za afya ambazo hukusaidia kudumisha, kujifunza na kuboresha ujuzi na utendakazi wa kila siku.

Bima ya Afya: Mpango unaolipia huduma za afya. Baada ya kujisajili kwenye mpango huo, kampuni au wakala wa serikali hulipia huduma za afya zinazolipiwa na bima. Baadhi ya mipango ya bima huhitaji malipo ya kila mwezi, yanayoitwa ada ya kujisajili (premiums).

Tathmini ya Hatari ya Afya/Uchunguzi wa Hatari ya Afya: Orodha ya maswali ambayo hutusaidia kujua mahitaji yako maalum ya huduma za afya vyema zaidi.

Huduma za Afya za Nyumbani: Huduma unazopata ukiwa nyumbani ili kukusaidia kuishi vyema zaidi baada ya upasuaji, ugonjwa au jerahia. Usaidizi wa dawa, vyakula na kuoga ni baadhi ya huduma hizi.

Huduma za Wagonjwa Mahututi: Huduma za kumfariji mtu anayekufa na familia yake. Huduma za wagonjwa mahututi zinaweza kubadilika kulingana na hali husika na zinaweza kujumuisha matibabu, ushauri na utunzaji wa muda.

Matibabu ya Kulazwa Hospitalini na Kurejea

Nyumbani Baada ya Kutibiwa: Matibabu ya kulazwa hospitalini ni wakati ambapo mgonjwa hulazwa hospitalini na kukaa huko kwa angalau usiku 3. Matibabu ya kurejea nyumbani baada ya kutibiwa ni upasuaji au matibabu unayopokea hospitalini na kisha kuondoka baadaye.

Uratibu wa Uangalizi Makini wa Wagonjwa (ICC):

Kiwango cha juu cha huduma za kuratibu matibabu. ICC husaidia matatizo na mahitaji changamano ya matibabu. Mwanachama ye yeyote anayehitaji usaidizi anaweza kuutafuta bila kupewa rufaa. Meneja wa kesi atawasiliana nawe.

Uchunguzi wa Awali wa Hatari: Fomu fupi ya uchunguzi ya kutusaidia kubainisha ikiwa kuna jambo lolote tunaloweza kukusaidia kuhusu.

Huduma za Mkalimani: Wakalimani wa lugha au wa ishara kwa ajili ya watu ambao hawazungumzi lugha sawa na mto huduma wao au watu wenye ulemavu wa kusikia.

Mtaalamu wa Tiba Aliye na Leseni: Mtu ambaye amefuzu kutoa maagizo ya dawa.

Huduma Zilizo na Kikomo: Huduma za Afya ya Akili ambazo ni sehemu ya gharama zake tu hulipiwa na bima. Unaweza kulazimika kulipia huduma hizi ikiwa unajua kwamba huduma hizo zimekekwa kikomo na ukubali kupokea matibabu hata hivyo. Hii inajumuisha huduma zinazozidi zile zinazohitajika ili kubainisha tatizo.

Zinazohitajika Kimatibabu: Huduma na bidhaa ambazo zinahitajika ili kuzuia, kutambua au kutibu tatizo la afya au dalili zake. Pia zinaweza kumaanisha huduma ambazo zinakubaliwa katika taaluma ya tiba kama matibabu ya kawaida.

Mpango wa Afya wa Tiba: Mpango wa afya amba una kandarasi na Mamlaka ya Afya ya Oregon (Oregon Health Authority au OHA kwa ufupi). Mpango huu hutoa huduma za matibabu, upasuaji, kuzuia magonjwa na uraibu wa kemikali.

Usimamizi wa Matumizi ya Dawa: Kuagiza na kufuatilia dawa zako, lakini bila kulipia gharama ya dawa zako.

Agizo la Afya ya Akili: Hati inayoeleza matibabu unayotaka endapo utakosa uwezo wa kufanya maamuzi mema kutokana na ugonjwa wa akili.

Mtandao: Watoa huduma wa matibabu, afya ya akili, afya ya meno, famasia na vifaa ambao wameafikiana na shirika la matibabu yanayoratibiwa (CCO).

Mtoa Huduma wa Mtandao: Mtoa huduma ye yeyote aliye kwenye mtandao wa CCO. Ikiwa mwanachama ataona watoa huduma wa mtandao, mpango hutoa malipo. Baadhi ya wataalamu wa mtandao huhitaji wanachama kupata rufaa kutoka kwa mto huduma wao wa msingi wa matibabu (PCP).

Mtoa Huduma Asiye wa Mtandao: Mtoa huduma ambaye hajatia mkataba saini na CCO, na ambaye huenda asikubali malipo ya CCO kama malipo kamili ya huduma zake.

Mchunguzi wa Malalamiko ya Wanachama (Ombudsperson): Mtu asiyependelea upande wowote

ambaye sio sehemu ya mpango wa afya, ambaye huwasaidia wanachama kusuluhisha malalamiko.

Mtoa Huduma wa Nje ya Mtandao: Mtoa huduma ambaye hajatia mkataba saini na CCO, na ambaye huenda asikubali malipo ya CCO kama malipo kamili ya huduma zake.

Afyaya Mwili: Afya inayohusiana na mwili wako.

Huduma za Daktari: Huduma unazopokea kutoka kwa daktari.

Mpango: Shirika la matibabu, afya ya meno, afya ya akili au CCO linalolipa huduma za afya za wanachama wake.

Ada ya Usajili: Kiasi cha pesa kinachopaswa kulipwa kwa ajili ya hati ya bima.

Idhini ya Awali (Uidhinishaji wa Awali yaani Prior Authorization au PA kwa Kiingereza): Hati inayosema kwamba mpango wako uthalipia huduma. Baadhi ya mipango na huduma huhitaji idhini ya awali kabla ya kupata huduma. Madaktari hushughulikia hii kwa kawaida.

Dawa Zinazoagizwa na Daktari: Dawa ambazo daktari wako hukwambia utumie.

Bima ya Dawa Zinazoagizwa na Daktari: Bima ya afya au mpango ambao husaidia kulipia dawa zinazoagizwa na daktari.

Mtoa Huduma wa Msingi wa Matibabu (PCP): Pia anajulikana kama "PCP", huyu ni mtaalamu wa afya ambaye hushughulikia afya yako. Kwa kawaida huwa mtu wa kwanza unayempigia simu unapokuwa na matatizo ya afya au unapohitaji matibabu. PCP wako anaweza kuwa daktari, muuguzi, msaidizi wa daktari, mtaalamu wa tiba maungo, au wakati mwingine daktari wa tiba asili.

Daktari wa Msingi wa Matibabu: Daktari wa msingi wa matibabu (primary care physician au PCP kwa ufupi), ni daktari ambaye huwa mtu wa kwanza

wa kuwasiliana naye kwa mtu aliye na tatizo la afya ambalo halijatambuliwa na ambaye hutoa matibabu yanayoendelea ya matatizo tofauti ya afya.

Daktari wa Msingi wa Meno: Daktari wa meno unayemwendea kwa kawaida ambaye hutunza meno yako na fizi.

Mtoa Huduma: Mtu au wakala yeyote anayetoa huduma za afya.

Huduma za Kurejesha Hali ya Kawaida: Huduma maalum za kuimarisha nguvu, utendakazi au tabia, kwa kawaida baada ya upasuaji, jeraha au matumizi ya dawa za kulevyaa.

Kutafuta Huduma Bila Kupewa Rufaa: Humaanisha kwamba huhitaji ruhusa kutoka kwa daktari wako wa msingi anayekutibu ili kupata matibabu.

Utunzaji Stadi wa Uuguzi: Usaидizi kutoka kwa muuguzi wa kutunza kidonda, tiba au kutumia dawa yako. Unaweza kupata utunzaji stadi wa uuguzi hospitalini, katika kituo cha uuguzi au nyumbani kwako kwa huduma za afya za nyumbani.

Mtaalamu: Mtaalamu wa tiba ambaye amepokea mafunzo maalum ya kutibui sehemu fulani ya mwili au aina ya ugonjwa.

Usikilizaji wa Haki wa Kesi wa Jimbo: Usikilizaji wa kesi wa OHA kuhusu hatua ya kunyima, kupunguza au kusitisha mafao. Mwanachama wa OHP au Mwakilishi wa Mwanachama anaweza kuomba kusikizwa kwa kesi.

Matibabu ya Haraka: Matibabu ambayo unahitaji katika siku hiyo hiyo kwa maumivu makali, kuzuia jeraha au ugonjwa kuwa mbaya zaidi, au ili kuepuka kupoteza utendakazi katika sehemu ya mwili wako.

MADOKEZ

MADOKEZ

